

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA SITA

Kikao cha Ishirini - Tarehe 6 Julai, 2004

(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2004/2005.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MAKAMU MWENYEKITI WA
KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:**

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 188

Mradi wa Umwagiliaji

MHE. IBRAHIMU W. MARWA (k.n.y. MHE. TEMBE K. NYABURI)
aliuliza:-

Kwa kuwa mapema mwaka 2002 Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula alitoa wito Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge kuhimiza Wilaya zetu kupitia Ofisi za Kilimo Wilayani kuandika miradi ya umwagiliaji ya zamani ambayo ilihitaji kufuatiliwa; na kwa kuwa Wilaya ya Bunda pamoja na Miradi mingine, iliandika Miradi ya Nyatwali na Tamau na Serikali iliahidi kutenga fedha kwa ajili ya miradi hiyo:-

(a) Je, hadi kufikia tarehe ya kujibisha kwa swali hili ni fedha kiasi gani zimepelekwa Bunda kwa lengo la kutekeleza miradi niliyoitaja?

(b) Kama fedha zilipelekwa, je, Serikali ina taarifa kama miradi imekamilika au bado na kama bado haijakamilika ni lini inatarajiwaa kutekelezwa na kukamilika?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tembe Kerenge Nyaburi, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kuanzia mwaka wa 2003/2004, Wizara ya Kilimo na Chakula ilianza kuwahimiza na kuwasaidia wakulima kuanzisha mashamba ya kilimo cha umwagiliaji maji mashambani kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria katika eneo linalozunguka ziwa hilo kwa lengo la kutengeneza ukanda wa kijani. Katika mpango huo, Skimu za Nyatwali na Tamau zenyeh hekta 20 kila moja katika Wilaya ya Bunda, zimeainishwa. Kazi zilizoainishwa ambazo zinaendelea kutekelezwa katika mwaka wa 2004/2005 ni ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani ikiwa ni pamoja na ukarabati wa mifereji na pampu za kusukumia maji.

Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, imewasaidia wakulima wa Tamau kuunda kikundi cha umwagiliaji maji mashambani. Taratibu za kakisajili kikundi hicho kisheria zinafanywa na kinatarajiwaa kusajiliwa katika mwaka wa 2004/2005.

Kwa upande wa Skimu ya Nyatwali, shughuli za usanifu zimekamilika. Hadi sasa fedha zilizotolewa kwa miradi yote miwili ni shilingi milioni 50. Kati ya hizo, shilingi milioni 40 zimetolewa na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na shilingi

milioni 10 zimetolewa na Serikali. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwaka huu wa 2004/2005.

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii, ili niweze kuuliza maswali kama ifuatavyo:-

(a) Pamoja na majibu ya Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, kuhusu maswali ya msingi yaliyoulizwa na Mbunge wa Bunda, sijui kama Waziri ana taarifa kwamba, fedha hizi hazikupelekwa kwenye miradi hii? (*Makofî*)

(b) Je, Waziri atalieleza nini Bunge lako Tukufu kwamba fedha hizi badala ya kupelekwa katika Mradi huu wa Nyatwali na Tamaau, fedha hizi zimepelekwa Wilaya ya Magu na bado analiambia Bunge kwamba fedha zimepelekwa kwenye Miradi hii ya Bunda? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, fedha kutoka *UNDP* mara nyingi hazifiki moja kwa moja kwenye Wizara, zinapitishwa kwa mwakilishi wao wa *UNDP* wa kanda hiyo. Kwa hiyo, naomba awe na subira. Zile hela hawaipi Wizara yenye moja kwa moja. Tukishaandaa kila kitu malipo yanafanyika kupitia mwakilishi wa *UNDP* wa eneo husika. Sasa hizi nyingine anazozitaja za Serikali ni, kweli hazikupelekwa moja kwa moja kwenye mradi kwa sababu kwanza sasa hivi inafanyika *design* na malipo mengine yanafanyika kupitia ofisi yetu ya kanda. Sasa ukanda wa ziwa ukianzia Ngara, Karagwe, kuzunguka Mwanza mpaka Mara, mwakilishi wa Wizara ya Kilimo anaitwa *irrigation engineer* wa kanda na maskani yake ni Mwanza. Kwa hiyo, baada ya taratibu hizi naomba tuonane nimirambulisse. Vinginevyo pesha ziko katika ofisi ya kanda na zitalipwa. (*Makofî/Kicheko*)

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuuliza swali kama ifuatavyo: Sasa hivi Naibu Waziri ametuambia fedha zilishapelekwa au Wizara ilipeleka shilingi milioni 10 na *UNDP* ikapeleka shilingi milioni 40. Sasa anasema kwamba hajui, tunataka jibu kamili, je, fedha zimekwenda ama hazijakwenda? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, fedha zimepelekwa lakini kupitia Ofisi ya Kanda Mwanza. Sasa kama ni kupeleka tumepeleka, kufika kule ni katika utekelezaji wa mradi na mradi haujaisha. Kwa hiyo, naomba awe na subira fedha zipo kule. Kwa maeleo zaidi tafadhari tuonane baada ya kikao. (*Makofî/Kicheko*)

Na. 189

Baa la Njaa Nchini

MHE. OSCAR T. MLOKA aliuliza:-

Kwa kuwa kutokana na ukame usiokuwa wa kawaida ambao uliikumba nchi yetu, wakulima wa Jimbo la Morogoro Mjini wamekosa mavuno kiasi kwamba sasa hawana hata mbegu za kupanda msimu ujao. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao chakula na mbegu za bei nafuu ili njaa isiendelee kuota mizizi msimu ujao?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Oscar Thobias Mloka, Mbunge wa Morogoro Mjini, kama ifuatavyo:-

Serikali imekuwa ikifuatilia na kutathmini hali ya chakula nchini kwa kipindi chote cha msimu wa 2002/2003. Tathmini ya kina ya kutambua kaya na idadi ya watu walioathirika zaidi na upungufu wa chakula iliyofanyika mwezi wa Juni na Julai, 2003 kwa kushirikisha wadau mbalimbali wa masuala ya chakula, ilibaini kwamba katika Mkoa wa Morogoro, Wilaya za Morogoro Vijijini, Mvomero na Ulanga, ndizo zilizoathirika zaidi na upungufu wa chakula.

Aidha, tathimini iliyorudiwa mwezi Februari, 2004 na Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Ushirika na Masoko, Taasisi ya Chakula na Lishe na Mamlaka ya Hali ya Hewa, ilibaini kuwa Morogoro Mjini watu wapatao 1,993 waliathirika na upungufu wa chakula na kuhitaji tani 48 za chakula kwa kipindi cha miezi ya Machi hadi Aprili 2004, ambapo mavuno mapya ya msimu wa 2003/2004 yalianza kupatikana. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilitoa tani 1,000 za mahindi kutoka Hifadhi ya Chakula ya Taifa kwa Mkoa wa Morogoro ya kuuzwa kibiashara chini ya usimamizi wa Uongozi wa Mkoa ili kuongeza upatikanaji wa chakula na kupunguza makali ya bei. Morogoro Mjini iligawiwa tani 100 za mahindi hayo.

Katika kutafuta mbegu za bei nafuu, Serikali iliomba msaada wa mbegu wa tani 3,200 kwa ajili ya kuzipatia kaya 302,026 zilizoathirika zaidi na upungufu wa chakula. Wahisani kupitia Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa walitoa tani 915.8 za mbegu. Mkoa wa Morogoro uligawiwa tani 84 za mbegu ambapo kati ya hizo tani 74 zilikuwa za mahindi na tani 10 za mtama. Tani 40 za mahindi na tani 10 za mtama ziligawiwa katika Wilaya za Mvomero na Morogoro Vijijini ambako wakulima wapatao 102,989 kutoka Morogoro Mjini hulima huko.

Aidha, tathmini ya uzalishaji wa chakula kwa msimu wa 2003/2004, ilibaini kwamba, Mkoa wa Morogoro kwa mwaka wa 2004/2005 utajitosheleza kwa chakula kwa kiwango cha asilimia 113. Hali hiyo, inatokana na uzalishaji wa tani 499,043 za chakula ikilinganishwa na mahitaji ya tani 440,981 za chakula kwa mwaka.

MHE. OSCAR T. MLOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, swali hili lina muda mrefu kidogo na niliuliza wakati tuna njaa na tulikuwa tunahitaji mbegu, lakini sasa najibowi wakati wa mavuno, hivi Serikali haioni kwamba haikunitendea haki katika hili? (*Makofî*)

(b) Mheshimiwa Spika, katika Kitabu cha Hotuba ya Wizara ya Kilimo na Chakula, ukurasa wa 14 amezungumzia kwamba Serikali inao mpango wa kununua tani 75,000 hadi 100,000 kwa ajili ya Hifadhi ya Taifa. Kwa nchi kama Tanzania ambayo ina watu takribani milioni 35, sawa sawa na kugawana punje mbili mbili hapa. Hivi kweli Serikali haina mkakati madhubuti wenyewe sura ya ukweli wa baa la njaa inapoweza ikatokea katika nchi yetu? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, swali hili liliulizwa muda mrefu wa nyuma, lakini kutokana na utaratibu wa kupanga maswali kujibiwa Bungeni na kwa bahati mbaya mimi sina mamlaka moja kwa moja, nasikitika hakupata jibu mapema. Laiti lingekuwa mapema, tungelitoa kwa wakati husika, sahamani sana.

Kuhusu mpango wa kununua tani 75,000 mpaka 100,000 ni kiasi kama kugawana punje mbili mbili, hapana naomba nimtoe wasiwasi huo Mheshimiwa Mbunge mwenzangu. Nafurahi kuwa yuko *concerned* sana na masuala ya njaa, nashukuru. Lakini hiki kiasi ambacho tunaongezea kiasi kile kilichopo albaki ya msimu huu iko mle ndani. Hii ni nyongeza kuwa na lundo kubwa zaidi la masuala haya. Kwa hiyo, namwondoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kuhusu suala hili. (*Makofî/Kicheko*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nina swali dogo kama ifuatavyo: Kwa kuwa mara nyingi nafuatilia majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, kwa kuwa kilimo ni sekta kiongozi katika nchi hii, wanalinganisha mwaka wa fedha wa 2002/2003 sawa sawa na mwaka wa kilimo kutoka Januari mpaka Desemba, hivi hii ni Wizara ni Wizara ya Kilimo na Chakula au Wizara ya Kilimo na Chakula cha Kununua? (*Makofî/Kicheko*)

SPIKA: Ni Wizara ya Kilimo na Chakula. Huna haja ya kujibu hilo tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. (*Kicheko*)

Na. 190

Ruzuku kwa ajili ya Shughuli za Maji - Mpwapwa

MHE. GEORGE M. LUBELEJE atauliza:-

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na utaratibu wa kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa Sh. 1,500,000/= kwa mwezi kama ruzuku kusaidia shughuli za uendeshaji katika Idara ya Maji, Wilaya ya Mpwapwa:-

(a) Je, kwa nini Serikali imesita kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa fedha hizo za ruzuku kuanzia mwezi Agosti, 2000 hadi sasa?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuipatia Halmashauri hiyo fedha ambazo hazikutolewa kuanzia Agosti, 2000 hadi sasa?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba iwapo itatoa fedha za ruzuku kwa Hamashauri hiyo, zitasaidia sana Idara ya Maji kwenye Wilaya hiyo kwa kulipia gharama za umeme na kununua dawa ya kusafisha maji?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu uliokuwa ukitumika katika kuendesha miradi ya maji katika Makao Makuu ya Wilaya nchini katika kipindi cha mwaka 2000/2001 ni ule wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa kukusanya fedha kutokana na mauzo ya maji kwenye miji husika na kisha kuzituma kwenye Halmashauri za Wilaya ili huduma ziweze kuendelezwa kama ilivyopangwa. Utaratibu huo ndio uliotumika pia kwa Mkoo wa Dodoma, ambapo maduhuli yaliyokusanywa na Ofisi ya Mkoo wa Mkoo yalirejeshwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, kwa ajili ya kutoa huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa. Sambamba na marejesho hayo kutoka Mkoani, Serikali ilikuwa pia ikitoa ruzuku kwa ajili ya matumizi mengine kama vile umeme.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali mbaya ya kifedha, Serikali ilishindwa kutoa ruzuku ya shilingi 1,500,000/= kuanzia 1999/2000 hadi 2001/2002 na badala yake uendeshaji wa mradi ulitegemea maduhuli ya shilingi 300,000/= yaliyokusanywa na Mkoo kila mwezi.

Kwa kuzingatia taratibu za matumizi ya fedha za Serikali, haitawezekana kwa sasa kuipatia Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa, ruzuku ambayo haikutolewa mwaka 2000/2001 kwa ajili ya kulipia umeme na madawa ya kusafishia maji.

Mheshimiwa Spika, tofauti na utaratibu wa zamani, huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa hivi sasa inatolewa na Mamlaka ya Majisafi iliyoundwa mwezi Julai, 2003 kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato na utendaji kwa ujumla na hivyo kuboresha huduma ya maji mjini hapo. Chini ya usimamizi wa Bodi ya Mamlaka hiyo, hivi sasa Mamlaka inakusanya wastani wa Sh. 2,500,000/= kwa mwezi ikilinganishwa na Sh. 300,000/= kwa mwezi kwa mwaka ambao Mheshimiwa Mbunge ameutaja. Aidha, mamlaka imeweza kukusanya madeni kiasi cha Sh. 9,256,000/= kati ya Sh.14,612,025/= iliyokuwa inadai wateja wake tangu mwaka 2000/2001. Makusanyo yanayotokana na mauzo ya maji yanakidhi gharama za uendeshaji kwa sehemu kubwa ukiondoa gharama za umeme.

Gharama za umeme zitaendelea kulipwa na Serikali kama ruzuku hadi hapo mamlaka itakapoweza kujitegemea na kwa kutekeleza hili, Serikali imekwishalipia madeni yote ya umeme ya Mji wa Mpwapwa hadi mwezi Desemba, 2003. Ni matumaini

yangu kwamba, fedha zinazokusanywa zitatumika kwa ajili ya kugharamia upanuzi, uendeshaji na uendelezaji wa huduma kwenye Mji huo wa Mpwapwa.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Serikali ina mpango mzuri sana wa kuboresha huduma ya maji katika Mji wa Mpwapwa pamoja na vitongoji vyake kama vile Enhawe. Je, mpango huo utaanza lini?

(b) Kwa kuwa Benki ya Dunia kwa kushirikiana na Serikali ya CCM imefanya kazi nzuri ya kuwachimbia visima wananchi wa Vijiji vya Sazima, Belege, Chaludewa na Chipogolo na kwa kuwa hadi sasa bado *pump* hazijafungwa na wananchi bado hawajaanza kupata huduma ya maji. Je, ni lini *pump* hizo za maji zitafungwa katika vijiji hivyo? Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimkumbushe Mheshimiwa George Lubeleje kwamba, Mpwapwa iko katika mradi wa maji wa Benki ya Dunia na vijiji alivyovitaja ni mojawapo ya vijiji ambavyo vinanufaika na mradi huo. Sasa kwa vile mradi huo ulianza mwaka 2003, nina hakika kwamba mpaka kumalizika programu nzima, maeneo mengi sana yatakuwa yameshughulikiwa ikihusisha ununuzi wa *pump* kwenye vijiji au kwenye skimu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja. Lakini pia ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuwa, kwa sababu *facility* bado ipo, waangalie maeneo ambayo yanaweza kusaidia *ku-supply* maji kwa Mji wa Mpwapwa ili kuipa nguvu mamlaka iliyopo iweze kuhudumia wananchi vizuri zaidi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Uongozi wa Wilaya, wajaribu kuangalia utaratibu huo. Kwa vile maduhuli wanayokusanya sasa hivi yanatosha kuendeleza huo mradi, nina hakika kwamba *supply* ya maji kwenye Mji wa Mpwapwa itaendelea kutengemaa.

MHE. FROF. DAIMON M. MWAGA: Mheshimiwa Spika, je, Naibu Waziri anafahamu kwamba Idara nyingine kama Idara ya Afya, Kilimo, zinapata *OC* moja kwa moja kutoka Serikalini na kilichokuwa kikiombwa hapa ni *OC* kutoka Wizarani kwa ajili ya Idara ya Maji, je, kuna tatizo la kutoa *OC*? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, nina hakika Mheshimiwa Mbunge anaelewa utaratibu wa *OC* ambayo inaombwa, ambayo inajumlisha mishahara na shughuli nyingine, inatakiwa itokane kwanza na mapato ya Halmashauri yenewe na pili inapatikana kutoka ruzuku ya Serikali ambayo inapitia Hazina na kupelekwa moja kwa moja. Kwa hiyo, kama *OC* ndiyo tatizo, mimi sioni kama kuna tatizo lingine lolote lile kwa vile Wilaya ya Mpwapwa ni sawa na Wilaya nyingine, wanapata *OC* kwa matumizi ambayo yameainishwa na Serikali kupitia ruzuku inayotolewa na Hazina.

Sasa kwa vipi tutofautiane sisi na Wizara ya Afya na sehemu nyingine, inategemeana na muundo, lakini ninavyofahamu sisi hatu-*manage* shughuli zilizo kwenye Halmashauri moja kwa moja. Tunachofanya tunatoa sera na *support* na tunajaribu kutafuta misaada kwa niaba ya nchi nzima kutoka nchi za nje. Kwa hiyo, kwa sasa hivi utaratibu huo ndiyo unaotumika, unaweza kutusaidia kwenda mbele kama kila Halmashauri watafanya kama inavyotakiwa.

Na. 191

Mradi wa Maji ya Chankorongo

MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. KABUZI F. RWILOMBA)
aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekubali kufufua Miradi ya Maji ya Chankorongo, Chigunga, Nyakagomba na Nyansembe.

(a) Je, Serikali haioni kuwa ni vyema ikahakikisha kwamba maji hayo yanapelekwa hadi Gereza la Butundwe na Miji ya Nyamigota na Katoro ambako kuna wakazi wengi sana na hakuna Maji?

(b) Kwa kuwa mwaka 2002/2003 Serikali ililiambia Bunge kwamba uchunguzi uliofanyiwa ulibainisha kwamba maji ya visima kwa Kanda ya Ziwa siyo salama kutokana na kuwepo kwa madini ardhini, je, Serikali imefanya jitihada gani za kuwapatia maji yanayofaa wananchi wa Geita ili kuokoa maisha yao?

(c) Je, ni dalili zipi mbaya za kiafya zimeshaanza kujitokeza kwa watu wanaotumia maji ya visima katika maeneo ya Mikoa ya Mwanza na Shinyanga, hususan katika Jimbo la Busanda, ambako kuna shughuli za madini karibu kwenye kila Kata?

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwiomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Serikali imekubali kufufua Mradi wa Maji wa Chankorongo (*Nyakagomba Group Water Supply*), uliobuniwa mwaka 1973 kwa lengo la kuvipatia maji vijiji 11 vya Nyakagomba, Chigunga, Bukondo, Nyanchiluluma, Butundwe, Nyansembe, Chankorongo, Chikobe, Chemamba, Nyakaswa, Kabuguzo na Hospitali ya Butundwe. Bomba kuu la kusukuma maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya mradi huu lina kipenyo cha inchi sita na urefu wa kilometra saba na ni la plastiki (*PVC*), kwa sehemu kubwa ambapo sehemu ndogo tu ya bomba hilo ndiyo ya chuma. Kutokana na udogo wa kipenyo cha bomba hilo kuu, haitakuwa rahisi kupanua mradi huu ili kupeleka maji hayo hadi Gereza la Butundwe, lililoko umbali wa kilometra 20 kutokea Hospitali ya Butundwe ambapo mradi huo umeishia ama katika Vijiji vya Nyamigota na Katoro, ambavyo navyo

vipo mbali zaidi kutoka Hospitali ya Butundwe. Kufanya hivyo kutasababisha upungufu mkubwa wa huduma hiyo na inawezekana kabisa hata sehemu ambazo wanatakiwa kupata maji hawatayapata.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa baadhi ya maeneo katika ukanda wa Ziwa Victoria hayana vyanzo vizuri vya maji chini ya ardhi kutokana na maji kutokuwa na ubora wa kuridhisha. Hata hivyo, yapo maeneo mengi katika ukanda huo, yanayonufaika kwa kutumia maji chini ya ardhi. Kwa mfano, kati ya mwaka 2002 na 2004, jumla ya visima virefu 25 na visima vifupi 225, vilichimbwa katika Wilaya ya Geita na kuwa na maji yenye ubora wa kuridhisha. Aidha, Mji wa Geita unanufaika na huduma ya maji kutokana na visima 11 vilivyochimbwa katika maeneo ya mji huo. Kutokana na kupanuka kwa Mji wa Geita, chanzo cha uhakika na cha kudumu cha maji kwa ajili ya mji huo kutoka Ziwa Victoria ndiyo ingeweza kuwa suluhisho sahihi.

Hivyo, Serikali imetoa jumla ya Sh. 5.0 milioni kwa ajili ya kupima na kusanifu mradi huo katika kipimo cha mwaka 2003/2004 na kwa mwaka 2004/2005 kiasi cha shilingi milioni 5 kitatengwa ili kukamilisha kazi ya upimaji na usanifu wa mradi.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa, maji yanayosambazwa kwa wananchi ni safi na salama kwa afya za watumiaji. Hadi sasa Wizara yangu haijapata taarifa yoyote kuhusu dalili mbaya za kiafya kujitokeza katika maeneo ya Mikoa ya Mwanza na Shinyanga likiwemo Jimbo la Busanda kutokana na matumizi ya maji ya visima, licha ya kuwepo kwa shughuli nyingi za uchimbaji madini katika maeneo hayo.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, katika jibu lake la msingi amesema kwamba Mji wa Geita una visima 11 tu na hivyo havitoshelezi kabisa kwa wakazi wa mji huo na amesema kwamba wametenga shilingi milioni tano, kwa ajili ya kufanya utafiti ili kuuletea Mji wa Geita maji safi.

Je, ni lini Mji wa Geita watauletea maji safi kutoka katika Ziwa Victoria? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama nilivyoeleza, Mji wa Geita ukilinganisha na upatikanaji wa maji wa sasa, hayatoshelezi. Lakini vile vile ni kweli kwamba, bado usanifu (*design*) ya mradi wa kuchukua maji kutoka *Lake Victoria* inafanyika.

Kwa hiyo, napenda nitoe shukrani sana kwa Mheshimiwa Mbunge, kwa jitihada wanazofanya kwa vile Mamlaka ya Maji ya Mji Mdogo wa Geita mwaka 2003 kwa kutumia fedha zao wao wenyewe, waliweza kujenga tanki la kuweka maji, ambalo limekuwa ni kichocheo kizuri sana kwa ajili ya kuongeza *supply* ya maji kwa ajili ya Mji wa Geita. Lakini hapo tutakapopata ripoti ya taarifa ya *design* ya mradi ndiyo pale tutaanza kuangalia uwezekano wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuupatia Mji wa Geita maji kutoka Ziwa Victoria. (*Makofî*)

Wananchi kuchukua Sheria Mkononi

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya hotuba za kila mwezi za Mheshimiwa Rais alizotoa mwaka 2002, amekemea vikali tabia ya wananchi ya kujichukulia sheria mikononi mwao kwa kuwapiga na mara nyingi kuwaua wahalifu; na kwa kuwa kila mara baada ya mauaji ya aina hiyo, Jeshi la Polisi limeendelea kuwakumbatia wananchi wanaofanya mauaji ya aina hiyo kwa kusema wananchi wenyе hasira wamemuua mhalifu huyo:-

(a) Je, Serikali inaelewa kuwa hao wauaji wengi wao siyo wananchi wenyе hasira bali ni wahalifu wengine na vijana wasio na ajira na waliokata tamaa na wengine wanachukua tu mazoezi ya kuua?

(b) Kwa kuwapamba wauaji hao kwa lugha ya wananchi wenyе hasira, je Serikali haioni kwamba inawapa kiburi tu na inakwenda kinyume na wito wa Rais wa kuwataka wananchi kutochukua sheria mikononi mwao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haina taarifa kwamba, wanaoendeleza tabia ya kuwapiga na kuwaua wahalifu ni vijana wasio na ajira au watu wanaochukua mazoezi ya kuua. Serikali imachofahamu ni kuwa, baadhi ya wananchi Mijini na Vijijini, baada ya kukerwa na tabia ya uhalifu, pale wanapomkamata mwizi, hushikwa na ghadhhabu kubwa na hujichukulia hatua za kumpiga na hata kumuua. Serikali kwa upande wake haliridhishwi na vitendo vya wananchi kuwaua watuhumiwa pasipo kuwafikisha Mahakamani. Tabia hii imekuwa inakemewa mara kwa mara na Viongozi wa Serikali, pamoja na Mheshimiwa Rais. Aidha, Jeshi la Polisi mara nyingi limekuwa kimbilio la watuhumiwa wanaosulubiwa na wananchi wenyе hasira na kwa kweli mara nyingi Polisi wamewaokoa watuhumiwa hao wasiuawe.

Napenda kutumia fursa hii, kwa mara nyingine tena, kukemea tabia hii ambayo inaweza kuleta madhara makubwa ya kiusalama katika jamii yetu. Vile vile, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge, tusaidiane na Serikali kuwaelimisha wananchi katika majimbo yetu kwamba, wakimkamata mhalifu wampeleke katika vyombo vya sheria na sio kujichukulia sheria mikononi mwao. (*Makofi*)

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo hayana utafiti, ningependa niulize maswali mawili ya nyongenza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa bado Serikali haijafanya utafiti kuhakikisha kweli wanaoua ni wananchi wenye hasira na sio vijana wasiokuwa na ajira na waliokata tamaa hasa hawa wezi wadogo wadogo ambaio sio majambazi. Je, Serikali itakubali sasa kufanya utafiti kuweza kujua ni matatizo gani hasa yanayosababisha wananchi hawa kuua na kwamba wala sio hasira?

Pili, kwa kuwa mimi nimeshuhudia mwenyewe sio mara moja au mbili, hawa vijana wakiwaua wenzao ambaio wamekwapua vitu vidogo vidogo kutoka kwa wapita njia na Askari wakiwa wanaangalia pembedi. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuwachukulia hatua Askari ambaio hawawazuii watu kuua watu kinyume cha sheria? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, sio kweli kwamba, Serikali haijafanya utafiti suala hili. Ukweli ni kwamba, ni tabia ya binadamu tu, watu wote waliosomea *sociology* wanajua kabisa, hata Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga mwenyewe anajua kabisa kama simu yake ya Sh.500,000/= akiporwa pale Ilala, aliyempora ile simu baada ya hatua mbili akikamatwa yeye mwenyewe atakuwa wa kwanza kumpiga teke. Ni hulka ya binadamu. Simwombe yampate, lakini ukweli ni kwamba, binadamu akichokozwa, akiwa *provoked*, alivyoumbwa ana tabia ya kuhamaki. Hii ndiyo sayansi yenye ya tabia ya binadamu. (*Kicheko/Makofî*)

Kusema ukweli Polisi wamekuwa wanafanya kazi nzuri sana kuokoa vijana wanaosulubiwa. Ningependa Polisi waendelee na kazi hiyo na wenyewe vibaka, hawa wanaofanya mambo haya wanajua kabisa kwamba wanaposulubiwa mahali pa kukimbilia ni Polisi. Hiyo wanajua wazi kabisa na Polisi wamekuwa wanafanya kazi nzuri ya kuokoa. Lakini jambo kubwa kabisa, hili jambo sio la Polisi ni letu wote, raia wote tusaidiane kuelimishana na raia wetu kwamba mhalifu apelekwe katika chombo cha sheria na sio kuanza kumhukumu kule kule alikokamatiwa. (*Makofî*)

Na.193

Sheria ya *Traffic*

MHE. EDSON M. HALINGA (k.n.y. MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA) aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeona umuhimu wa kutazama upya Sheria ya *Traffic* ili iende na wakati huu kwa vyombo vyaya usafiri barabarani kama magari, pikipiki na hata baiskeli na kwa kuwa upo ushahidi wa kutosha wa kuonesha kuwa ulevi wa waendesha vyombo hivyo unachangia kwa kiwango kikubwa idadi ya ajali za barabarani:-

(a) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba katika sheria hiyo, matumizi ya pombe yapigwe marufuku kwa wahusika wanapokuwa wakiendesha vyombo hivyo?

(b) Je, Serikali itaanzisha utaratibu wa kutoa leseni za Daraja C kwa madereva waliopata mafunzo katika Vyuo vinavyotambuliwa na kuweka pia kiwango cha elimu?

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mbunge wa Kwela, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa ulevi wa waendesha vyombo vya usafiri kama magari, pikipiki na hata baiskeli huchangia kusababisha ajali za barabarani. Kwa kutambua hali hiyo, katika Sheria ya Usalama Barabarani Na.30 ya mwaka 1973, kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.4 ya mwaka 1996, ulevi umepigwa marufuku kwa madereva wanapokuwa wanaendesha magari.

Aidha, kwa mujibu wa sheria hiyo hiyo, Serikali imeweka utaratibu wa kupata leseni Daraja C. Kwa mujibu wa sheria hiyo mwombaji wa leseni ya Daraja C ni lazima awe amepata leseni ya Daraja la chini kisha apate mafunzo maalum ya udereva wa magari makubwa na ya abiria katika Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali. Masharti mengine ni kwamba, mwombaji wa hiyo Daraja C anatakiwa awe ana umri usiopungua miaka 21 na uzoefu wa udereva katika leseni ya chini kwa muda usiopungua miaka mitatu.

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na kwamba Semina au mafunzo yanafanyika kwa madereva, lakini Mheshimiwa Waziri anajua kuwa mikokoteni ni usafiri unaosababisha ajali sana? Je, wana mpango gani wa kuendesha Semina hizo? (*Kicheko/Makofi*)

La pili, Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kufahamu kwamba usalama uko katika barabara kuu tu, lakini ukienda Mjini humo kwenye *streets* uendeshaji hauna sheria? Je, yuko tayari kufuutilia hali hiyo ili uendeshaji wa *streets* hizi Mijini uwe salama? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza Mheshimiwa Edson Halinga kuhusu waendesha mikokoteni hawa nao vile vile ni watumiaji wa barabara na sote tunabanwa na sheria zile zile za usalama barabarani na Jeshi la Polisi kuititia Kitengo cha *Traffic* wanavyo vipindi vya usalama barabarani ambavyo vinatoka kila wiki. Ningewashauri watumiaji wa barabara wote, waendesha mikokoteni, baiskeli na watembeao kwa miguu, wawe na tabia ya kusikiliza vile vipindi kwa sababu iko elimu ya kuwasaidia kuijokoa na ajali kwa kufuata sheria. Lakini vile vile kila mwaka katika kila Mkoa huwa tuna wiki ya kuelimishana, Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani, kila mwaka tunafanya na mwaka huu kila Mkoa tutafanya mwezi Septemba na Kitaifa tutafanya kule Songea na Mwenyekiti wa Kamati ya Mkoa wa Songea, Mheshimiwa Jenista Mhagama pale anawakaribisheni. Kwa hiyo, katika wiki ile vile tunatumia nafasi elimu kama hii kwa watumiaji wa barabara wote. (*Makofi*)

Swali la pili kuhusu kwamba Sheria za Barabarani zinatumika tu kwenye *highway*, katika barabara nyingine hakuna sheria, ukweli ni kwamba, sheria za barabarani zinatumika mahali popote, iwe ni barabara kuu, ziwe ni barabara za Mkoa, barabara za Wilaya mpaka barabara za Vijijini. Cha muhimu ni kwamba, sote tuzingatie zile sheria, tuijelimishe na zile Sheria za Barabarani kwa sababu popote pale utakapovunja sheria hata kama ni barabara ya mitaani ya Vijijini, bado utakamatwa kwa mujibu wa sheria.

Na.194

Tatizo la Mashamba Yenye Lease Babati

MHE. DAMAS P. NAKEI aliuliza:-

Kwa kuwa moja kati ya kero za wananchi wa Wilaya ya Babati ni suala zima la ardhi/mashamba yenye *lease* yaliyomegewa baadhi ya wanavijiji/wakulima; na kwa kuwa baadhi ya wanavijiji wanakabiliwa na tishio la kuondolewa kwa nguvu kwenye maeneo hayo licha ya kwamba wamejjengwa katika maeneo hayo hususan yale ya Singu/Arri kwa karibu miaka 20 sasa:-

- (a) Je, Serikali inatoa ufanuzi gani kutokana na utata uliopo kwenye mashamba ya Endasago, Singu na Dohom?
- (b) Je, Serikali iko tayari kufanya zoezi la kuwamegea ardhi baadhi ya wanavijiji wa Kata ya Arri ambao tayari wamekwishayaendeleza maeneo ya ardhi/mashamba hayo kwa takriban miaka 20?

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Pascal Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilikwishashughulikia utata uliokuwepo kati ya Wamiliki wa Mashamba ya Endasagu, Singu na Dohom katika Wilaya ya Babati na wanavijiji wanaozunguka mashamba hayo kwa utaratibu ufuatao:-

Kwanza, Shamba la Endasangu lililokuwa na ukubwa wa ekari 1,321 lilimegewa mwaka 1999 kwa idhini ya mmiliki wa shamba hilo ambaye kwa sasa ni Ndugu Suleiman Mchinji na kuwagawia wananchi wa Kijiji cha Arri eneo la ardhi lenye ukubwa wa ekari 215.39. Ni dhahiri kuwa wananchi wanaopakana na shamba hilo walishirikishwa katika zoezi zima la umegaji wa eneo hilo.

Pili, Shamba la *Singu Estate* lililokuwa na ukubwa wa ekari 5,564 lilimegwa mwaka 1983 kwa idhini ya mmiliki wa shamba hilo, ambaye kwa sasa ni *Tanzania Breweries Company Ltd.* na kuwagawia wananchi wa Vijiji vya Sigino na Arri eneo la ardhi lenye ukubwa wa ekari, 2,451.

Tatu, Shamba la Dohom lenye *Land Office Number 3122* lililokuwa na ukubwa wa ekari 2,114 lilimegwa mwaka 1999 kwa idhini ya Chama cha Ushirika cha *Rift Valley Cooperative Union (RIVACO)*, ambacho kwa sasa kinamiliki shamba hilo. Katika umegaji huo, jumla ya ekari 100 ziligawiwa kwa wanavijiji.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na mgawanyo wa mashamba nilioueleza hapo juu, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hususan Halmashauri ya Wilaya ya Babati, hivi sasa inashughulikia taratibu za kuwamilikisha rasmi wananchi waliogawiwa maeneo hayo. Hivyo, napenda kuwatoa wasiwasi wananchi waliogawiwa ardhi kihalali kutoka kwenye mashamba hayo kuwa hawataondolewa kwa nguvu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali za kumega sehemu ya mashamba yaliyotajwa na kuwagawia wananchi katika maeneo yanayozunguka mashamba hayo, bado kuna uhaba wa ardhi kwa wanavijiji. Hivyo, wananchi wanaendelea kuvamia ndani ya mashamba hayo kwa ajili ya kilimo na makazi.

Kutokana na uhaba wa ardhi katika maeneo hayo, Serikali kwa mara nyingine iko tayari kuwamegea ardhi baadhi ya wanavijiji wa Kata ya Arri kulingana na mapendekezo yatakayowasilishwa Wizarani kwangu na Wilaya kwa kushirikiana na Mkoa baada ya kufanya tathmini ya mahitaji halisi ya ardhi kwa wananchi wake kwa kushirikiana na wamiliki wa mashamba hayo. Kwa sasa Wizara yangu haijapokea mapendekezo ya kubadilisha hatimiliki za mashamba hayo kwa lengo la kuwagawia wananchi. Katika zoezi kama hili, suala la kulipa fidia lazima lizingatiwe.

Aidha, napenda kutoa wito kwa wananchi wenye matatizo makubwa kabisa ya ardhi wafikirie uwezekano wa kuhamia maeneo yenyе ardhi ya kutosha hapa nchini. Pia nazishauri Halmashauri za Wilaya kwa Kushirikiana na Mikoa yenyе mashamba makubwa yaliyotelekezwa, wawasilishe mapendekezo ya kubatilisha hatimiliki zilizohai Wizarani kwangu ili ardhi hiyo irejeshwe na wagawiwe wananchi wa maeneo husika kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizopo.

MHE. DAMAS P. NAKEI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa bado kuna upungufu mkubwa wa ardhi katika maeneo hayo hasa sehemu za Dohom na Arri, je, Serikali inaweza kuwagawia wananchi wa Dohom mashamba ya *RIVACO* ambayo yamegeuka mapori hayaendelezwi ili yaweze kusaidia wananchi hawa ambao wana upungufu mkubwa wa ardhi? (*Makofi*)

(b) Pamoja na kuwa Serikali imeahidi kwamba wananchi wa maeneo yanayozunguka mashamba ya Singu hawatahamishwa kwa nguvu au kwa lazima; je, Serikali inaweza kutoa maagizo kwa mwekezaji ambaye sasa hivi tayari anatishia kuwaondoa hao wananchi ambao wamezunguka maeneo hayo ili wananchi ambao wamejijenga pale kwa miaka 20 sasa wasiendelee kuishi kwa wasiwasi kwa sababu tayari wameshajijenga kiuchumi kwa kuwa hawana mahali pengine pa kwenda?

SPIKA: Aah, sasa mbona unatoa hotuba? Swali limeshaelewaka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:
Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba taratibu zifuatwe. Hatukatai kwamba mashamba makubwa ambayo hayaendelezwi wasipewe wananchi, lakini kwa utaratibu, pamoja na kwamba Serikali imesema kwamba itagawa, lakini haiwezi kugawa Wizarani isipokuwa kutokana na huko mlipokuwa na matatizo mnakwenda katika Serikali za Viji, kuna Serikali za Kata, Tarafa, Wilaya mpaka Mkao. Mnashirikiana katika mazungumzo na mwenye maeneo hayo, baadaye mapendelekezo yakitolewa, basi ndipo yanaletwa Wizarani ili muweze kugawiwa. Lakini Wizara haiwezi kugawa moja kwa moja mashamba haya kutoka Wizarani mpaka kwenye eneo hilo.

La pili kusema kwamba watu wamevamia wakaondolewe, narudia tena kwamba, uvamizi ni kitendo cha jinai. Hakuna haki pamoja na kwamba hakuna mahali pa kukaa lakini sio halali kwenda kuvamia shamba la mwenzako bila utaratibu. Kwa hiyo, wafuate taratibu na sheria zilizopo ili waweze kulipata kwa uhalali. La sivyo, hatutaki vurugu zifanyike katika maeneo mnayoishi. Ardhi ni mali ya Serikali lakini alipewa mtu kuimiliki. Sasa anapoimiliki, basi kama ni kunyang'anywa, anyang'anywe kwa utaratibu wa kutumia sheria zile ambazo zilimpa ardhi hiyo. (*Makofî*)

Na.195

Kivuko - Musoma na Mji wa Kinesi

MHE. IBRAHIMU W. MARWA aliuliza:-

Kwa kuwa kwenye miaka ya hamsini na mwanzoni mwa miaka ya sitini kulikuwepo na kivuko kilichokuwa kikihudumia Miji ya Musoma na Kinesi; na kwa kuwa umuhimu wa kuwa na kivuko hicho sasa ni mkubwa zaidi kwani kitasaidia kufungua uchumi, kuondoa kero ya usafiri wa abiria na mizigo/shehena zao na kwamba utafiti umeonesha umuhimu wa kuwepo kwa kivuko hicho:-

(a) Je, kivuko ambacho kinaweza kutosheleza mahitaji ya usafiri wa abiria, mizigo na magari machache kinaweza kugharimu kiasi gani cha fedha?

(b) Je, Serikali iko tayari kulipokea ombi la wananchi wa Musoma na Kinesi kupatiwa huduma hiyo muhimu katika mwaka wa Fedha wa 2004/2005?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kivuko cha Kinesi kilichokuwa kinamilikiwa na mtu binafsi, kilisitisha kutoa huduma ya kuvusha abiria na mizigo kati ya Mji wa Kinesi na Mji wa Musoma mwaka 1967. Kusimama kwa kivuko hicho kulitokana na sababu mbalimbali ikiwemo kivuko hicho kuendeshwa kwa hasara kwa wakati huo.

Baada ya maelezo haya, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ibrahimu Wankanga Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kivuko ambacho kinaweza kutosheleza mahitaji ya usafiri wa abiria, mizigo na magari machache na chenye uwezo wa kubeba tani 50 kinaweza kugharimu kiasi cha Shilingi za Kitanzania bilioni 1.5.

(b) Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa fedha, Serikali haikutenga fedha kwa mwaka 2004/2005 kwa ajili ya ununuzi wa kivuko hicho?

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kwa mwaka huu wa fedha wa 2004/2005, kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali haikutenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa kivuko hicho; nilikuwa napenda kuuliza, je, kama nilivyouliza katika swali la kwanza kipengele cha pili, Serikali inapokea ombi la kuweza kupatiwa kivuko hicho?

Pili, kama ombi hilo linapokelewa, je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha hizo kwenye bajeti itakayofuata ya mwaka 2005/2006? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, vivuko vinavyohitajika kuhudumiwa na Wizara ya Ujenzi vyote tunavifahamu na hiki ni kimojawapo. Ndiyo maana tumesema kwa mwaka huu tumeshindwa kupangia fedha, lakini tunakijua umuhimu wake na kipo katika *list* ya Wizara ya Ujenzi kwamba ni kivuko kimojawapo ambacho tukipata pesa tutanunua kivuko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kupanga fedha mwaka 2005/2006, inategemea na bajeti ya wakati huo, siwezi kuahidi hivi sasa.

Na.196

Elimu ya Juu ya Ugonjwa wa Mabusha na Matende

MHE. DR. AISHA O. KIGODA (k.n.y. MHE. SALOME J. MBATIA) aliuliza:-

Kwa kuwa wakati akitoa elimu kwa Wabunge, Dr. Kisanga wa Hospitali ya Taifa Muhibili mwezi Julai, 2003 kuhusu mabusha, matende na hususan akiongea kuhusu kansa na tezi ya uume alisema, mbali na mambo mengine, wan'anume wanaoanza ngono mapema na wenyewe wapenzi wengi hupata tatizo hilo ambalo dalili zake ni mkojo kutoka wenyewe au kutomalizika kwenye kibofu na hivyo kusababisha mtu kwenda haja ndogo mara kwa mara, tatizo ambalo kama halikufanyiwa kazi mapema, mauti humfika muathirika:-

(a) Kama hii ni kweli ni kwa nini Serikali haitoi elimu hii kwa vijana kupitia programu mbalimbali yakiwemo mashule ili vijana watambue na kuelewa na hivyo kuepuka ngono za mapema na holela ili kuepuka janga hilo la uzeeni?

(b) Kwa kuwa ni kweli hatujasikia elimu hii ikitolewa na vijana kwa jumla kuhamashisha tukiwemo vijana wa zamani, Serikali inaliahidhi nini Bunge na Taifa hili?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swal la Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) naomba nitoe maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa matende na ngiri maji unaenezwala mbu wa aina ya *culex*. Ugonjwa wa tezi ya uume, yaani *Prostate Hypertrophy*, hutokana na mabadiliko ya chembechembe za kawaida na kuwa tezi au hata kuwa *cancer* kwa kadri ya umri wa mwanaume unavyoongezeka. Chanzo hakijulikani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, sasa napenda kujibu swal la Mheshimiwa Salome Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia vitengo vyake mbalimbali vya Elimu ya Afya kwa Umma, pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, yamekuwa yakitoa elimu mashulen, makazini na kupitia Vyombo vya Habari yani redio, magazeti na runinga, kuhusu athari mbalimbali yakiwemo magonjwa ya zinaa na Ukimwi, ambazo wanazipata vijana kutokana na kuanza tendo la ngono mapema.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali pamoja na Taasisi mbalimbali zitaendelea kutoa elimu mashulen, vyuoni, maofisini na sehemu nyinginezo zenye mikusanyiko ili kuweza kuwaepusha vijana pamoja na vijana wa zamani, juu ya athari zitokanazo na kuanza ngono mapema na hasa ngozo zisizo salama.

MHE. DR. AISHA O. KIGODA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize kama ifuatavyo: -

Kwanza, kwa vile moja ya dalili za wale wenye mabusha na matezi ya kokwa za kiume mojawapo ni kushindwa kukojoa au kukojoa kidogo kidogo, je, wale watu wa kawaida watatofautishaje kwamba hii ni ngiri maji au ni mabusha na lile tatizo ambalo linasababishwa na kuziba kwa njia ya mkojo kwa sababu ya uambukizo?

Pili, kwa vile tatizo la mabusha huwa linaweza kuwapata pia akina mama, naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atupatie taarifa kwamba ni kweli kwamba akina mama wanaweza kupata mabusha na kama wanapata ni kanda gani ambayo inaathirika zaidi? Ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, swalí la kwanza sio sahihi kwamba mabusha na ile *prostate hypertrophy* zina dalili zinazofanana. Mabusha hayahusiani na kuziba kwa njia ya mkojo. Hii ni *hydroseal* ambayo iko sehemu tofauti kabisa. Isipokuwa ile *prostate* au tezi ya uume ndiyo ikiwa imekuwa sana hupelekea kuziba kwa njia ya mkojo kwa hiyo, dalili zake ni tofauti kabisa.

Kuhusu swalí la pili kwamba, je, mabusha huweza kuwapata akina mama? Lazima niseme kwamba, hili ni swalí ambalo pengine ninaweza nikapata jibu la utaalamu zaidi baadaye, lakini kwa ninavyojuu mimi *hydroseal* haiwpati akina mama. (*Makofi/Kicheko*)

Na.197

Hospitali ya Mwalimu Nyerere DDH

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Mwalimu Nyerere *DDH* ni muhimu sana katika kutoa huduma ya matibabu katika Jimbo la Serengeti na kwa kuwa sasa inakabiliwa na ukosefu wa Madaktari Bingwa hasa wale wa fani ya watoto na akina mama wajawazito:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia hospitali hiyo Madaktari wa fani nilizozitaja?

(b) Je, Serikali imeipatia Hospitali hiyo Madaktari Bingwa wangapi kuanzia mwaka 1997 - 2004?

(c) Je, Serikali imepandisha Vyeo wafanyakazi wangapi katika Hospitali hiyo tangu mwaka 1997 - 2004 na ina mpango gani wa kuwapandisha vyeo wafanyakazi waliobaki?

NAIBU WAZIRI WA AFYA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalí la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti, Mugumu *DDH*, ambayo sasa inaitwa Mwalimu Nyerere, inayomilikiwa na Kanisa la *Menonite*, iliteuliwa kuwa Hospitali ya Wilaya mwaka 1976. Kwa mujibu wa Mkataba tuliowekeana baina ya Serikali na Kanisa la *Menonite* ni jukumu la Serikali kutaoa fedha zote za uendeshaji (*Recurrent Expenditure*), ikiwa ni pamoja na mishahara ya watumishi wote waliopo na Kanisa la *Menonite* Tanzania litagharamia miundombinu na *Capital Expenditure*.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina mpango wa kuipatia Madaktari Bingwa Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti kwa kuwa kada hiyo kwa sasa haipo katika Hospitali za Wilaya kwani huwekwa kwenye Hospitali za Mikoa na za Rufaa tu. Endapo Kanisa linaweza kupata Madaktari Bingwa kutoka mahali pengine, Wizara yangu haina pingamizi ya wao kufanya hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu hapo awali, kwa sasa Madaktari Bingwa huwekwa katika Hospitali za Mikoa na Rufaa tu. Kwa mantiki hiyo, Wizara yangu haikupeleka Madaktari Bingwa wowote kati ya mwaka 1997 - 2004.

(c) Mheshimiwa Spika, watumishi wa Hospitali Teule ya Wilaya ya Serengeti hupandishwa vyeo na Wizara ya Afya kama inavyofanyika kwa watumishi wengine wa Hospitali za Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kati ya mwaka 1997 - 2004, Wizara yangu iliwapandisha vyeo watumishi 87. Hivi sasa Wizara ya Afya inapitia mapendekezo ya majina 157 ya watumishi wa Hospitali hii waliopendekezwa kupandishwa vyeo.

MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na vile vile namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Lakini nina maswali mawili.

(a) Kwa kuwa nilitembelea Hospitali hivi karibuni nikakuta kuna kero nyingi, wafanyakazi wengi hawajapandishwa vyeo, pili, hata *allowances* zao hazijalipwa, tatu, mishahara yao tulioongeza tangu Julai, 2003 mpaka leo walikuwa hawajalipwa, je, ni lini Waziri atakwenda kutembelea hiyo Hospitali na kuangalia hizo kero ili ziweze kutatuliwa?

(b) Ni lini nyongeza ya mishahara ya wafanyakazi hawa za mwaka 2003 zitalipwa kwa sababu mwaka tayari umekwisha na wenyewe hawajalipwa? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali kuhusu suala la vyeo, ni kwamba, kuna majina 157 ambayo sasa hivi yanashughulikiwa. Endapo kutakuwa na majina mengine zaidi ya haya ambayo wanastahili kupandishwa vyeo, basi nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, anifikishie ili yaweze kushughulikiwa.

Kuhusu *allowances* na nyongeza za mishahara, ningeomba Mheshimiwa Mbunge kupitia Halmshauri yake, atuletee taarifa rasmi ya jambo hili ili tuweze kuona ni posho zipi zinazozungumziwa na uhalali wa nyongeza za mishahara ambazo ni watumishi gani wanaohusika na tutalifanya kazi mara moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kutembelea Hospitali hii, napenda tu niseme kwamba, nitakuwa tayari kufanya hivyo. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa na muda wa maswali umekwisha. Kuna tangazo la Kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Sophia Simba, anaomba Wajumbe wake wakutane leo tarehe 6 Julai, 2004, saa tano asubuhi katika Ukumbi Na.227 ghorofa ya pili.

Baada ya hapo, kwa kuwa kuna Waheshimiwa Wabunge, kadhaa wamechukua karatasi za ruksa kwenda kwenye Saba Saba, basi napenda kuwalishwa kwamba, tuna ugeni mkubwa utakuja hapa Bungeni siku ya Jumatatu tarehe 12 Julai, 2004. Tumearifiwa kwamba, Rais wa Namibia, Mheshimiwa Sam Nujoma, atakuwa Tanzania mwishoni mwa wiki hii na katika shughuli atakazofanya ni pamoja na kuja Dodoma kulihutubia Bunge. Kwa hiyo, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge, waliochukua ruksa za usafiri, wajitahidi ili tuwepo hapa Bungeni siku ya Jumatatu kumpokea Mgeni wetu, Mheshimiwa Rais Nujoma. (*Makofi*)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutohakana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais - Ikulu (Fungu 20 na 30), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33) na Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa kazi kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu, likubali kuptisha Makadirio ya Fedha ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kwa ushirikiano na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha Bungeni hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumshukuru na kumtakia afya njema, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, ambaye licha ya kuwa na matatizo ya kiafya katika kipindi hiki, bado ameweza kuendelea kusimamia na kutekeleza shughuli za Chama, Serikali na Taifa, kwa dhati na bila kutetereka. Tunaomba Mwenyezi Mungu, aendelee kumjalia afya njema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kukubali ombi la Uingereza kuwa mmoja wa Makamishna katika Kamisheni ya Afrika iliyoundwa na Waziri Mkuu wa Uingereza kwa kuandaa na kukamilisha ripoti kuhusu *a Fair Globalization, Creating Opportunities for All*, iliyofadhiliwa na *World Commission on the Social Dimension of Globalization*. Hiki ni kielelezo cha kutambulika kwa hekima, busara na mchango wa Rais wetu katika masuala ya nchi na Kimataifa. Jukumu la Kamisheni ya Afrika ni kutathmini vikwazo ambavyo vimekuwa vikiathiri maendeleo katika bara hili na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuondokana na athari hizi. Aidha, ripoti hiyo imeainisha athari za utandawazi kuhusu uchumi wa dunia, hasa katika nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa hotuba yake yenye upeo mpana ambayo imetoa dira ya utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2004/2005. Pia, nawapongeza Mheshimiwa Basil Pesambilii Mramba, Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba zao ambazo zimebainisha misingi, sera, malengo na mwelekeo wa bajeti na uchumi wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2004/2005. Ninapenda vile vile kutumia nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri waliotangulia kwa hotuba zao ambazo zimeonyesha mchango wa Wizara zao katika kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, naomba kumpongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Bunge la Afrika mwaka huu. Uteuzi huu umetuthibitishia Watanzania kuwa tunao viongozi wenye uwezo mkubwa kushika nyadhifa za Kitaifa na Kimataifa. Aidha, napenda pia kuwapongeza Mheshimiwa Dr. William F. Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani W.A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani Zanzibar na Mheshimiwa Athumanji Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchaguliwa kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Mhambwe, kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. Pia, naomba kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge la *SADC (SADC Parliamentary Forum)*. Aidha, napenda kumpongeza pia Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Elimu wa Bara la Afrika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kikipongeza Chama cha Mapinduzi na mgombea wake, Mheshimiwa Danhi B. Makanga, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, kwa kupata ushindi ambao ni kielelezo tosha cha ushindi mwingine wa CCM katika chaguzi zetu zijazo, hususan Uchaguzi Mkuu mwakani (2005). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, natoa pole kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Yete Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, ambaye alifariki ghafla wakati akihudhuria Vikao vya Bunge hapa Dodoma. Naomba Mungu aiweke roho yake marehemu mahala pema peponi, *amen*.

Aidha, napenda pia kutumia fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kufiwa na baba yao mzazi tarehe 7 Juni, 2004. Vile vile naomba kuwapa pole Waheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Estherina Kilasi na Mheshimiwa Charles Makongoro kwa matatizo yaliyowapata.

Mheshimiwa Spika, hotuba ninayoitoa inahusu Ofisi ya Rais ambayo inajumuisha Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma. Nitaanza maelezo yangu kwa kutoa majukumu na mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa fedha wa 2003/2004 na baadaye nitaezeza mpango wetu kwa mwaka huu wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Utumishi wa Umma ni nguzo ya Taifa lolote duniani. Watumishi wa Umma wanatoa mchango mkubwa katika kulinda na kujenga heshima ya nchi, kudumisha usalama, amani na utulivu na kuiwezesha Serikali kutekeleza shughuli zake ipasavyo. Hivyo, daima utumishi wa umma lazima uwe hatua moja mbele ili kuhakikisha kuna utawala bora, ufanisi, uwajibikaji na utoaji huduma nzuri. Huu ndio msingi wa mpango wa Serikali wa kuboresha utumishi wa umma kwa kuweka mifumo na kanuni nzuri pamoja ili kuwa na utendaji kazi mzuri na uwajibikaji katika Wizara na Idara zote. Lengo ni kuufanya utumishi wa Umma nchini Tanzania kuwa chombo chenye kutukuka kitakachoiwezesha Tanzania kuwa na uchumi unaondelea kukua na endelevu, wenye kuleta matumaini na unaoweza kutokomeza umaskini katika karne hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi tulizopanga kuzifanya katika mwaka wa fedha 2003/2004, kulingana na mpangilio wa mafungu yanayohusika kama ambavyo nimeyaelezea hapa juu yaani, Ofisi ya Rais - Ikulu, Utumishi, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Rais ndiye Mkuu wa Nchi hivyo ndiye ana dhamana ya kusimamia uendeshaji wa Serikali yote kwa ujumla. Ofisi yake ina jukumu la kusimamia utawala bora, pia ina Taasisi mbili chini yake, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund - TASAF*). Katika mwaka wa 2003/2004, Ofisi ya Rais iliendelea kusimamia utekelezaji wa maamuzi yaliyotolewa

na Rais pamoja na Baraza la Mawaziri. Aidha, Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake, iliendelea kutekeleza kazi zake kama ifuatavyo, nitaanza na Utawala Bora:-

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa ya Utawala Bora ni kuratibu, kusimamia na kupima utekelezaji wa programu ya kujenga utawala unaozingatia sheria na haki na hasa kuhakikisha kwamba Mkakati wa Taifa wa kupambana na rushwa unatekelezwa ipasavyo. Katika mwaka 2003/2004 maafisa wasimamizi (*Focal Persons*) wa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, walipewa mafunzo ya kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kupambana na rushwa katika maeneo yao. Aidha, iliandaliwa warsha kwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambao pia ni Wajumbe wa Mtandao wa Wabunge wa Afrika walioko katika mapambano dhidi ya rushwa (*African Parliamentary Network Against Corruption - APNAC - TANZANIA CHAPTER*) ili kuwashirikisha na kuwawezesha nao waandae na kutekeleza programu zao za kupambana na rushwa. Ili kuiweshera Serikali kuufikia umma kwa haraka zaidi, semina iliendeshwa kwa wamiliki wa vyombo vya habari na wahariri wa magazeti kuhusu mpango wa Serikali wa kupambana na rushwa kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuanzisha *investigative journalism* nchini.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya ukarabati, ambayo inahusu ujenzi wa nyumba ya mapokezi pamoja na kuweka vifaa na zana za kisasa jengo la polisi na sehemu za kuegesha magari, inategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, vita dhidi ya rushwa inahitaji mifumo ya kiuchumi inayolenga kupata huduma bila kutoa au kuomba rushwa. Pia, wananchi wote kuwa na tabia ya uadilifu na silaha kubwa ya kujenga mifumo ya aina hii ni kubadili taratibu za utendaji kazi ili kujenga uwazi na uwanjibikaji na elimu kwa umma kwa maendeleo yanayoletwa kwa kufanya kazi kwa bidii, juhudhi na maarifa. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2003/2004, TAKURU imetekeliza shughuli zake na kupata mafanikio yafuatayo:-

- Kesi 202 za tuhuma za rushwa ziliendeshwa mahakamani, na kati ya hizo kesi 66 zimeweza kutolewa maamuzi, kesi 15 watuhumiwa wamefungwa, kesi 25 watuhumiwa waliachiwa huru, kesi 6 ziliondolewa mahakamani na kesi 20 Serikali imekata rufaa. Aidha, kiasi cha shilingi milioni 557 ziliokolewa kutohana na hatua zilizochukuliwa na TAKURU mara baada ya kupokea taarifa ya hujuma hizo. Pia majalada 20 yamewasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (*DPP*) kwa ajili ya kupata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani;
- Upanuzi wa huduma kwa kufungua ofisi katika wilaya zote Tanzania Bara isipokuwa Wilaya za Namtumbo, Kilolo, Ruangwa, Uyui, Nkasi na Kilindi ambazo inategemewa zitafunguliwa mapema iwezekanavyo;
- Kuendesha mafunzo kwa wachunguzi 35 na mafunzo maalum kwa ajili ya waendesha mashitaka 40 ili kuwaongezea uwezo katika uchunguzi, uongozi, upeo na kuendesha mashtaka;

- Uendeshaji wa tafiti katika maeneo yafuatayo: Kwenye viwanda vya sukari kutathmini madhara ya sukari kwa wajawazito na watoto, Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi - MMEM, kuangalia usimamizi na utekelezaji wake, Halmashauri, kufuutilia uteuzi wa Wakurugenzi, Chuo Kikuu cha Mzumbe kuhusiana na sifa za baadhi ya wahadhiri na Dar-es-Salaam, kufuutilia mfumo wa utoaji leseni za biashara kwa wawekezaji nchini;
- Kushiriki maonyesho mbali mbali kwa nia ya kuleta mwamko kwa wananchi ili washiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya rushwa; na
- Kuchapisha kalenda 30,000, vipeperushi 50,000 na majarida 88,000 yanayoelezea ujumbe wa mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, tuliedelea kutekeleza programu maalum kuhusu elimu ya kuzuia rushwa kwa walimu ili kuwawezesha kufundisha elimu hiyo mashulenii.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), ilianzishwa kama mradi shirikishi wa kujenga uwezo wa wananchi kujitegemea na kama mkakati wa kuondoa umaskini. Matokeo mazuri ya utekelezaji katika wilaya 48 za awamu ya kwanza yamewezesha mradi huo kuenezwa katika wilaya zote katika awamu ya pili itakayoanza hivi karibuni. Katika mwaka wa 2003/2004, *TASAF* ilitekeleza miradi mbalimbali katika wilaya hizo kama ifuatavyo:-

- Mafunzo yalitolewa kwa wasimamizi na watekelezaji 22,230 wa mradi;
- Miradi 1,337 ilitekelezwa kupitia Miradi ya Jamii na baadhi yake imeanza kutoa huduma muhimu kwa jamii;
- Miradi 34 inaendelea kutekelezwa kupitia Mpango wa Makundi Maalum, kama vile yatima, wazee, wajane, walemavu na waathirika wa IKIMWI;
- Miradi 305 ilitekelezwa kupitia Miradi ya Ujenzi na baadhi yake imeanza kutoa huduma muhimu kwa jamii;
- Walengwa zaidi ya 102,106 walifikiwa kupitia miradi ya kuinusuru jamii; na
- Uendelezaji wa taasisi pamoja na mifumo ya huduma za uendeshaji, kujenga uwezo wa wadau na ununuzi wa bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004 kama ifuatavyo:-

- Maslahi ya watumishi yameendelea kuboreshwa mwaka hadi mwaka. Bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia 201.14 kutoka shilingi 154.1 bilioni mwaka 1995/96 hadi shilingi 464.06 bilioni mwaka 2003/2004. Kima cha chini cha mshahara

kimeongezeka kwa asilimia 214.3 kutoka shilingi 17,500 hadi shilingi 55,000 katika kipindi hicho. Muundo wa mishahara umeboreshwa, hatua ambayo pia imehusu malipo ya pensheni kwa wastaafu. Serikali pia inaendelea kutekeleza Sera ya Muda wa Kati ya Malipo ya Mishahara ya mwaka 1999. Miundo mipyä ya utumishi imetekelizwa na viwango vya mishahara vimepandishwa kwa watumishi wote. Kwa mfano, kuanzia mwaka 2000 hadi 2003 kima cha chini cha mshahara kimeongezeka kwa asilimia 34 kutoka Shillingi 41,000 hadi Shillingi 55,000 kwa mwezi. Aidha, mshahara wa ngazi za kati umeongezeka kwa wastani wa asilimia 50.6 kutoka wastani wa Shillingi 158,815 hadi Shillingi 239,115 kwa mwezi. Kwa wastani mishahara ya watumishi wa Serikali imeongezeka kwa asilimia 57 kati ya mwaka 2000 hadi 2003.

- Tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja wa ofisi yangu umefanyika na kuonesha sehemu tulizofanikiwa na zile ambazo bado tunahitaji kuboresha zaidi utendaji kazi. Pamoja nyingine kama zilivyoonyeshwa katika ukurasa wa 12 hadi ukurasa wa 20 wa hotuba yetu.
- Serikali imeendelea kuboresha ajira na uteuzi wa wanawake katika nafasi za uongozi Serikalini. Mwaka 2003/2004 jumla ya wanawake 63 waliteuliwa kushika nafasi za uongozi. Kutokana na uteuzi huu idadi ya wanawake walio na nyadhifa za Katibu Mkuu iliongezeka na kufikia asilimia 28, Makatibu Tawala wa Mikoa asilimia 29, Makatibu Tawala wa Wilaya asilimia 16 na Wakurugenzi wa Halmashauri asilimia 26. Tangu mwaka 2000 zaidi ya wanawake 500 wamepatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwaongezea sifa na uwezo, hatua ambayo itaiwezesha Serikali kuwateua kushika nafasi mbalimbali za uongozi.
- Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 uliendelea kwa kukamilisha uteuzi wa Wajumbe wa Tume, kukamilisha na kuidhinisha matumizi ya Kanuni za Utumishi wa Umma na Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma za mwaka 2003 na kutoa Waraka wa Utumishi wa Umma Na.I wa mwaka 2004 unaoelekeza utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma. Aidha, Waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 2004 kuhusu utekelezaji wa Miundo ya Utumishi ultolewa.
- Idara moja imebadilishwa kuwa Wakala wa Serikali wa Mamlaka ya Chakula na Dawa. Aidha, Idara saba ambazo ni Idara ya Utafiti wa Kijiolojia, Misitu na Nyuki, Umeme na Ufundu, Makumbusho na Mambo ya Kale, Kitengo cha Uzalishaji Mbegu, Chuo cha Usalama wa Anga na Kabidhi Wasii Mkuu ziko katika hatua mbali mbali za kubadilishwa kuwa Wakala wa Serikali.
- Majukumu na Miundo ya Wizara mbili na Idara Zinazojitegemea tatu imehuishwa ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mahakama, Tume ya Pamoja ya Fedha na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (*TACAIDS*). Aidha, Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali mbali mbali zilipewa ushauri kuhusu majukumu na miundo yao ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi za Serikali.
- Vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano vimeanzishwa katika wizara kumi. Vitengo kama hivi vitaanzishwa katika wizara zote zilizosalia kufuatia Agizo la

Mheshimiwa Rais linalokusudia kuhakikisha kwamba, wananchi wanaeleweshwa kuhusu majukumu na utendaji wa Serikali.

- Mfumo wa kuboresha utendaji kazi (*Performance Management System*) katika Utumishi wa Umma umeanzishwa katika Wizara zote na Idara Zinazojitegemea tisa, ambazo zimekamilisha taratibu zote kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao kulingana na mipango ya kimkakati (*Strategic Plans*) kuanzia 2004/2005.
- Ukaguzi wa kumbukumbu na malipo ya mishahara kwa waajiri 11 ulifanyika. Katika ukaguzi huo kumejitokeza upungufu kadhaa wa kiutendaji na ofisi yangu imeagiza waajiri kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu dhidi ya watendaji waliohusika.
- Mafunzo maalum yaliendeshwa juu ya utayarishaji wa makadirio ya Ikama na mishahara ya watumishi kulingana na mipango ya mikakati (*Strategic Plans*). Kwa mwaka wa fedha 2003/2004, washiriki 359 walihudhuria mafunzo hayo toka Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Matokeo yake yameanza kuonekana kwa maafisa husika kuandaa ikama na bajeti za mishahara.
- Elimu ya maadili kupitia vyombo vya habari, redio, *TV* na magazeti imetolewa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2004 mada 52 zilitangazwa na Redio Tanzania, Dar es Salam na *Radio Free Africa* na pia kutolewa katika magazeti kama makala. Kuanzia katikati ya mwaka 2001 hadi mwezi Mei 2004, jumla ya mada 197 zilitangazwa na redio hizo.
- Vitabu vidogo vinne vinavyohusu maadili katika utumishi wa umma na uboreshaji wa utendaji kazi Serikalini, vilitayarishwa. Nakala 10,000 za vitabu hivyo zilichapishwa na kusambazwa sehemu mbali mbali nchini.
- Kanuni za Maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa umma zilihuishwa na Kanuni mpya kutayarishwa.
- Malalamiko ya wananchi kupitia vyombo vya habari au yaliyotumwa na walalamikaji moja kwa moja Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma yalifuatiliwa kwa kuwasiliana na Wizara, Idara au Mikoa husika ili kupata ukweli wa tuhuma dhidi ya walalamikiwa. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili, 2004 jumla ya malalamiko 143 yalipokelewa na kufuatiliwa kama ilivyoelezwa hapa juu na kati ya malalamiko hayo 61 yalijibowi. Katika kipindi cha miaka mtano kuanzia mwaka 2000 malalamiko 1,073 yalipokelewa na 340 kujibowi na Taasisi husika. Aidha, ofisi yangu inaendelea kuyashughulikia malalamiko 733 ikiwa ni pamoja na kuyaelekeza katika Taasisi nyingine za Serikali ili yashughulikiwe ipasavyo.
- Kutoa mwongozo na mikakati sahihi ya mafunzo kwa waajiri katika matumizi bora ya Rasilimaliwateru.

- Kuhuisha Waraka wa Ajira ya Wataalamu wa Kigeni ili kuweka utaratibu mzuri wa kupata wataalam hao ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wataalam wazalendo.
- Kukamilisha uhuishaji wa Waraka wa Utumishi Na.9 wa 1992 unaohusu utaratibu wa kuajiri na kutumia vizuri wataalam wazalendo ndani na nje ya Utumishi wa Umma.
- Kuwezesha kubadilishwa kwa kilichokuwa Chuo cha Utumishi wa Serikali kuwa Wakala wa Serikali. Chuo hiki sasa kinaitwa Chuo cha Utumishi wa Umma na kinashughulika na mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa utumishi wa umma.
- Kuendelea kuimarisha Chuo cha Utumishi wa Umma kwa upanuzi wa majengo, kuajiri waalimu wenyе sifa zinazohitajika na kuwaendeleza waliopo na kununua zana za kazi za kisasa na kuboresha maslahi ya watumishi wa chuo ili kuongeza ufanisi.
- Kuwezesha kubadilishwa kwa kilichokuwa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo Mzumbe, kuwa Chuo Kikuu cha Mzumbe.
- Kutumia Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani (*Tanzania Global Development Learning Center*), kuboresha taaluma ya viongozi. Kituo kimekuwa na ongezeko la kozi na midahalo ya uongozi, uchumi, afya na jinsia tangu mwaka 2000 kilipoanzishwa, ambayo iliwashirikisha wataalam na viongozi wapatao 2,816 kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano.
- Kuwapa mafunzo Mawaziri, Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya kuhusu *ICT literacy*.
- Kupitishwa kwa Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu Serikali ya elektroni (*e-government*).
- Kufanya maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Nyaraka na Kumbukumbu tuli.
- Kuandaa miswada na rasimu za marekebisho ya Sheria mbalimbali kama ifuatavyo:-
- Sheria ya Majadiliano ya Pamoja: Sheria hii inaanzisha utaratibu mpya wa ushirkishwaji wa watumishi wa Umma, kuitia vyama vyao vya wafanyakazi, katika kupanga na kufikia uamuzi kuhusu maslahi yao. Ushirikishwaji wa wafanyakazi katika mambo yanayowagusa ni utekelezaji wa utawala bora na ni hatua nzuri ya kuleta maelewano, utulivu na mshikamano sehemu za kazi. Sheria hii tayari imeidhinishwa na imeanza kutumika kuanzia Julai 1, 2004.
- Marekebisho ya Sheria ya Mafao ya Viongozi Wakuu Wastaafu. Sheria husika zinafanyiwa marekebisho ili kwenda na wakati na kuboresha huduma kwa Viongozi Wakuu wa kitaifa wanapostaafu.

- Sheria ya Kuwaenzi Viongozi Waasisi wa Taifa la Tanzania. Mapendekezo ya marekebisho ya muswada yanaendelea kuboreshwa kwa kuzingatia maoni ya wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, katika kutekeleza kazi zilizopangwa mwaka 2003/2004, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilipata mafanikio yafuatayo:-

- Kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni kutoka kwa viongozi wa umma 1,989 kwa mujibu wa sheria.
- Kukamilisha uchunguzi wa malalamiko 61 kati ya 82 yaliyopokelewa, uchunguzi unaendelea kwa malalamiko 21 yaliyobaki.
- Kutoa mafunzo kwa viongozi kwa njia ya redio, magazeti, warsha na semina kuhusu umuhimu wa kuzingatia maadili ya viongozi wakiwemo Madiwani, Watendaji Wakuu wa Halmashauri, Wakurugenzi wa Utumishi na Utawala katika Wizara na Idara na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.
- Kufungua ofisi katika kanda tatu, Arusha, Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kuanzishwa kwa Tume ya Utumishi wa Umma ni matokeo ya utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Tume ya Utumishi wa Umma inajumuisha makundi yafuatayo: Utumishi wa Serikali Kuu, Utumishi wa Serikali za Mitaa, Utumishi wa Afya, Utumishi wa Ualimu, Utumishi wa Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji. Kazi kubwa ya Tume hii ni kuhakikisha masuala ya utumishi yanaendeshwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu pamoja na kuhakikisha kuwa ajira katika utumishi wa umma inazingatia sifa, uwezo na ushindani kwa madhumuni ya kufanikisha utendaji wenye malengo na matokeo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana niliwasilisha mbele ya Kamati yako bajeti ya iliyokuwa Tume ya Utumishi Serikalini, ambayo sasa ni kati ya Tume zilizofutwa na shughuli zake kuchukuliwa na Tume ya Utumishi wa Umma. Hivi sasa kazi kubwa ya Tume ya Utumishi wa Umma ni kukamilisha kazi zote ambazo hazikukamilishwa kabla ya Tume kuundwa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa mwaka wa fedha 2004/2005 katika mwaka wa fedha 2004/2005, Ofisi ya Rais, Ikulu itaendelea kufuatalia na kuratibu Utawala Bora na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Serikali. Aidha, Ofisi itaendelea kuchambua mambo mbalimbali ya kisera na Miswada ya Sheria kwa lengo la kumshauri Rais na Baraza la Mawaziri. Kazi nyingine zitakazofanywa ni kuendelea kuratibu utendaji kazi wa vyombo vya dola kuhusu usalama wa Taifa, kuimarisha masuala ya mawasiliano kwa Umma na kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali kwa wananchi. Vilevile, Ikulu itaendelea kuwapa mafunzo watumishi wake kwa ajili ya kuboresha utendaji wao wa kazi na kusimamia shughuli za uendeshaji wa ofisi.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha majukumu ya kupambana na rushwa nchini, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) itaendelea na utafiti kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa na kutoa mapendekezo ya namna ya kuiziba hasa katika maeneo yanayolalamikiwa sana. Aidha, Taasisi itaendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya haki zao, madhara ya rushwa na jinsi ya kupambana na kujiepusha na vitendo vya rushwa. Ili kuhakikisha elimu hii inawafikia wananchi wengi, njia zote za kutolea habari zitatumika ikiwa ni pamoja na redio, televisheni, magazeti na vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jukumu la kuzuia rushwa, katika mwaka wa 2004/2005, Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) itaendelea kupambana na tatizo la rushwa kwa kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- Kuchunguza majalada 2,715 ambayo hayakukamilika mwaka 2003/2004;
- Kukamilisha mipango ya kufungua ofisi katika Wilaya sita ambako TAKURU haina ofisi;
- Kuendesha kesi 156 ambazo ziko mahakamani na zingine zitakazofunguliwa; na
- Kujiardaa kikamilifu kufuatilia maandalizi na mwenendo wa Uchaguzi Mkuu wa 2005.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa awamu ya kwanza ya Mradi wa *TASAF* inaishia Desemba, 31 2004, *TASAF* itaendelea kushirikiana na wilaya katika kuzisaidia jamii ambazo bado hazijakamilisha utekelezaji wa miradi iliyopo ili ikamilike. Jumla ya miradi 492 ya jamii, 61 ya makundi maalum na 200 ya ujenzi inategemewa kukamilishwa katika kipindi kilichosalia.

Mheshimiwa Spika aidha, maandalizi ya awamu ya pili ya *TASAF* yameanza na yatakamilika mwezi Desemba, 2004, ambapo utekelezaji wake unategemewa kuanza rasmi Januari 1, 2005. Awamu hii italenga kuziwezesha jamii kupata na kutumia rasilimali za kijamii na kiuchumi zinazopatikana katika maeneo yao, kujenga uwezo wa mashirika yasiyo ya kiserikali, taasisi za kijamii, taasisi za kuweka fedha za kijamii, wasimamizi wa miradi na wananchi kwa ujumla, kusimamia maendeleo na kuboresha mahusiano yao na wadau wengine katika maendeleo, kutoa ajira za muda kwa kaya maskini na wakati huo huo kuboresha huduma za jamii, kuboresha maisha ya makundi maalum na wasiojiweza na kuwezesha jamii kupata mikopo, kuboresha uwekaji wa akiba na mitaji.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2004/2005, tutaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa kuboresha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma ulioanza mwaka 2000. Katika kipindi hiki tutaendelea na jitihada za kuwaelimisha wadau na umma wote kwa ujumla kuhusu utekelezaji wa mpango huu kwa njia mbalimbali, kama vile semina, warsha,

vipeperushi, vipindi nya redio na televisheni na kwenye maonyesho mbalimbali kama ya Saba Saba na Nane Nane.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya Mpango huu imelenga zaidi kufanikisha ubora wa utoaji huduma, uwezeshaji wa watendaji kwa kuwapa mafunzo na vitendea kazi na pia kuwajengea mazingira mazuri ya kazi, kushirikiana na sekta binafsi na wakala wa serikali katika kutoa huduma na kulipa mishahara inayovutia ili watumishi wa utumishi wa umma wasijihushe na vitendo vinavyokwenda kinyume na maadili mema ya kazi. Aidha, mpango huu kwa sasa unaainishwa na mipango mingine ya kuboresha sekta zingine za Umma kama vile Fedha, Sheria na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha kuwa mipango hii, kwa pamoja, inachangia katika juhudzi za kuboresha utoaji huduma na kuwaletea wananchi maisha mazuri zaidi kwa kuwapunguzia umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha 2004/2005, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaelekeza nguvu zake nyingi hususan katika utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002. Sheria hii inazingatia Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma (1998) kwa kuhimiza, pamoja na mambo mengine, utendaji kazi wenye matokeo (*results-oriented management*) na uwajibikaji wa waajiri na waajiri kwa upande mwengine.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga uwajibikaji katika Utumishi wa Umma, ofisi yangu, imeandaa utaratibu mpya wa kupima utendaji kazi wa watumishi wa umma. Ofisi yangu inaandaa utaratibu mpya wakupima utendaji kazi kwa watumishi wa umma. Utaratibu huu umeandaliiwa ili kurekebisha upungufu wa utaratibu wa zamani ambao upimaji wa ufanisi wa mtumishi ulifanywa kwa siri bila kumshirikisha anayepimwa. Katika zama hizi za uwazi na ukweli ni vizuri Utumishi wa Umma ukaendeshwa kwa uwazi na kwa kuzingatia malengo yanayopimika na yaliyokubaliwa kati ya mtumishi na msimamizi wake.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kuwa na wataalam wenye sifa na wenye kukidhi mahitaji, waajiri sasa wamepewa mamlaka na Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002, ya kusimamia masuala ya ajira, maendeleo ya watumishi na nidhamu. Lengo ni kuwa na watendaji bora wenye uwezo wa kutoa huduma za uhakika kwa wananchi. Kwa watumishi ambao wamepungukiwa na sifa kwa kuzingatia miundo mpya ya Utumishi wa Umma, juhudzi zitafanyika kuwaendeleza ili wawze kujipatia sifa zinazohitajika. Hivyo, watumishi wa aina hii wanatakiwa kutumia vizuri nafasi hiyo watakayopewa na waajiri wao kuhakikisha wanapata sifa zinazohitajika kuwafanya wawe wataalamu katika fani zao.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuhakikisha kuwa ajira na upandishwaji vyeo vinafanyika kwa haki na ushindani, utaratibu wa kutangaza nafasi za kazi kitaifa na kutoa muda wa kutosha kwa waombaji kuwasilisha maombi yao, kuweka vigezo vinavyooleweka na kupimika katika usaili, na utaratibu mzuri na wa wazi wa uteuzi wa washindi kwa nafasi husika vinasisitizwa sana ili kudhibiti ajira zenye mwelekeo wa kikabila, kindugu au kirafiki. Hili linafanyika kwa madhumuni ya kulinda umoja wa Taifa letu. Lengo la sheria mpya ya Utumishi wa Umma ni kukasimu madaraka kwa

waajiri, lakini bila kukwepa wajibu, na wakati huo huo kuhakikisha kuwa Utaifa unapewa kipaumbele katika kanuni na taratibu zetu za utendaji na uendeshaji wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, ni azma yetu kujenga Serikali inayoweza kutoa maamuzi sahihi kwa wakati muafaka ili kuwahudumia wananchi wake kwa usahihi na ukamilifu. Hivyo, katika mwaka huu wa fedha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imepanga kuanzisha ujenzi wa mtandao wa kiserikali wa mawasiliano ya huduma za simu pamoja na taarifa za kompyuta. Mtandao huu utapunguza ghamama za uendeshaji pamoja na kuongeza tija ya huduma zetu. Vile vile, tumepanga kuanzisha mifumo ya taarifa za maarifa (*Knowledge Management Systems*), kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa taarifa zinazohitajika kwa utoaji wa maamuzi katika sehemu zote za Serikali. Aidha, Ofisi ya Rais, Utumishi inatarajia kusambaza huduma za mfumo mpya wa usimamizi wa ajira na mishahara Serikalini, ili waajiri waweze kuwajibika kwa kusimamia kwa karibu mienendo yote ya taarifa za ajira na ulipaji wa mishahara kwa watumishi walio chini yao.

Mheshimiwa Spika, ili kuwepo na mpango timilifu na endelevu katika utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Taifa katika taasisi na asasi za Serikali, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaanza kuhuisha kumbukumbu za watumishi wa Serikali katika ngazi za wizara kwa kuzingiza katika mfumo wa kompyuta. Lengo la zoezi hili ni kuhakikisha kwamba kumbukumbu muhimu za kiutumishi zinakuwa mahali pamoja na hivyo kusaidia utoaji huduma kwa watumishi kwa kasi zaidi. Aidha, tutaendelea kushirikiana na programu ya Serikali za Mitaa kwa kuboresha masijala zake ili kusaidia upatikanaji wa taarifa mara zinapohitajika na hivyo kupunguza kwa kiasi kikubwa kero kwa wananchi. Pia tutaendelea na juhudzi za kuboresha masijala na kujenga uwezo wa watendaji wa masijala. Kadhalika, Ofisi yangu itaanza kukarabati nyaraka kongwe za Kijerumanzi zinazohifadhiwa katika Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa ili kuhakikisha kuwa urithi andishi wa taifa letu haupotei na ili kuhifadhi historia ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazoendelea za kuboresha utendaji kazi katika utumishi wa umma, lipo suala la kujenga uwezo wa kiutendaji wa taasisi na watumishi wa umma. Mfumo wa sasa wa demokrasia ya vyama vingi vyenye itikadi tofauti, kasi ya uvumbuzi wa teknolojia mpya inayopokelewa na kutumiwa katika nyanja zote za utendaji kazi, na kupanuka kwa uchumi wa soko vinahitaji kuendeshwa na kusimamiwa na watu wenye uwezo mkubwa wa kuelewa na kuamua. Hivyo, suala la kuendeleza na kuijenga raslimali-watu katika utumishi wa umma lina umuhimu wa pekee. Kutokana na kutambua umuhimu huu Ofisi ilitoa mwongozo kwa Wizara, Idara Zinazojitegemea na Mikoa na kuagiza kwamba waandae programu za mafunzo kwa watumishi wao na kuhakikisha kwamba kila mwaka wanatenga fedha katika bajeti zao kwa ajili ya kutekeleza programu hiyo. Tutaendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo haya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuhimiza mipango ya mafunzo kwa watumishi wa umma jitihada zinafanywa pia kuimarisha Chuo cha Utumishi wa Umma na Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani (*Tanzania Global Development Learning*

Center), ili kwa pamoja viwe na uwezo wa kutoa mafunzo ya ujuzi ya muda mfupi kwa watumishi kutoka Serikalini na taasisi mbali mbali. Aidha, katika mwaka huu wa fedha tutaendelea kukipatia Chuo cha Utumishi wa Umma walimu, vifaa na kukifanya ukarabati kwa lengo la kukipa hadhi ya kuweza kufanya tafiti ambazo matokeo yake yanaweza kuboresha na kukidhi mahitaji ya mafunzo hapa nchini kuliko kuendelea kutegemea vyuo vya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Tanzania cha Mafunzo ya Maendeleo Duniani, kilichoanzishwa Juni, 2000, ni moja ya vituo 10 vya kwanza duniani vinavyotumia teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya Setilaiti. Hadi sasa, vituo hivi vimeongezeka na kufikia 81 duniani, na hivyo kupanua uwezo wa Kituo chetu kufundisha wataalam wanaohitajika kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Kwa kupitia Kituo hiki, viongozi na wataalam mbalimbali wanayo nafasi ya pekee ya kushiriki kwenye midahalo ya kimataifa, mafunzo na kubadilishana mawazo na wataalam wengine walio nje ya nchi. Hatua zinachukuliwa ili kuongeza uwezo wa Kituo kuhudumia viongozi na wataalam wengi zaidi, na pia kupanua uwezo wa kuwafikia Watanzania wengine walio nje ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kuelimisha Umma, kwa njia mbalimbali, kuhusu maadili ya msingi katika utumishi wa Umma. Lengo ni kutumia Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake, Sera ya Menejimenti na Ajira Katika Utumishi wa Umma (1998) pamoja na Kanuni zingine husika katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na watumishi bora, waadilifu na wanaowajibika ipasavyo kwa Umma ikiwa ni moja ya njia muhimu ya kuimarisha utawala bora.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mikakati ya kujenga utawala bora kwa kuboresha maslahi ya watumishi wa umma, sambamba na juhudzi za kuboresha mfumo wa utendaji kazi chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma. Serikali inajitahidi kuboresha mishahara ya watumishi wote hasa wale walio katika ngazi za utealam na uongozi, ili iweze kuwavutia na kuwabakiza kwenye utumishi wa umma watumishi wenye sifa watakaoweza kuongeza tija.

Kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyotoa maelezo katika Bunge lako, Serikali imetenga jumla ya Shilingi 551.15 bilioni kwa mwaka wa fedha huu 2004/2005, kwa ajili ya kugharamia mishahara ya watumishi. Hili ni ongezeko la asilimia 18.7 ikilinganishwa na jumla ya Shilingi 464.061 bilioni zilizotengwa kwa mwaka 2003/2004. Nyongeza hii itasaidia kugharamia ajira mpya, upandishwaji vyeo kwa watumishi wenye utendaji wenye matokeo na marekebisho ya mishahara ya watumishi kwa kati ya asilimia 9 hadi asilimia 12.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua za makusudi zinazochukuliwa na Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Serikali ya Tanzania, pamoja na jitihada za ziada zinazochukuliwa na ofisi hii kujenga na kuendeleza uwezo wa wanawake kupata mafunzo zikiwepo warsha na semina mbalimbali za kuhamasisha masuala ya jinsia, katika mwaka 2004/2005 tutatoa mafunzo ya shahada ya

pili kwa wanawake 50 pamoja na mafunzo ya muda mfupi yanayolenga kuongeza uwezo na ujuzi wa kazi kwa wanawake 450.

Mheshimiwa Spika, haitakuwa vyema kusisitiza juu ya uboreshaji wa utumishi wa umma bila ya kuzungumzia tatizo la janga la UKIMWI ambalo linagusa kila sehemu ya utumishi wa umma. Kwa kutambua athari kubwa itokanayo na janga la UKIMWI, hasa tukizingatia kuwa UKIMWI, si tu unapunguza idadi ya watumishi, bali pia unaathiri watumishi wenye vipaji na uzoefu mkubwa, ofisi yangu inajumuika na wadau wengine kupanga na kutekeleza mikakati ya kupambana na janga hili. Tayari nimelieleza Bunge lako Tukufu kuwa tunao mpango wa kuhimiza utekelezaji wa maadili ya utumishi wa umma ambao yakizingatiwa yatawaepusha watumishi kwa kiasi kikubwa kuijingiza katika vitendo na tabia zinazoweza kuwasababishia maambukizi. Ofisi yangu katika mwaka huu wa fedha imepanga kuelimisha na kufanya utafiti juu ya athari za UKIMWI kwa utumishi wa umma ili kuwa na mikakati madhubuti ya kukabiliana na janga hilo ndani ya Utumishi wa Umma. Nichukue nafasi hii kwa mara nyingine kuwaasa watumishi wa umma kujiepusha na tabia na mienendo ya maisha inayohatarisha afya zao hasa kutokana na janga hili la UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma naomba sasa nitoe maelezo kuhusu mpango wa kazi wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka kipaumbele katika kutekeleza kazi zifuatazo:-

- Kufungua ofisi tatu za kanda katika Mikoa ya Tabora, Mwanza na Mtwara;
- Kuchunguza malalamiko kutoka kwa wananchi dhidi ya viongozi mbali mbali wanaotuhumiwa kukiuka maadili ya uongozi, pamoja na kukamilisha uchunguzi wa malalamiko 21 yaliyopokelewa mwaka 2003/2004;
- Kupokea na kuhakiki tamko la mali na madeni ya viongozi wa umma kwa mujibu wa sheria;
- Kutoa elimu ya maadili ya uongozi kwa umma na viongozi kwa njia ya redio, semina na machapisho mbali mbali; na
- Kukamilisha mradi wa kukuza maadili (*Ethics Promotion Project*), unaojumuisha mafunzo ya kitaalam kwa watumishi, ununuzi wa vifaa na uhamasishaji wa wananchi kuhusu maadili ya viongozi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maelezo juu ya mpango wa kazi wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2004/2005 ambao pia ni mwaka wake wa kwanza wa kazi tangu kuundwa. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Tume ya Utumishi wa Umma imejiwekea malengo yafuatayo:-

- Kukamilisha kazi zilizokuwa zitekelezwe na Tume zilizovunjwa ambazo hazikukamilika katika kipindi cha mwaka 2003/04;

- Kuandaa na kuhuisha miongozo ya ajira kwa misingi ya sifa;
- Kuandaa na kutoa miongozo, kufuatilia na kuhakikisha kuwa ajira katika Utumishi wa Umma inazingatia misingi ya sifa, uwazi na ushindani;
- Kuandaa taarifa za tathmini za utekelezaji wa miongozo, taratibu na kanuni zinazosimamia ajira kwa madhumuni ya kuhakikisha ajira hiyo inazingatia sifa na ushindani;
- Kuandaa taarifa za tathmini za utekelezaji wa mazoezi ya upandishaji vyeo yenye kuzingatia matokeo ya kazi na sio muda wa kukaa katika ngazi moja kama ilivyokuwa hapo awali;
- Kufuatilia, kukagua na kutathmini utekelezaji wa miongozo kuhusu taratibu za nidhamu na kiwango cha uwajibikaji miongoni mwa mamlaka za Ajira, Waajiri na Watendaji;
- Kupokea, kuchambua, kupendekeza, kuamua na kuwasiliana na wenyе rufaa kuhusu uamuzi wa Tume;
- Kuandaa mafunzo kwa watumishi wa Tume na wadau mbali mbali kwa madhumuni ya kuimarisha shughuli za Tume; na
- Kutoa elimu kwa umma kuhusu shughuli za Tume kuititia vyombo vyahabari.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa mwaka 2004/2005 unakusudiwa kuhakikisha kwamba, watumishi wote wa umma wanatendewa haki sawa, kwamba ajira katika utumishi wa umma unazingatia misingi ya ushindani, uwazi, usawa wa jinsia na uadilifu. Aidha, Tume itahakikisha kwamba utumishi wa umma unabadijika kuwa ule unaozingatia matokeo ya kazi ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu wa ukaguzi utakaohakikisha kuwa malengo ya Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma yanafikiwa na mamlaka zote za ajira.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais pamoja na Idara zilizo chini yake na ambazo zimejumuishwa katika hotuba hii, kwa pamoja, inalo jukumu maalum la kujenga Utumishi wa Umma madhubuti, wenyе uwezo wa kusimamia maendeleo ya Taifa hili kwa kuimarisha huduma kwa wananchi na kwa vyombo vingine vyahabari na kwa njia ya kusimamia utawala bora, wenyе haki na usawa na unaojenga mazingira yenye utulivu na amani.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieza Bunge lako Tukufu mwaka jana, Serikali madhubuti itatokana na utumishi wa umma unaoaminika, wenyе kuchukua hatua sahihi pale unapotakiwa kufanya hivyo, kutekeleza wajibu wake kitaalam na kwa moyo na kukumbuka kuwa wapo kazini kutokana na dhamana waliyopewa na wananchi. Sheria ya Utumishi wa Umma ya 2002 ambayo nimeizungumzia kwa kirefu katika hotuba hii inalenga kutusaidia kutekeleza dhamira hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali madhubuti na inayoendeshwa kwa misingi ya kisheria, haki na usawa ni nguzo ya msingi katika kuleta demokrasia ya kweli na utawala bora, maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wananchi. Pia, kazi zote ambazo zimekuwa zikitekelezwa na Ofisi hii na Taasisi zake zimelenga kwa njia moja au nyingine katika kujenga Serikali madhubuti yenye uwezo wa kusimamia maendeleo ya Taifa kujenga demokrasia na utawala bora unaolenga kukuza amani, utulivu na umoja wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mengi ambayo tunatarajia kuyatekeleza kwa mwaka huu wa fedha ni malengo ambayo yamo katika Programu ya Kuboresha Utendaji Kazi na Utoaji Huduma bora katika Utumishi wa Umma (*Public Service Reform Programme*).

Napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wote wa Kisiasa na Kiutendaji na hasa Waheshimiwa Wabunge, kwa kuilewa na kuipa msukumo maalum Programu hii na kwa ushirikiano wao mkubwa katika kueneza ujumbe wa Programu hii na hivyo kurahisisha utekekelezaji wa malengo yake kwa mapana ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa kiasi kikubwa yamechangiwa na misaada toka nchi rafiki na mashirika mbalimbali. Nachukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika yafuatayo: Uingereza, Uholanzi, Malaysia, India, Ujerumani, Australia, New Zealand, Singapore, Pakistan, Misri, Thailand, Uswisi, Italia, Korea ya Kusini, Benki ya Dunia, *NORAD*, *JICA*, *UNDP*, *UNIDO*, *DANIDA*, *CIDA*, *SIDA*, *USAID*, *ACBF*, Jumuiya ya Madola na Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia hotuba yangu, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa ushirikiano wake mkubwa katika kusimamia majukumu tuliyopewa na katika matayarisho ya hotuba hii. Aidha, ninapenda kuwashukuru Katibu Mkuu Kiongozi, Bwana Matern Y. C. Lumbanga, Katibu Mkuu (UTUMISHI), Bwana Joseph A. Rugumyamheto, Katibu Mkuu (IKULU), Bwana Abel W. R. Mwaisumo, Wenyeviti na Makatibu wa Tume na Taasisi mbalimbali na Watumishi wote walioko katika Wizara, Mikoa, Wilaya na Idara Zinazojitegemea, siyo tu, kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaotoa katika kufanikisha malengo ya Serikali katika sehemu zao za kazi, bali pia kwa mchango wao uliowezesha matayarisho ya hotuba hii ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi nilioutoa hapa juu, ambao umeonyesha hali ya utekelezaji wa shughuli zilizofanywa na Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma mwaka 2003/2004, pamoja na mpango wa kazi kwa mwaka 2004/2005, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee maombi yetu ya fedha, ambayo yanafikia jumla ya Sh.144,971,790,000/= kwa ajili ya kugharamia mpango wa kazi kwa mwaka 2004/2005 kwa mgawanyo ufuatao:-

(a) Ofisi ya Rais - IKULU:

Fungu 20	-	Sh. 4,163,392,200/=
Fungu 30	-	Sh. 92,729,703,900/=

- (b) Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma:
Fungu 32 - Sh. 40,994,091,200/=
- (c) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma:
Fungu 33 - Sh. 690,735,000/=
- (d) Tume ya Utumishi wa Umma:
Fungu 94 - Sh. 6,393,867,700/=

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninapenda kukushukuru tena wewe Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Wachangiaji wanne wa mwanzo kwenye hoja hii ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Bernard Membe na Mheshimiwa Halimensi Mayonga, wanne wa mwazo, hapo sasa! (*Kicheko*)

Sasa namwita Msemaji wa Kamati iliyochangwa hoja hii, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE (k.n.y. MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA): Mheshimiwa Spika, naomba nitoe mbele ya Bunge lako Tukufu, maoni kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2003/2004 na mapendekezo ya makadirio ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005 kwa Ofisi ya Rais, Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba tena nichukue fursa hii, nimpongezeMheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kwa mara nyingine kuwa Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki. Kuchaguliwa kwake tena ni kutokana na imani kubwa walijonayo Wananchi wa Bariadi Mashariki, kwake yeye binafsi na kwa Chama cha Mapinduzi (CCM). (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yetet Mwalyego, aliyefariki ghafla hapa Dodoma wakati analiwakilisha Jimbo lake la Mbeya Vijijini, tarehe 24 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, yameelezwa katika Kanuni za Bunge Na. 93(2), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 87(2) na 93(1), Wajumbe wa Kamati hiyo ni wafuatao:-

Mheshimiwa Athuman Janguo, Mwenyekiti, Mheshimiwa George Lubeleje, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Chifu Abdallah Fundikira, Mheshimiwa Profesa Jumanne Abdallah Maghembe, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Grace Kiwel, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Juma Suleiman N'hunga, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ramadhan Khalfan, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa George Mlawa, Mheshimiwa Pascal Degera na Mheshimiwa Nimrod Mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Kamati hii ilitoa maagizo yafuatayo kwa lengo la kuboresha utendaji wa kazi Serikalini na katika taasisi zake:-

(a) Kuhusu ajira ya wataalam wa kada ya afya, Kamati iliagiza kwamba, utaratibu uliotumika kuajiri Walimu pia utumike katika ajira ya watumishi wa kada ya afya hasa katika Halmashauri za Wilaya.

(b) Kuhusu ajira katika Halmashauri, Kamati iliagiza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, isimamie kwa karibu ajira katika Halmashauri ili zisifanyike kwa upendeleo, jambo ambalo linaweza kuteteresa umoja wa nchi yetu.

(c) Kuhusu muda wa utendaji kazi Serikalini kutozingatiwa, Kamati iliagiza Serikali ifanye utafiti ili kubainisha kwa nini watumishi wa umma hufanya kazi kwa saa chache sana. Wakati umefika tujue kiini cha tatizo hili, tutolee maelezo na tupate mbinu za kukabiliana nalo.

(d) Kuhusu vita dhidi ya rushwa, Kamati ilibaini kwamba, vita dhidi ya rushwa inashindikana kwa kuwa kesi nyingi za rushwa zinafungwa kutokana na kukosa ushahidi. Kamati ilitaka kujua hatua zilizochukuliwa kukabiliana na suala hili.

(e) Kuhusu mishahara ya Walimu, Kamati iliagiza Serikali kuwa mishahara ya Walimu iboreshwe ili kuondoa uwezekano wa wao kukimbilia sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imeridhishwa na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kutekeleza maagizo yaliyotolewa na Kamati yangu. (*Makofi*)

Hata hivyo, baadhi ya maagizo yanahitaji muda mrefu ili yaweze kutekelezeka na pia yanahitaji jamii nzima iijuhishe katika utekelezaji wake kwa mfano, vita dhidi ya rushwa. Aidha, Kamati inashauri kuwa mbinu mbalimbali zikiwemo za kisayansi zibuniwe ili kupambana na rushwa katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, chini ya Ofisi ya Rais, Kamati ilipitia mafungu yafuatayo: Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Fungu 30 - Ikulu, Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Fungu 94 - Tume ya Utumishiwa Umma.

Mheshimiwa Spika, chini ya Fungu Na.20 na Fungu Na.30, Kamati ilielezwa kuwa ukarabati wa jengo la Ikulu unaendelea baada ya kusimama kwa muda. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa ingawa fedha zote zilizokasimiwa kwa ajili ya kazi hiyo kwa mwaka 2003/2004, zilikuwa zimetolewa ifikapo Juni, 2003. Fedha hizo zitakuwa na upungufu wa Sh.800 milioni, ambazo zilitumika kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*). Kwa hali hiyo, fedha hizo hazitamaliza kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2004/2005 imetoa Sh.2.4 bilioni kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo ingawa fedha hizo hazikuhusu ukarabati wa jengo hilo kwa sehemu iliyoungua. Hali hii ilielezwa inatokana na kuwa gharama zake hazikukasimiwa.

Mheshimiwa Spika, ni vema fedha hizo zikakasimiwa mapema ili kuendeleza ukarabati. Hata hivyo, Wajumbe walisisitiza umuhimu wa kuweka vifaa vyta kugundua tishio la moto ili janga kama hilo lisije kutokea tena katika Ikulu yetu na Ikulu Ndogo huko Mikoani.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa *TASAF*, Kamati ilielezwa kwamba, awamu ya kwanza ya mradi huu itakamilika mwezi Desemba, 2004 na kuwa awamu ya pili inategemewa kuanza Januari, 2005. Kamati ilielezwa kwamba, awamu ya pili ya mradi huu utazihusu Wilaya zote nchini. Ni matumaini ya Kamati yangu kuwa, majadiliano yataendelea vizuri na kwamba awamu hiyo ya pili itaanza mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuitia mafungu ya mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2004/2005, Kamati ilishtushwa na bei kubwa ya kununulia magari ya Serikali. Kamati ilijadili na kujiuliza kama bei hizo ndizo bei za chini ambazo Serikali inaweza kununulia magari yake. Kwa kweli bei hizi ni kubwa sana ambapo *Toyota Land Cruiser*, kwa mfano, hizi *VX linagharimu* zaidi ya Sh. 80 milioni.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikuridhishwa kuona kuwa Tume ya Utumishi wa Umma haijapangiwa fedha za maendeleo kwa mwaka huu wa fedha. Moja ya sababu

zilizotolewa ni kuwa Tume hii bado haina ofisi zake. Kamati inashauri kuwa Tume hii ipatiwe jengo litakalokidhi mahitaji ya Ofisi na Idara zake zote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, nitoe maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

(1) Serikali iangalie uwezekano wa kununua magari ya Wizara na Idara zake zote moja kwa moja kutoka kwa watengenezaji ambapo yatapatikana kwa bei nafuu kuliko ilivyo sasa ambapo yananunuliwa rejareja kutoka kwa mawakala kwa bei kubwa mno. (*Makofi*)

(2) Kutokana na kazi nyingi walizonazo Makatibu Wakuu wa Wizara ingekuwa vyema wasipewe madaraka ya kuwa Wenyeviti wa Bodi mbalimbali nchini kwa vile mara nyingi hawahudhurii vikao na badala yake wanawatuma Wasaidizi wao wakiwemo ambaao hawawezi kuchukua maamuzi yanayohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo na maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais na mapendekezo ya Bajeti kwa mwaka 2004/2005, Kamati inakubaliana na maombi ya fedha ya Sh.144,971,790,000/= ambayo yana breakdown ifuatayo:-

- (a) Ofisi ya Rais ya Rais, Ikulu:
Fungu 20 - Sh. 4,163,392,200/=
Fungu 30 - Sh.92,729,703,900/=
Jumla - Sh.96,893,096,100/=
- (b) Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma:
Fungu 32 - Sh.40,994,091,200/=
- (c) Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma:
Fungu 33 - Sh.690,735,000/=
- (d) Tume ya Utumishi:
Fungu 94 - Sh.6,393,867,700/=

Jumla yote - Sh.144,971,790,000/=

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni ya Kamati yetu. Napenda kumshukuru pia Mheshimiwa Dr. Mary M. Nagu, Waziri wa Nchi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utawala Bora), Makatibu Wakuu na Viongozi wote katika Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Umma, Sekretarieti ya Maadili na Tume ya Utumishi wa Umma, kwa ushirikiano mzuri ambaao wameutoa kwa Kamati yangu katika kipindi chote cha mwaka 2003/2004. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kuchambua kwa makini utekelezaji wa mapendekezo ya Bajeti ya mwaka 2004/2005 ya Ofisi ya Rais.

Naomba pia nimshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Kipenka Mussa, Makatibu wa Kamati yetu Ndugu Ernest Zulu, Ndugu Aggrey Nzowa na Ndugu Emmanuel Mpanda, kwa kuihudumia vyema Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, inaunga mkono hoja hii na kwa heshima kubwa, tunaliomba Bunge lako Tukufu lijadili hoja hii na hatimaye kuipitisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Mwanga kwa kunisaidia katika utekelezaji wa majukumu yangu kama Mbunge wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naomba kuwasilisha, ahsante. (*Makofî*)

MHE. GRACE S. KIWELU - MSEMAJI WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Yetete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, aliyefariki ghafla tukiwa hapa Dodoma kwenye kikao hiki cha Bajeti. Tunamwomba Mwenyezi Mungu, ailaze roho yake mahali pema peponi, *amin*.

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, pamoja na wataalam wao wote kwa ujumla, kwa kuandaa Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wote waliochaguliwa kutuwakilisha katika nafasi mbalimbali zikiwemo Bunge la Afrika na Bunge la *SADC*. Kipekee napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, kuwa Makamu Mwenyekiti na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mbunge wa Karatu, kuwa Katibu Mkuu wa Chama na mimi mwenyewe kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa, nawapongeza sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumshukuru Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge wa Jimbo la Micheweni, ambaye ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Ofisi ya Rais, Utawala Bora, kwa ushirikiano wake katika kuandaa Bajeti hii. Aidha,

tunampongeza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani, kwa kuiongoza Kambi yetu kwa umahiri na ukakamavu mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mara nyingi viongozi wetu wa juu wamekuwa wakijitangaza dunia nzima kwamba, Tanzania ni nchi ya mfano wa kuigwa katika Utawala Bora lakini kutokukomaa kwa vyombo vya dola na watendaji wake katika Mfumo wa Demokrasia ya Vyama Vingi ni kitu kinachopaswa kurekebishiwa.

Tunasema haya kutokana na mapungufu ambayo yanatokea huenda kwa makusudi au kwa kutokuelewa wajibu na mipaka ya vyombo vya dola na utumiaji wa mali za umma katika masuala ya kisiasa. Mfano ni matumizi ya Jeshi la Polisi (*FFU-Section*), kuzunguka na kupandisha bendera nyekundu kwenye mikutano ya hadhara inayohutubiwa na Viongozi wa Vyama vya Siasa, tofauti na namna linavyofanya kwa Chama Tawala. Mbinu hii ya kiimla inatumika kuwachanganya raia wema na kuwapa sura tofauti kuhusu mwelekeo wa siasa za Vyama Vingi hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya ni matumizi ya mali za walipa kodi, kwani kodi hazichagui ni mpinzani au sio mpinzani wote tunalipa. Magari ya Serikali, Mashirika na taasisi za umma kutumika kwenye masuala ya siasa, hili ni suala linaloondoa kabisa dhana ya Utawala Bora na uwajibikaji katika mfumo wa sasa wa Siasa za Vyama Vingi. Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora, atoe miongozo kuhusiana na mambo tuliyoyaeleza hapo juu, kwa manufaa ya nchi yetu na sifa zake duniani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aliyoeleza Msemaji wetu Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya rushwa na hatua ambazo amependekeza zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kuliwezesha zaidi Bunge, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Mkuu wa *PCB* kwamba, ziwajibike kwa Bunge na sio kwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, rushwa imezidi kwa sababu hakuna uwajibikaji ndani ya Serikali, upo ushahidi wa matukio mengi tu ikiwa ni pamoja na wizi wa mamilioni ya fedha kwa kuagiza vifaa vibovu kinyume na utaratibu kama ilivyotokea Wizara ya Elimu na Utamaduni kununua *computer* 225 kwa zaidi ya Sh.290,000,000/=, wahuksika wamehamishiwa sehemu nyingine na hakuna hatua iliyochukuliwa na *PCB*. Taarifa ya *Auditor General* inaelezea kila kitu. Sasa ushahidi gani Serikali inahitaji katika matukio ya rushwa zaidi ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali japo kwa kuanzia ili kuonyesha tu kwamba iko serious? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wapo watu wengi waliowahi kutoa taarifa kama vile Ndugu Mtikila lakini hakuna hatua iliyochukuliwa. Tunaendelea kusisitiza kama aliyooyasema ni uongo, achukuliwe hatua kali vinginevyo waliotajwa wafkishwe Mahakamani. Hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa Polisi wasiwe wao ndio wapelelezi na waendesha mashtaka, kazi hiyo ifanywe na Mkurugenzi wa Mashtaka (*DPP*) na Mkurugenzi Mkuu wa *PCB* ateuliwe na Rais na kuthibitishwa na Bunge na taarifa kamili ya utekelezaji wa *PCB* zifkishwe kwenye Kamati husika ya Bunge ili kutoa uwajibikaji mkubwa zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa zipo hatua zilizochukuliwa katika kuimarisha Utawala Bora, lakini malengo ya hatua hizi hayatafikiwa kama tu, mambo yafuatayo hayatazingatiwa:-

- (a) Kuchukua hatua au kuwa na utaratibu wa kuwajibika kwa kila kiongozi mambo yanapotokea katika eneo lake.
- (b) Rais awawajibishe wahusika bila ya kuwaonea haya.
- (c) Kuimarisha ukaguzi wa ndani kwa kila sekta.
- (d) Kuwezeshwa kwa Bunge na Kamati zake kufanya uchunguzi wa mara kwa mara katika maeneo ambayo yanashukiwa kuwa na ubadhirifu na upotevu wa fedha.
- (e) Utaratibu wa kuwachukulia hatua wahusika uboreshwe na hasa uharaka wa kuchukua hatua tofauti na sasa ambapo hatua zinachelewa sana.
- (f) Wanaofanya vizuri watambuliwe kwa kupongezwa na kupewa tuzo/zawadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, rushwa mbali na kwamba ni adui wa haki, pia inapokithiri kama kwetu, hukwamisha maendeleo na ukuaji wa uchumi hivyo ni budi kuipiga vita kwa kutumia kila mbinu inavyowezekana kuitumia.

Mheshimiwa Spika, demokrasia siyo suala la kuwa na miundombinu tu bali pia ni kuwa na miundombinu ya usimamizi. Kwa upande wa Tanzania, kuna matatizo makubwa ya kutokuwepo na miundombinu ya usimamizi. Kila miundo iliyopo ya usimamizi ni ya kirasimu na inawajibika kwa mamlaka ya Kiserikali kama Tume ya Maadili, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Taasisi ya Kuzuia Rushwa na kadhalika. Kambi ya Upinzani inafikiri wakati umefika wa kuwa na mamlaka huru ambazo zitakuwa zinasimamia taasisi za umma zitakavyoendeshwa badala ya kuripoti kwa mamlaka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo makubwa kwenye Idara za Serikali kuhusu uhamisho. Imebainika kwamba, wapo baadhi ya watumishi baada ya kupewa uhamisho kwenda vituo vipya, inawachukua muda wa miezi michache tu kurudi kwenye vituo vile vile ya awali na nafasi zile zile. Hii inatia mashaka makubwa.

Kwa muono wa kawaida, rushwa lazima inatumika kwa suala kama hili. Tukumbuke rushwa sio ya pesa tu hata upendeleo wa dhahiri unaowanyima wengine haki zao za msingi nayo vile vile ni rushwa na hicho kitu ni kibaya kama UKIMWI na Polio. Ni kitu cha kukipigia kelele kwa nguvu zote kwani kinawagawa watumishi wa umma na kuwaondolea moyo wa uchapaji kazi na uwajibikaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunazipongeza juhudzi za Serikali kwenye Idara ya Ajira (TUMEAJIRI), kwa kiasi fulani inawajibika lakini bado kuna vigezo vinavyotolewa kwa waomba ajira kama vigezo vya kuondoa kundi fulani na kuwapa watu fulani *opportunities* ya kubadilisha ajira moja kwenda nyingine. Kigezo cha uzoefu wa kuanzia miaka mitatu, mitano na kuendelea, ni dalili za kumtoa mhitimu aliyetoka Chuoni. Uzoefu ataupata wapi kama Serikali haikumpa uzoefu kwani watumishi wote uzoefu hawakuupata vyuoni wameupata kwenye ajira? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hili Kambi ya Upinzani inashauri kigezo hiki kiondolewe kama sifa mojawapo ya kupata ajira kwenye taasisi na idara za umma. Mbali na hilo TUMEAJIRI bado hawajadhibiti taasisi zinazotangaza nafasi wakati zimeshajazwa au zimewekwa kwa ajili ya mkubwa fulani wakati ameshatoa *ki-memo* au ana mtu wake. Sehemu nyingine hata usaili huwa hauitishwi pamoja na kutoa matangazo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hii sio kama inadharaulisha taaluma husika, bali pia utendaji wa watu wanaopewa kazi za zawadi unaharibu kabisa utendaji kazi katika idara husika. Kambi ya Upinzani inamwomba Waziri apate marejeo ya ajira hasa kwenye taasisi zinazoundwa kwa Mikataba na sheria zilizopitishwa Bungeni. Tunamtaka Waziri ahakikishe utaratibu wa *vi-memo* unakoma mara moja ili Watanzania wasio na *ma-referee* au vigogo nao waweze kupata haki yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania inao vijana wengi na wenyewe sifa za uwezo wa kufanya kazi, lakini kwa njia moja ama nyingine wanaamua kukimbilia nchi za nje na hivyo kupoteza mchango wao katika Taifa hili licha ya Serikali kugharamia elimu yao. Kitu kinaachotushangaza ni kwamba Tanzania inao Wakuu wa Wilaya na Mikoa ambao umri wao ni miaka zaidi ya 60.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa wamefanya mengi kwa Taifa letu hivyo imefikia wakati wa kuwapa nafasi vijana nao waweze kutoa mchango kwa Taifa lao sasa na hao wakawa washauri kwa vijana, kuendelea kukaa kwenye uongozi vijana watapata wapi uzoefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa umri wa utendaji kazi kwa hawa watu vitiliwe mkazo ili kuwapa nafasi vijana wahitimu washike usukani wa Taifa letu badala ya kutumikia Mataifa mengine, tuache kugawa vyeo kama shukrani au zawadi, tuangalie vigezo vinavyohitajika kwa manufaa ya Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna suala la watumishi wa umma kuhamishwa baada ya kuharibu au kufanya ubadhirifu wa dhahiri na kupelekwa sehemu nyingine. Mfano, mtu ameharibu Mkoa wa Dar es Salaam anapelekwa Rukwa au Kigoma. Hii ina maana gani katika uwajibikaji kwa ujumla? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani na wananchi kwa ujumla tunalionia jambo hilo kuwa ni kulindana tu, hivyo tunashauri ni bora kitu kama hicho kinapotokea

wahusika wachukuliwe hatua za kinidhamu badala ya kuhamisha uozo toka sehemu moja na kuupeleka sehemu nyingine. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, watumishi wa Serikali, utendaji wao unaweza kupanda na kushuka kutegemeana na mazingira wanayofanya kazi. Utendaji wa kazi kuwa mbaya unatokana na *u-veteran*. Watumishi kukaa sehemu moja muda mrefu na kuona kuwa kila kitu anakielewa hana *challenges* ya jinsi wengine wanavyofanya kazi na mazingira tofauti na yale aliyoyazoea ye.

Kambi ya Upinzani inashauri kuwa tuwape watumishi mazingira tofauti ya utendaji kazi ili watendaji waondokane na mawazo ya kudumaa au kujenga himaya. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, maaskari walioajiriwa katika vyombo ya ulinzi wana kanuni na taratibu zao zinazowaongoza katika kupanda au kushuka kwa maslahi. Kupanda kwa mishahara yao hakufuati kanuni sawa na zile za Idara Kuu ya Utumishi. Lakini ni kweli kwamba kuna watumishi amba ni waajiriwa katika vyombo vya ulinzi lakini sio askari, tunaomba ufanuzi toka kwa Waziri maslahi yao na upandishwaji wa vyeo unashughulikiwaje kwani kumekuwepo na manung'uniko ya hapa na pale.

Mheshimiwa Spika, mishahara ni kitu kinachoongeza tija kwa Taifa na vile vile ni motisha kwa watendaji ili kufikia malengo. Ni ukweli usiofichika kuwa watumishi wa Serikali wanashindwa kufanya kazi ya Serikali na kutumia muda mwangi kushughulikia miradi binafsi ya kuwaongezea kipato, kitu kinachosababisha huduma mbovu au wenye shida kutokupata majibu ya vitu au taarifa kwa wakati toka Serikalini. Aidha, wapo watendaji wengi wazuri wanaoingia au kuchukuliwa na makampuni/miradi binafsi kwa sababu ya mshahara mzuri.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii aeleze analishughulikia vipi suala hili. Au mfanyakazi wa Serikali ya Tanzania inabidi aendelee kutumia bongo ili aweze kumudu maisha kama tulivyoelezwa na Serikali hapa Bungeni. Lazima tuwe wakweli, nyongeza inayotolewa kwa watumishi wa Serikali haiendani sambamba na hali halisi ya gharama za kimaisha. Ili kuficha aibu ya namna mfanyakazi wa Kitanzania anavyobanwa mbavu kimshahara, Serikali imeamua kulifanya ongezeko la mishahara kwa watumishi wake kuwa siri. Hivi ongezeko la shilingi elfu nane au kumi tunalificha la nini? Kama ni suala la kuogopa eti bei za vitu zitapandishwa kiholela mbona bei za vitu na huduma zinapanda kila kikicha? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma wanacheleweshewa sana upandishwaji vyeo kwa mujibu wa muundo wa utumishi Serikalini na wakipandishwa vyeo inachukua muda mrefu sana kubadilishiwa mishahara na baadaye kulipwa malimbikizo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri afuatilie tatizo hili na kulipatia ufumbuzi haraka. Aidha, Serikali itenye fungu ambalo litakidhi malipo ya malimbikizo ya watumishi wa umma ili walipwe haki zao za kiutumishi. Kitendo cha Serikali kuanza kushughulikia mafao ya watumishi wake nusu nusu sio kizuri kwani

kinawavunja moyo watumishi wa kada nyingine. Tunaomba zoezi hili lifanyike kwa watumishi wote wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sekretarieti ya Maadili ya Umma. Chombo hiki cha utendaji wa Serikali na majukumu yake kwa kweli tunaweza kusema kuwa ni kama mchezo wa mazingaombwe.

Mheshimiwa Spika, toka Sekretarieti hii iundwe mpaka sasa wananchi ambao wanalipa kodi zao kusudi watendaji wafanye kazi hawajui ni viongozi wangapi wametaja mali zao na wangapi bado, ni hatua gani za kisheria zimeshachukuliwa kwa wale ambao wameandika majumba na magari ya thamani ya milioni hamsini kwa watoto walio chini ya umri wa miaka 15? Kibaya zaidi ni pale ambapo mwananchi anapotaka kuelewa kiongozi wake anamiliki nini na nini, anaambiwa ajaze *form* za maombi na kulipa fedha (*application fees*) na taarifa atakazozipata haruhusiwi kuzitoa popote. Hivi urasimu wote huu ni wa nini kama sio kutengeneza mfumo wa kulindana? (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza kuwa utendaji kazi wa Sekretarieti ya Maadili ya Umma ina manufaa gani kwa mwananchi wa kawaida na baada ya kufanya kazi yake kinachofuata ni nini?

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri ili kutoendelea ku-*abuse* fedha za walipa kodi, kitengo hiki kiondoshwe kabisa na Bajeti yake ielekezwe kwenye huduma muhimu kama afya, elimu na kilimo. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, majukumu ya sekretarieti hii yanaweza kufanya na vyombo vingine kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, *PCB*, Usalama wa Taifa na vingine vingi ambavyo Serikali imejiundai na kama tulivyoshauri ili taarifa na kazi za vyombo hivi ziweze kufanyiwa kazi ipasavyo ni muhimu vyombo hivi viwajibike Bungeni.

Mheshimiwa Spika, suala la Ikulu ni suala nyeti sana kwa jamii nzima ya Kitanzania na vile vile mbele ya sura ya Kimataifa. Kama alivyoeleza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni katika kikao kilichopita cha Bunge kuhusu moto uliozuka na kuunguza Ikulu ya Watanzania nami nina machache ya kuongezea.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliyoundwa na Serikali na kutoa taarifa yake juu ya uchunguzi wa fedha tulioipata Watanzania wote kuhusiana na kuungua kwa Ikulu, ilikuwa ni taarifa ya jumla na sio taarifa ya uchuguzi. Ni taarifa ambayo kwa mtu ye yeyote hawezni kukubaliana nayo, Tume iliyopewa idhini ya kuchunguza tukio kama hilo si rahisi kutoa taarifa kama hiyo labda tuelezwe kuwa wameshindwa kufanya kazi kwa sababu ambazo Serikali inazijua.

Mheshimiwa Spika, nadhani wahusika wamesahau kuwa Ikulu sio mali ya mtu au chama bali ni mali ya Watanzania wote hivyo wana haki ya kuelewa chanzo cha hiyo hujuma. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, Kiongozi wa Upinzani wakati wa hotuba yake kuhusu tukio hilo alishauri Serikali kuleta wachunguzi ambao hawana uhusiano na Serikali ili kufanya kazi yao bila kuingiliwa na chombo chochote cha dola na kutupa chanzo halisi cha tukio hilo, lakini ushauri wake ukapuuzwa. Taarifa ya Kamati inasema chanzo cha moto ni pasi wanasahau uchakavu wa jengo hilo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika moja ya vikao vya Bunge lako Tukufu, Bunge lilikwishatenga fungu la mabilioni ya fedha kuifanya matengenezo Ikulu, lakini cha kushangaza kumbe badala ya kuanza kwa kukarabati anapolala na kushinda Rais na wageni wetu wa Kimataifa wakakarabati kwanzza uzio wa Ikulu. Hii ni sawa na kununua matairi ya gari wakati gari lenyewe huna! (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, utawala bora kama nilivyosema ni suala pana na sio tu kuwa na vyombo vingi vya kusimamia tu, bali ni jinsi vinavyofanya kazi na uwajibikaji wake ukoje. Kuna suala ambalo sasa limekuwa ni ugonjwa au fashion kwa yeoyote yule anayeteuliwa na Rais au mamlaka nyingineyo anakuwa haguswi, hawajibishwi hata kama anaboronga au analalamikiwa namna ya utendaji wake.

Mheshimiwa Spika, jambo hili tunalionaa kama ndio kigezo kikubwa cha kuhalalisha uzembe mkubwa wa kutowajibika. Jambo hilo limejionyesha hata hapa hapa Bungeni kwa baadhi ya Waheshimiwa kutaja jinsi baadhi ya viongozi wanavyopwaya kiutendaji kwenye nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iwaangalie hawa inaowaona viongozi bora, wawe bora katika kuleta maendeleo na kufikiwa kwa malengo na siyo kuwaacha kuendelea kuvuruga wananchi au kukwamisha maendeleo kama ambavyo imejitokeza Wilayani Karatu, Kigoma-Ujiji, Pwani na kwingineko. Kulindana hakutatupeleka popote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kudondoaa mapungufu ya wazi kuhusiana na Wizara hii na kazi zake kwa ujumla kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya awali kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Nianze kwa kuwapa pole Wabunge wote waliopata misukosuko ya kufiwa na wapendwa wao na kupata ajali. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa kwa nyadhifa mbalimbali za Kimataifa akiwemo hivi karibuni kaka yangu Balozi Mchumo. Hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aidha naungana pia na Waheshimiwa Wabunge wengine wote kumwomba Mola amweke mahali pema peponi Marehemu Yeti Sintemule Mwalyego, aliyetangulia mbele ya haki. Nomba niseme kabisa kwamba naunga mkono hoja hii iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Mawaziri wa Nchi, hawa wawili kwa hotuba yao nzuri sana. Lakini mimi nitakuwa na mambo mawili tu ambayo nataka nichangie nayo yanahu su utawala bora. Misingi ya utawala bora ni utawala wa sheria unaozingatia haki za binadamu, ni utawala unaohimiza kuwepo kwa uwazi, ukweli na haki katika utendaji kazi wa kila siku wa Serikali. Lakini inashangaza kuwa katika Halmashauri zetu na *Alhamdulillah* Halmashauri hizi ni chache bado Watendaji Wakuu hawasimamii dhana hii ya kuwepo kwa utawala bora. Nitatoa mfano, mwezi Februari, Halmashauri yangu ya Manispaa ya Tabora kupitia Mtendaji wake Mkuu waliamua kuvunja vibanda vya biashara vilivyojengwa maeneo yasiyoruhusiwa kisheria yaani ni *road reserve*.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba mimi sipingani kabisa na dhana hii na uamu zi wa kuvunja vibanda hivyo maana haya ni mambo ambayo tulishawaahidi wananchi kupitia Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Sipingani kabisa, lakini kinachosikitisha ni kwamba chanzo cha mgogoro huo ni watendaji hao wa Halmashauri kutoheshimu misingi ya utawala bora katika kuwaongoza wananchi kuvunja sheria pale ambapo wanawapa maeneo haya huku wakijua fika kabisa kwamba huku ni kuvunja sheria. Wanaelewa kabisa maeneo haya hayaruhusiwi kujenga, lakini wanawapa masharti makubwa, kwa mfano, pale barabara ya Tabora karibu na Mkuu wa Wilaya, wananchi wa pale walipewa masharti ya kwanza wajenge vizuri mabucha yao kwa segmenti, waweke marumaru na vioo. Mwishoni wakawapa leseni za biashara. Lakini la kusikitisha sasa baada ya kuwapa leseni hizo ikapita siku tatu au wiki wakavunjiwa mabanda hayo kwa *notice* ya siku moja hadi wiki moja tu. Mambo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ingawa kutokujua sheria siyo kinga ya kuvunja sheria, lakini wale ambao ndio wangekuwa dira kwa wananchi hawa wanawapa leseni kwenye sehemu ambazo haziruhusiwi hivi taratibu za utawala bora, zinasemaje kwa hawa watendaji wa Serikali ambao wanawaingiza wananchi katika kuvunja sheria? Wanachukuliwa hatua gani? Maana hawa ndio wamekuwa chanzo cha wananchi hawa kuvunja sheria. Lakini Mheshimiwa Waziri pia naomba anieleze hivi ni kipi kinawashawishi kuvunja sheria hawa watendaji wakuu? Maneno hayo. Leo sina mengi ya kusema nataka niseme la pili ambalo nitapenda Waziri huyu wa Utawala bora ambaye namwelewa ni mzuri kabisa, anitolee majibu, ni suala la uundaji wa Tume za Serikali na hatma ya taarifa za Tume hizo. Serikali inaunda Tume kuchunguza kitu fulani, taarifa zinatolewa sasa hatma ya taarifa hizo inakuwaje. Nitatoa mfano. Katika Manispaa yangu ya Tabora, Diwani mmoja wa Manispaa ambaye sasa ni marehemu alitoa shutuma katika vikao vya Halmashauri yetu kuhusu ubadhirifu wa matumizi ya fedha za MMEM kwamba zilikuwa zimehujumiwa. Baada ya kuona kuwa kwenye Manispaa mambo hayaendi akamwandikia Mkuu wa Mkoa wa Tabora kuhusu suala hili. Mkuu wa Mkoa akaunda Tume ya kuchunguza hiyo tuhuma. Tume ili wajumuisha wataalam wa mambo haya, akiwemo Mwenyekiti ambaye ni Mhakikimali wa Mkoa wa Tabora, akawemo na *DRSO, Local Government Officer*, Mboharia na *DAS*.

Mheshimiwa Spika, Tume hiyo ya Mkuu wa Mkoa ikathibitisha tuhuma yote ya Marehemu Diwani huyo wa Tabora na Mheshimiwa Masilingi amekaa Tabora pale anapafahamu vizuri. Kiti cha mbao tu cha kawaida baada ya kuuzwa shilingi elfu kumi

kikauzwa shilingi hamsini na tano elfu. Meza ya kawaida tu badala ya kuuzwa shilingi elfu arobaini ikaузwa shilingi laki moja na thelathini elfu. Kabati badala ya kuuzwa shilingi sitini elfu, likauzwa laki moja na arobaini elfu. Tume hiyo iligundua mambo mengi tu ya ubadhirifu kama vile uteuzi wa Wazabuni ulikuwa haufuatiliwi na kadhalika. Inakadiriwa kuwa zaidi ya shilingi milioni arobaini zilihujumiwa. Lakini siku ya tatu kabla ya Tume kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Madiwani, Diwani aliyehoji uhalali huo akapigwa risasi. Siku ya pili akafariki katika mazingira ya kutatanisha kabisa maana alikuwa ameahidi kuleta nyaraka zingine za kuthibitisha ubadhirifu huo ambao Kamati Teule ya Mkuu wa Mko wa Tabora iliugundua. Wauaji hawakuchukua fedha wala chochote nyumbani kwa Marehemu Ibrahim Daudi Mlilo. Lakini Marehemu kule hospitali aliwataja wale ambao walihusika na kifo chake.

Mheshimiwa Spika, la kushangaza ni kuwa mpaka hivi sasa ubadhirifu alioutaja Marehemu Mlilo pamoja na kuthibitishwa na Kamati Teule ya Mkuu wa Mko hakuna lolote lililofanyika. Ukimwuliza Mkuu wa Mko anasema suala hili amelipeleka kwenye Baraza la Madiwani. Ukimwuliza Meya wa Manispaa ya Tabora anasema mimi sikuunda Tume hiyo, nendeni kwa Mkuu wa Mko. Kila mtu anamtupia mpira mwenzake. Sasa naelewa kwamba kwa kweli watu wa kuwajibisha hawa watendaji wakubwa ni Madiwani. Lakini siyo siri kwamba pale Manispaa ya Tabora Madiwani wanaogopa kufa kama alivyokufa Diwani mwenzao. Sasa unapokuwa na hali kama hii ambayo Mkuu wa Mko ameunda Tume, Tume imetua majibu, ameyapeleka kwenye Manispaa. Sasa, kwani utawala bora ndio unasema basi kazi yake imekwisha? Wananchi wa Tabora wamenitura nige niulize kwa Mheshimiwa Waziri ambaye anahusika na Utawala Bora kwamba hivi ndiyo suala lao limekwisha? Hivi mwenzao ambaye alikuwa anahoji ubadhirifu na ubadhirifu huo ukathibitishwa na Tume ya Mheshimiwa Mkuu wa Mko, ndiyo basi au wafanyeje hawa wananchi wa Tabora? Wamenitura na naomba Mheshimiwa Waziri Masilingi anisaidie sana, najua yeze ni Askari wa Mwavuli na Tabora amekaa, mazingira ya Tabora anayajua. Lakini tufanye hili kwa kweli tukimkumbuka Mheshimiwa Mlilo. (*Makofi*)

(Hapa Mheshimiwa Mbunge alishikwa na uchungu akatokwa na Machozi na kushindwa kuendelea na mchango wake)

MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza nichukue nafasi hii na mimi kutoa salaam zangu nyingi za rambirambi kwa familia ya Marehemu Yetete Mwalyego. Naomba Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi. *Amina*. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, watumishi wote, wafanyakazi na viongozi katika Ofisi ya Rais kwa hotuba nzuri na kwa kweli kwa kazi nzuri wanayofanya. Lakini niseme tu kwamba suala la mishahara ambalo nimelizungumzia hapo nyuma nimpongeze kwa hatua ambazo anazichukua kurekebisha mishahara. Najua kwamba kule kupandisha mishahara kwa kiwango kikubwa mara moja kunaweza kuleta *distortion* katika uchumi na hata bei kupanda. Lakini tunasema basi hii *systematic and*

gradual inclement ya mishahara basi iwe na kasi ambayo ni ya kuridhisha ili tufike mahali ambapo watumishi wa Serikali wanaweza kupata mishahara ambayo inaridhisha na kuongeza tija.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo mimi nizungumzie *rationalization* ya mishahara katika utumishi wa umma. Ni ukweli usiopingika kwamba kuna tofauti kubwa mno, basi kama hao wengine hawawezi kuongezewa kwa kiasi kikubwa basi kusiwe na njia ya kuwavunja nguvu hawa watumishi wa Serikali kwa kuunda *agencies* za Serikali na wale kupewa mishahara ambayo ni *world class*. Sasa hivi kuna hii ya kuanzia *Government Agencies* na kwa kweli unakuta mishahara yao ni mikubwa sana, lakini vile vile unapozungumzia mashirika ambayo bado ni ya umma wale nao si watumishi wa umma, kwa nini mishahara yao inakuwa na tofauti kubwa sana? Mimi nadhani kuna haja ya kuliangalia hilo kwa sababu hawa wote wanafanya kazi za umma, hizi si *private companies* na nimeshazitaja huko nyuma zinajulikana. Mimi nadhani kuna haja ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye utawala bora. Pamoja na kazi nzuri sana ambayo imefanyika na taasisi zetu za *PCB* pamoja na *Secretariat* ya Maadili bado kuna haja ya kuziboresha taasisi hizi na kuzipa nguvu zaidi ili ziweze kufanya kazi vizuri. Kwa kweli vyombo vyote vya usimamizi wa shughuli za Serikali na utawala bora ambavyo vinaitwa *oversight bodies* bado havijapewa nguvu inayotakiwa na nyenzo zinazotakiwa. Vyombo hivi ni Bunge kuititia Kamati yake ya *PAC*, *PCB* pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Tunatakiwa kwa kweli tuendelee kuzipa nguvu zaidi. Vyombo vyote hivi lazima viripoti Bungeni moja kwa moja ikiwemo pamoja na *PCB* na hili tumekuwa tukilizungumza mara nyingi. Lakini bado unakuta Mkaguzi Mkuu hana nyenzo za kufanya kazi yake kissahihi. *PAC* yenewe bado haijapewa nyenzo inayotakiwa ili iweze kwa kweli kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia bado kuna masuala ambayo Wabunge wamekuwa wakizungumzia kama suala la Bunge kuititia Mikataba ya wafadhili, ya madeni na mikopo pamoja na ufadhili mwengine. Mimi nadhani bado kuna haja ya kuendelea kulizungumza hili ili ifike mahali tukubaliane. Hizi *International Financial Institutions (IFI)* zina *paradox* za ajabu sana. Wakati wanazungumzia utawala bora na wenyewe vile vile wanaendelea kutotilia umuhimu wa kusisitiza Serikali zetu kuleta Mikataba hii ndani ya Bunge. Mimi nadhani kuna haja ya kufanya hivyo. Kusema kwamba hizo kazi za Serikali tu sidhani kama ni kweli, kama kweli tunataka ile *oversight role* ya Bunge ioneokane vizuri.

Mheshimiwa Spika, *PAC* na hata Mdhibiti Mkuu na Mkaguzi wa Serikali kuna haja sasa wafanye kazi za *performance audit*. Huu ni ukaguzi wa ubora wa utekelezaji wa miradi. Sasa hivi *PAC* na hata Mkaguzi Mkuu tunaangalia tu mahesabu, nani alikula nini, nani alichukua *imprest* lakini kuangalia mradi kwenda kufanya *performance audit* kwamba mradi huu umegharimu sh. 50bn/= lakini thamani yake kwa kweli ilikuwa labda shs. 20bn/= tu na shs. 20bn/= ni hasara au zimeliwa, bado hatujakuwa na *capacity* ile. Kama *PAC* na kama *Controller and Auditor General* mimi nadhani kuna umuhimu wa

kufanya *performance audit*, ambapo ni suala ambalo linahitaji nyenzo na uwezo wa kifedha na watu ili kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini kukutana na wafadhili mwaka hadi mwaka kuna haja kama Wabunge au kwenye Kamati zetu. Tuliangalie hilo. ifike mahali basi, nipayendekeze kwamba kama ambavyo nchi zingine za Afrika zimefanya tuwe na *Assurance Committee* ya Kudumu hapa Bungeni ambayo itakuwa inafuatilia utekelezaji wa mihadi ya Serikali, kwamba Waziri aliahidi kitu fulani au alisema kitu fulani je, kimeteketeleza na vitu kama hivyo. Hata hii *PAC* ambayo mimi ni mjumbe, labda sasa ingekuwa *Public Accountability Committee, rather than Public Account Committee*, iwe ni Kamati ya Uwajibikaji wa Serikali. Nadhani tukifanya hivyo hii *role* ya *oversight* na utawala bora tutaiona kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa. Mimi niseme kwa dhati kabisa kwamba suala la rushwa kuzungumzwa lisiwekewe mizengwe. Kwa kweli tuendelee kuachia suala hili lizungumzwe kwa nguvu ndani na nje ya Bunge. Liingie kwa njia tu ya kuzungumza suala hili kwa wazi ndipo tunaweza kukabiliana nalo. Hii ya kwenda kuanza kutoa kauli za Serikali *ku-preempt* majadiliano ya kuzungumzia rushwa halitatuifikisha popote. Nchi zote zinaonyesha kwamba, kuzungumza kwa nguvu suala la rushwa ndipo unaweza kulikabili, *preemption* hizi tuziache, la sivyo kwa kweli hali hii itaendelea kuwa mbaya. Mimi nikiri hapa wazi kwamba kwa kweli chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa uthumi wa nchi hii umekuwa kwa kasi sana kuliko nchi nyingi za jirani. Tumekusanya kodi nyingi sana na miundo mbinu tumeboresha na suala la umaskini tunalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, hilo limefanyika na hata kule katika Jimbo langu la Ukonga, Ilani ya Uchaguzi tumeteketeleza kwa kiasi kikubwa sana kwa kufanya miradi mingi. Uchumi wa nchi unakua tunakubali lakini mimi niseme kwamba yatakuwa ni makosa makubwa kulinganisha ukuaji wa uthumi na kupungua kwa rushwa. Utafiti pamoja na uzoefu unaonyesha kwamba pale ambapo uthumi unakua kwa haraka, kweli miundombinu itajengwa lakini rushwa vile vile itapanda sana. Tuangalie nchi za Nigeria na Kenya ambapo uthumi umekua, rushwa ndio inapata nafasi nzuri.

Kwa hiyo, wakati uthumi ukikua ndio haja ya kuzungumzia rushwa kwa nguvu inahitajika. La sivyo tutakuwa tunajidanganya kwamba unaona uthumi umekua, sasa tunakusanya kodi nyingi sana. Kuna Mheshimiwa Waziri mmoja hapa anasema, mbona hatukuchukua hela yote kule *TRA* tukaja kugawana kwenye *Cabinet*. Kweli kauli kama hiyo unaweza kuitoa! Kwa sababu uthumi unakua, basi unadhani kwamba kwa sababu hela zimeongezeka lazima mziibe kama *Cabinet* ndiyo tuseme kwamba rushwa imepungua, siyo hivyo, hata kidogo.

Rushwa kubwa iko kwenye hiyo miradi inayoletwa na uthumi bora. Miradi mikubwa hujengeka wakati uthumi unakua na hiyo mikataba mikubwa pale ndiyo sasa kuna mianya mikubwa ya rushwa. Jenga madaraja makubwa na barabara nyingi na rushwa kubwa. Vitu hivi vinakwenda sambamba na ndiyo tunavipigia kelele. Sasa

tunaposema hayo yote mtu anaweza kusema kwamba ahaa hapana, uchumi wetu unakua kwa hiyo rushwa inapungua hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, kuna mifano ambayo tumeitoa lakini tumekuwa wala hatujibowi sawasawa ambayo inaonyesha kwamba Utawala Bora bado ni tatizo kwenye maeneo fulani na rushwa bado ni tatizo. Kuna Mheshimiwa Mbunge hapa amezungumzia suala la mradi na hiyo ndiyo naizungumza uchumi ukikua na miradi mikubwa inawekezwa na humo humo kunakuwa na rushwa kubwa. Limezungumziwa hapa jengo la Benki Kuu kwamba mpaka sasa limetumia shilingi bilioni 75 jamani mbona Bunge hatueleweshwi, basi kama tunakosea kuzungumza hilo basi tueleweshwe. Mheshimiwa Waziri asimame aseme hilo lilikuwa hivi na hivi, lakini linapokuwa brush aside tunalichukuaje wengine? Swali limeulizwa hapa halijapata majibu kwamba Bunge tumeidhinisha hivyo. Lakini habari ambazo zipo mitaani mimi sijathibitisha ni kwamba hata jengo lile si imara na kuna matatizo makubwa *architectural design* na nini. Sasa mpaka tupeleke suala hili kwenye *PAC* waanze uchunguzi kwa nini tusipate tu majibu ya Serikali tukaelewa kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa masuala ya Varambia hapa kwamba jamani huyu amelipwa bilioni 51 za Serikali Bunge limehusika vipi angalau kuidhinisha kwamba basi mlipeni kutoka kwenye fungu hili. Mbona njaa bilioni 10 mlikuja hapa kutuomba. Shilingi bilioni 51 za kumlipa huyu mtu aliyetushinda kesi Mahakamani kwa nini tuidhinishe kama Bunge. Sasa mtu anasema Utawala Bora huko hapa! Licha sasa ya kuidhinisha Bunge vile vile litataka lijue ni nani aliyehusika kama ni uzembe, kama ni utendaji mbovu nani amewajibika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hivi kwa nini neno uwajibikaji haliko kwenye *dictionary* ya nchi hii? Kwa nini tusifike mahali tukasema hapana wewe umetuletea hasara kumlipa huyu mtu shilingi bilioni 51 lazima uwajibike hata kama unakuwa ni Waziri hata kama ni nani uwajibike. Sasa maelezo hayo hayaji. Tukisema Utawala Bora haupo ahaa tunaletewa tamko la Serikali. Kuna mambo mengi ambayo yapo. Kwenye ununuzi na kwenye mikataba hii. Sasa hivi naambiya kuna msitu pale wa Rungusa kule Tanga, matiki ile ni mali kweli kwa Taifa. *Public Procurement Act* haitatumika pale naambiya kuna njia ya kuuza kwa bilioni 4 mtu ananiambia sijathibitisha hilo. Lakini thamani ya msitu ule ni *forty billion Tanzanian shillings*. Sasa kama ni *forty billion Shillings* halafu uuzwe kwa bilioni 4 itakuwa ni jambo la hatari na sisi tunalingojea. Hili bado sijawa na uthibitisho lakini tunalifuatilia. Ule msitu kweli ukiuzwa kwa njia ambayo siyo utaratibu mimi nadhani hili suala itabidi liangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, mengi yanazungumzwa ambayo lazima tuyaelekeze nguvu zetu. Tumeambiwa kuna rushwa katika uchapishaji wa vitabu katika Wizara ya Elimu na Utamaduni. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni ameingia hapa ndani. Je, ni kweli haya mambo watu wanaingiza vitabu mashulen ambavyo havikidhi kwa sababu tu ametoa rushwa basi vinachapishwa vitabu milioni moja na naambiya kuna mchapishaji mmoja sijui Nyota na Mkuki, sijui Nyota na Nguruwe mimi simjui, sijui hata wenye *Publishers* hao ni akinanani lakini najua kuna jina hilo linazungumzwa. Je, twende katika fedha zote zilizolipwa kwa *Publisher* huyu tuangalie

kama kweli *Public Procurement Act* ilitumika katika uchapishaji wa vitu vyote vya Serikali alivyochapisha. Hilo tutaangalia kwa sababu tuna *PAC* na tuna wataalam ambao wanaweza kuliangalia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli uwazi bado unakosekana katika masuala fulani fulani. Juzi nimezungumza hapa kuhusu *Public Appeals Authority* hakuna mtaalam wa ununuzi katika Bodi ile ambayo ukionewa katika masuala yote ya ununuzi ndiyo unakimbilia hakuna mtaalamu yule wa ununuzi na asilimia 50 ya Wajumbe ni hao hao aliowazungumzia Mheshimiwa Marwa hapa.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni pamoja na kuangalia kilio cha wananchi. Wananchi wanapopiga kelele huwaangalii kilio chao hakuna Utawala Bora. Wananchi wangu wa Kipawa ambao kwa muda wa miaka sita wamekuwa wakipiga kelele ni namna gani Serikali itawafidia au itawaondoa au haitawaondoa katika eneo la Kipawa ili waendeshe maisha yao kwa uwazi na kwa endelevu hakuna kinachosemwa. Ile tu kutamka kwamba hapana mradi ule wa kupanua uwanja wa ndege sasa hakuna endeleeni kujenga nyumba zenu, Vyuo vyenu msiwe na wasiwasi tutakapotaka kuja kuendeleza uwanja tutawafidia hata kama ni miaka 20 ijayo kulingana na sheria ya wakati huo hakuna tamko kama hilo. Wananchi wanaachwa wanateseka huu ni Utawala Bora kweli! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yapo mengi ya kuzungumza na ukienda kwenye suala la *PCB* pale kwa maana ya viongozi walioko ndani ya *PCB*. Kutokana na muda hili nitalizungumzia katika muda muafaka kutokana na muda ambao naona unanitupa mkono. Ninachotaka kusema lazima tukubali kuwa wa wazi kwenye Utawala Bora. Suala la rushwa turuhusiwe kuendelea kulizungumza ndani na nje na ni kwa kufanya hivyo tu ndipo kwa kweli tutafika mahali tupambane na rushwa. Rushwa haitoki lakini njia ni kuendelea kupambana nayo kama tunavyofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Mary Nagu, kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha leo asubuhi hii kuhusu *Management* ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Rais, nampongeza sana na bila kusita napenda nimhakikishie kwamba ninaiunga mkono hoja yake hii moja kwa moja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba pia ya wananchi wangu wa Jimbo la Mtama nichukue nafasi hii pia kuwapa pole wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kwa kufiwa na Mbunge wao mashuhuri Ndugu Yete Mwalyego, na ninamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia kuhusu kasi ya uhamaji wa watumishi katika Mkoa wa Lindi, lakini kabla sijafika hapo na mimi nieleze kero yangu moja haitafanana sana na ya rafiki yangu Ndugu Profesa Henry Mgombelo, aliyoitoa lakini inafanana

kidogo. Hili linahusu jukumu la Utumishi kuangalia sheria mbalimbali hasa za uhamiaji na kuzirekebisha sheria zile kwa kuzileta hapa ili iweze kujihakikishia kwamba inawathamini na kuwalinda watumishi wake wanaoathirika na baadhi ya sheria hizo hasa za uhamiaji na nitatoa mfano.

Mheshimiwa Spika, mtu anapozaliwa Tanzania katika maeneo ya mipakani na wazazi ambao si Watanzania waliohamia Tanzania miaka ya 1920 mtu huyo akazaliwa Tanzania, akasoma Tanzania, akasomeshwa mpaka akapata Shahada au Stashahada na Serikali ya Jamhuri, akafanya kazi miaka 20 hadi kufikia Ukurugenzi na baadaye uhamiaji inagundaiwa kwamba mtu huyu kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za *Immigration* si Mtanzania kwa sababu wazazi wake hawakuwa wa Tanzania ingawa ye ye mwenyewe alizaliwa Tanzania. Baada ya kuligundaiwa hilo mtu huyu anafukuzwa kazi bila kupata chochote kile kwa sababu eti si Mtanzania na sababu ni nini, kwa sababu wazazi wake hawakuzaliwa Tanzania. Mimi nasema Sheria za aina hii zimeanza kuitwa na wakati lazima tuzifanyie marekebisheso. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, kipengele kinachosema ili uwe Mtanzania mzazi wako mmoja lazima awe amezaliwa Tanzania kimeanza kuitwa na wakati na wala hakiwi *applied* yaani wala hakitumiki sana kwenye Mataifa mengi duniani. Kwenye nchi nyingi sana mtoto akizaliwa tu kule bora asitokane na diplomasia yaani asiwe mtoto wa Balozi anakuwa mwananchi wa nchi hiyo, sembuse mtoto aliyezaliwa katika nchi hii akakulia katika nchi hii, akasomeshwa katika nchi hii akafanya kazi kwa muda miaka 20 kwa nini huyu anapo julikana tu kwamba hakuwa Mtanzania kwa sababu wazazi wake hawakuwa Watanzania anafukuzwa kazi bila kupata haki zake zo zote.

Mheshimiwa Spika, lakini nikawa naijiliza mbona Tanzania hii hii huko nyuma hatukufanya hivyo. Mimi namfahamu Marehemu D. N. M. Bryceson, Marehemu A. K. Jamal, akina Dr. Sterling, Marehemu Austin Shaba, hawa wote hawakuwa Watanzania kwani wazazi wao hawakuwa Watanzania, lakini walifanya kazi kwa sababu *Immigration* baada ya kutambua kwamba hawa watu siyo Watanzania waliwajazisha fomu ya *naturalization* yaani ya kuwabatiza kuwa Watanzania na wakaendelea kufanya kazi. Haya yepi ya sasa hivi kumgundaiwa mtu na hasa kwenye maeneo ya mipakani kwamba wazazi wake hawakuzaliwa pale na amefanya kazi na amesomeshwa na Taifa anafukuzwa kazi na (hasa Kigoma anasema mwenzangu hapa Halimenshi Mayonga).

Mheshimiwa Spika, lakini pia naijiliza swali lingine mbona tunaajiri wafanyakazi kutoka nchi mbalimbali waliokuja kwa mikataba tu miaka mitano au miaka mitatu au mwaka mmoja na hatuwafukuzi.

Mheshimiwa Spika, namsemea rafiki yangu Anslem Masumbuko ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Mji, Mtwara Mjini, anasota na familia yake. Ameachishwa kazi kwa sababu wazazi wake siyo Watanzania. Lakini amesomeshwa na nchi hii na amefanya kazi katika nchi hii zaidi ya miaka 20 anasota na tumeipeleka kesi hiyo Ofisi ya Rais na ni matumaini yangu kwamba suala hili litapata uzito unaostahili kuokoa familia ya Mtanzania yule na tuangalie sheria za *Immigration*. Tuziangalie upya na

ziletwe hapa Bungeni na mimi nitakuwa mojawapo wa kupitisha marekebisho ya aina hiyo. Tusiache kile kipengele tunawaumiza Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nimesema nataka nizungumzie watumishi katika Mkoa wa Lindi kuhusu kasi ya uhamaji. Mkoa wa Lindi kihistoria utumishi wake ulikuwa duni. Hapo mwanzoni tunajua watumishi Mkoa wa Lindi walikuwa wanapelekwa kama adhabu lakini baadaye Serikali ikawa inatoa mkazo wa kuwaomba watu wanaohamishiwa Lindi na Mikoa mingine ya Kusini waende. Basi hilo limefanyika na kweli watumishi wanakwenda Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, lakini cha kushangaza ni kwamba wakifika Lindi hawakai, wengine wanakaa miezi tisa anahamishwa, mwingine anakaa mwaka mmoja anahamishwa na mwingine anakaa mwaka mmoja na nusu anahamishwa na mwingine anakaa miezi sita anahamishwa. Katika kipindi cha miaka mitatu na nusu kwa mfano, Lindi wamehamishwa viongozi wa juu kutoka ngazi ya Mkoa hadi Wilayani achilia mbali Maafisa wadogo wadogo wasiopungua 24 wakiwemo ma-*RPCs* watatu, Ma-*REO* wawili, Wakurugenzi wa Halmashauri zetu kama wanne, Maafisa Mipango wawili, achia mbali ma-*RC* wawili na Ma-*DC* watatu, acha mbali *TANROAD Engineers* wawili katika kipindi tu cha miaka mitatu na nusu kulikoni? Ni *coincidence*? Ni nini kinachofanya wakae kwa wastani wa mwaka mmoja nusu au miaka miwili ni nini ni mbinu tu za kwamba mtu anahamia kule lakini ameishasuka mipango kwamba nikishatumikia kifungo hiki kwa muda wa mwaka mmoja Lindi au miwili niwe ninarudi.

Haya yanatokea kwenye Mikoa mingine nawauliza wenzangu wa Rukwa na wa Kigoma. Anasema ni Jehanamu. Kwa nini kuna Mikoa watu wakifika maana yake sasa wanarioti kwenye vituo lakini hawakawii wanaondoka kunatokea kitu gani?

Mheshimiwa Spika, mimi nasema hivi watumishi wasipokaa katika sehemu moja angalau kipindi cha miaka mitatu, minne hadi mitano hatuwezi kuwa na maendeleo endelevu. Wakati wote tutakuwa tunaanza upya kupata kasi au *momentum* ya maendeleo na ningeomba Wizara ya Utumishi kumwomba Mheshimiwa Waziri alizingatie hili kwamba baadhi ya Mikoa ile ile ambayo ina matatizo makubwa watumishi wake hawakai kwa muda mrefu na wananchi wa Lindi wameanza sasa kuhisi kwamba inawezekana watumishi wanakuja tu pale kwa muda ili waondoke na sijazisema Wilaya nyingine za Mkoa wa Lindi, hizi ninazozisema ni za pale Makao Makuu, Lindi Mkoani. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba inawezekana sababu moja ni kwa sababu miundombinu katika Mikoa hii hasa ya Lindi ni duni na kwa vyovyyote vile wananchi au viongozi wanaohamishiwa kule kwa kuona kero hizo za miundo mbinu wanalazimika wakati mwingine kuondoka. Kwa hiyo, changamoto kwa Serikali ni kwamba moja inabidi kuendeleza na kuimarisha miundombinu ile. Naipongeza Serikali kwamba sasa barabara imo mbioni na daraja limekamilika lakini kuna suala la umeme, kuna suala la mawasiliano na barabara za Mkoani kwani ni mbovu zaidi. Miundombinu tukiikamilisha nadhani kwa muda mrefu inawezekana watumishi watacaa Lindi kwa muda mrefu zaidi. Lakini naiomba Wizara kwamba watumishi hao

wanapohamishiwa kwenda Lindi sababu za kuhama Lindi na kwenda katika sehemu nyingine zijulikane kama hazipo basi turuhusiwe sisi kuwa na *the benefit of doubt* kwamba inawezekana wanahama tu kutokana na matatizo na wana *god fathers* mahali fulani wanaosema ndiyo tutakuhamisha na kweli wanawahamisha.

Mheshimiwa Spika, nchi hii inahitaji kuendelea yote, nchi hii inahitaji watumishi waende kote bila kujali wapi kuna maji, wapi hakuna umeme, wapi hakuna barabara ni hapo tu tutaweza kuwa na uongozi bora. Kwa sababu hatimaye uongozi bora ni *even distribution* ya resources yaani ugawaji ambao unalingana kidogo kwa Taifa nzima ikiwepo sehemu moja ambayo ina upendeleo zaidi na sehemu nyingine ya Mkoa ambayo haina upendeleo zaidi, sehemu ile ya Mkoa ambayo haina upendeleo zaidi itazidi kuduma zaidi ili yalingane yaliyoandikwa kwenye Biblia: “Kwamba hata wale wenye kidogo kile kidogo nacho kitaondolewa na kupelekwa sehemu za walionacho zaidi.” (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayasema haya kwa uchungu kidogo. Mkoa wa Lindi haujaendelea, unahitaji watumishi bora siyo bora watumishi, unahitaji watumishi wanaokuja kukaa Lindi siyo kupumzika Lindi, unahitaji watumishi wenye uchungu na maendeleo ya nchi, siyo uchungu wa maendeleo ya kwao, tunahitaji watumishi wanaoitumikia nchi hii bila ubaguzi wa aina yoyote ile, siyo watumishi wanaokuja Lindi kuchumia na kwenda kulia kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mbao na magogo mengi sana yamevunwa Lindi, mbao nyingi sana za mninga mvule na kila kitu baada ya miaka mitano kuanzia sasa Lindi itakuwa jangwa na baadhi ya watumishi wa Mkoa ule wanashiriki katika uvunaji holela wa misitu hiyo na wakishamaliza shughuli hizi hawakai Lindi wanahama na utajiri na fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, unanisikia nazungumza kwa uchungu zaidi. Kwa sababu Lindi ingawa ni fukara ni tajiri tungependa watumishi wawe na nidhamu ya kuja kufanya kazi Mkoa wa Lindi bila kuwa na maslahi binafsi vichwani mwao waitumikie nchi na wafanye kazi Lindi na siyo kupafanya Lindi mahali pa kuchumia baadaye watukimbie asubuhi asubuhi bila sababu zozote zile. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kwa uchungu mkubwa. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri na kuomba kwamba haya niliyoyasema yazingatiwe. Nakushukuru, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi niweze kuchangia katika hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora. Kwanza, kabla sijaenda mbali naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Sina matatizo nayo kwa sababu imekuwa ni hotuba nzuri na inaleta matumaini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ambao wametoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Yete Mwalyego,

ambaye alikuwa ni rafiki yangu sana na tuliishi pamoja lakini Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, niongee tu kwamba wafanyakazi walio wengi wa Serikali hasa Wizara ya Elimu na Utamaduni wanashindwa kwa muda mrefu kwenda likizo. Watumishi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni hawapati likizo wanaopata likizo sasa hivi Serikalini ni watumishi wa ngazi za juu tu ndiyo wanaenda likizo, wanaenda na magari ya mashangingi nyumbani wanapumzika iwe hata Krismas wiki moja lakini hivi tunasahau hizi Wizara zingine.

Mimi ningeomba tu kama atakuwa na takwimu sahihi aelete ni walimu wangapi wanaenda likizo kwao kwa mwaka mmoja. Hata pale pale Jijini Dar es Salaam hawaendi. Huko Kigoma na Lindi ndiyo hawawezi kwenda kabisa anatokaje Lindi kwenda Kilimanjaro, anatokaje Kigoma kwenda Kilimanjaro haiwezekani kwa sababu hawalipwi fedha zao za likizo na wale watoto wa kisheria jambo hili linaonekana linazidi kuachwa tu kila kukicha. Sasa huu Utawala Bora amba unakwenda na mambo mengine ya karne ya 21 mengine yanasa haulika. Hilo ni ngumu naomba sasa hivi alizingatie Mheshimiwa Waziri wa Utumishi.

La pili, labda nijaribu kumwelezea kwamba sasa hivi Utumishi wameua nguvu na juhudzi zinazofanywa na wananchi kwa sababu wamejenga Zahanati kijiji kwa kijiji, shule za msingi kijiji kwa kijiji, Vituo vya Afya kufuatana na utaratibu.

Napenda kuipongeza Wizara ya Afya kwamba imetoa tamko hilo kwamba wajenge lakini kigezo au kikwazo kikubwa ni pale inapoonekana kwamba hakuna wafanyakazi katika Zahanati. Asilimia 75 ya Zahanati zilizopo nchini hazina watumishi. Hivi Serikali imefikia hatua tuliyonayo inashindwa kupata shilingi 70,000=, 70,000/= za mishahara. Yaani unaweza kusema kwamba kwenye zahanati tumekosa watu wa kuwaajiri wakati kuna watu wamesomea uganga wapo wametulia tu.

Sasa matokeo yake wale wataalamu amba wamepata vyeti hivyo wanauza vidonge mitaani. Mimi naiomba Serikali sasa hivi waache wale mara moja kuza vidonge mitaani waende wakaajiriwe kwa sababu wameelimishwa na Taifa na wengine wamejisomesha wao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kipindi kilichopita nilimwandikia Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na yeche mwenyewe anaelewa akanijibu akasema tunaitekeleza. Sasa nimesoma kwenye kitabu chake cha hotuba nione wapi ametekeleza hilo hakuna na mimi nisingesimama kabisa.

Labda Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha hoja yake aniambie kwamba safari hii wanaruhusu waajiri watumishi wa kuweza kumudu kuendesha hizo *dispensary* tangu lini mwanamke mmoja kwenye *dispensary* anakuwa huyo huyo ndiyo anaandika na huyo huyo ndiye Mkunga hiyo kazi inawezakana kwa nani na katika Taifa la nani. Taifa hili la Tanzania!

Mheshimiwa Spika, mimi najua kabisa Mheshimiwa Waziri atakaposimama ataelezea umma wa Watanzania ni pamoja na hili tuondokane nalo kabla hatujaingia kwenye uchaguzi unaokuja kwamba zahanati nilizosimamia mimi nalala huko vijijini, kheri nikija hapa Bungeni kupumzika, halafu naelezea haya nikirudi kule hakuna watumishi. Ziko wapi sababu za msingi nataka kuzielewa. Tena bahati nzuri leo nimekuja na Mheshimiwa Diwani ambaye yupo kwenye Jimbo langu na yeye amehamasisha shughuli hizo lakini hakuna ajira ya watumishi. Namwambia sasa asikilize haya ninayoeleza na yeye mwenyewe awe shahidi wa kuona na Mheshimiwa Waziri atakapojibu na yeye atasikia. Sasa unadhani nitayasema wapi mambo haya. Naomba hili litekelezwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, lingine niseme kuhusu mishahara ya walimu. Hivi huu Utumishi gani kwa nini hizi fedha tusiziweke kabisa zikawa chini ya Afisa Elimu hii ya kuzipitisha kwa Mkurugenzi imeleta kuzorota kwa ufanisi wa kazi. Naomba kwamba hawa walimu wanaokaa vijijini kwa muda mrefu wakienda kwa Mkurugenzi hawatambui, wapelekwe kwa *boss* wao Afisa Elimu. Kama hili halitafanyiwa marekebisho litaendelea kutupunguzia ufanisi wa kazi. Ningombwa hili lijaribu kutazamwa kwa mwenendo mzuri ili hii migogoro iweze kupungua. Ipo migogoro mikubwa kwa sababu utumishi wa watumishi wengi wako huko vijijini tunakokaa, huku miji nyinyi mmeshakuwa *standard* kwamba mambo yenu yanaenda sawa tu mnabebana kikamilifu. Lakini wale wanaokaa vijijini hali zao ni ngumu na maisha yao ni magumu.

Mheshimiwa Spika, sasa lingine ningeomba hivi hatuwezi kufanya kama Mataifa mengine. Huyu mtumishi anayeajiriwa leo tuna matumaini kwamba atalitumikia Taifa hili kwa zaidi ya miaka 20 au 40, vijana wengi wanaanza kazi wakiwa na umri wa miaka 25 kwa hiyo akifanya kazi kwa muda wa miaka 35 au 45 anakuwa amefikisha umri wa miaka 60 ndiyo anaweza kustaafu. Serikali nyingine wanawakopesha watumishi fedha kwa muda wa miaka 20 hata kama wanawakata shilingi 10,000/= kila mwezi, akianzisha hiyo shughuli kwa muda wa miaka 20 anaweza akafanya mambo ya kuweza kumwezesha ndivyo wanavyofanya huko Burundi, Rwanda na Kongo ambazo ni nchi zenye vita vya kudumu lakini watumishi wao wanawathamini. Je, hili nyinyi mnalo au mnalibuni?

Mheshimiwa Spika, sasa uboreshaji wa kusema kwamba mtumishi wa umma tumemwekea miundombinu aweze kuboreka. Sasa ukifutilia hili neno uboreshaji, uboreshaji limeishaanza kuchosha hata kusikia anaboreshwaje huyu mtu. Mboreshe sasa kwa kumpa shilingi milioni 5 kwamba mtamkata kwenye mshahara kwa muda miaka 20 haiwezekani hata ukifanya mahesabu.

Sasa hawa watumishi ni maskini tu. Akipelekwa mwalimu kijijini kule mahali pa kulala hakuna, ile fedha yake shilingi 70,000 ingetosha kumkata shilingi 10,000/= kila mwezi kwa muda wa miaka 20. Nani anatamani kuacha kazi akishapewa hizo fedha katika miaka 20 awe ameacha kazi hayupo hata mmoja. Hata mimi kwenye Ubunge nina miaka 15 ninaendelea na sasa nataka miaka mingine 15 nikifikisha miaka 30 ndiyo nitakuwa nimezeeka angalau kidogo siyo kuzeeka sana. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wapo Waheshimiwa Wabunge wana miaka zaidi ya 30 mbona bado wanaendelea kuwa Wabunge na wamepewa zawadi Mheshimiwa Edgar Maokolo Majogo pale tangu mwaka 1975 ni Mbunge si miaka 30 tayari na bado anaendelea.

Sasa, Je, mtumishi huyu naye si atazamwe. Hili ni wazo lililo nzuri hatuwezi kwenda na hadithi tu, ubora uko wapi sasa. Naomba suala hili sasa litazamwe. Nimesisitiza kwamba Vituo vya Afya na Zahanati vipatiwe watumishi kama inashindakana tunaomba maelezo na nitasimama kuuliza tu hili kwamba je, maelezo yanatosheleza.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, hivi fedha za pensheni za wastaafuli, ukisoma *Hansard* mliahidi kwamba mngekuwa mmewalipa mwezi Januari mwaka huu 2004. Sasa mmepeleka mwezi Januari mwaka kesho 2005 hivi ile tunaifuta hebu turudi kule tutizame kwa sababu hili lilisemwa katika Bajeti ya mwaka jana 2003 kwamba wangeanza kushughulikia mara moja kwa kuanzia mwezi Januari 2005 wapewe mafao ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi kama wanapewa mwaka kesho naomba *arrears* zote za kuanzia mwezi Januari mwaka huu mpaka mwaka kesho siyo tuwalipe kuanzia mwezi Januari, mwaka 2004 hapana na za mwaka wote huu kwa sababu hiyo ni ahadi ya Serikali hakuna Serikali inayojipinda. Hili naliomba sana Mheshimiwa Waziri ajaribu kulifuatilia je, kilichosemwa ni nini?

Katika pensheni naomba hizi shilingi 20,000/= hazina sababu yoyote ni kidogo sana. Yaani tuwe tumewaongezea kwa asilimia nyingine angalau 50. Shilingi 10,000/= pensheni ya sasa tukimlipa mstaafuli aliyetumikia umma wa Tanzania kwa shilingi 30,000 angalau inaleta matumaini. Anaweza akanunua hata kilo 50 ya mchele tu na shilingi 10,000/= akapitia mboga mambo yakawa yameisha. Wala hazizidi hapo. Lakini kama tunaendelea kuwasahau hao watumishi amba wamestaafu hawakupata marupurupu mazuri waliutumikia umma huu wa Tanzania kwa moyo mkunjufu na wana hali mbaya wala hakuna ambaye wamefaulu kujenga hata nyumba nzuri. Sijui waliishia kufanya nini. Lakini walikuwa wanapata mishahara midogo sana. Sasa mimi ningefikiri kwamba hii ndiyo iweze kuwafikiria waweze kumudu maisha angalau anaweza akanunua hata kiatu. Ni aibu kwa mtumishi aliyetumikia Taifa la Tanzania kwa muda mrefu halafu unamkuta anatembea hana hata kiatu. Hivi mimi ninayekuwa nimevaa kiatu mimi ndiyo nasema ndiyo baraka Mwenyezi Mungu ndiyo amenipatia mimi nipate baraka wewe basi ulizaliwa usiwe na baraka, unapata katika sura ya namna gani hiyo? Hawa wapo tunao, ebu tuwakumbuke hawa. Kama haiwezekani ni sababu ya namna gani. Halafu hivi ufanuzi wanalipwa mpaka lini. Hata amba wengine walistaafu wakapewa mkupuo shilingi 200/=, 200/= halafu sasa tunawarudisha. Je, ni mpaka maisha yao kama ana miaka 40 au pensheni ni hii ya miaka 12 basi anaachwa.

Hilo litazamwe. Kwa sababu hata sheria yenyewe ilikuwa inasema miaka 55. Tumeongeza ikawa miaka 60. Kwa hiyo, hata ile pensheni inazidi. Kwa hiyo, iwalipe mpaka waitwe na Mwenyezi Mungu kwa wakati wao. Sio tena kuanza kuwagawia

gawia halafu baadaye kama bado yupo anapumua unampeleka wapi? Huwezi kumgawia mtu halafu unasema tumemaliza. Haya mambo si sahihi. Naomba sasa hivi hii Serikali iwe ya uwazi na inayokwenda vizuri na tunayoipenda. Kwa sababu imeshafanya mambo mengi mazuri tofauti na miaka iliyopita. Hali inapendeza sasa, huko kuzorotazorota tu. Rushwa, rushwa lakini zipungue. Lakini sasa hivi Serikali inaleta matumaini mazuri na watu wanaanza kuifurahia. Sasa jambo lile linaloleta baraka na furaha tuliendeleze. Hii migogoro midogo midogo tu inayohitaji baraka tu za Serikali iliyopo waweze kuishi kwa maisha yanayoleta matumaini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana.
(*Makof*)

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi naungana na wenzangu kuwapa pole ndugu yetu baba yangu Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa kufiwa na kipenzi mtoto wake Vicky. Pia naomba nitoe pole kwa familia ya Mbunge mwenzetu Marehemu Yetet Mwalyego. Mimi nilikuwa naomba ndugu zangu Wabunge, Bunge ni *institution* na Wabunge ni ndani ya *institution* ya Bunge. Ni *culture* ya Watanzania unapofiya kuonyesha kama ulikuwa una duka unafunga ili umalize mazishi. Kwa hiyo, mimi naomba nyakati zingine inapotokea mwenzetu Mbunge anafariki akiwa hapa Bungeni na maiti iko Bungeni si vibaya basi kuonyesha simanzi zetu kwa kusimamisha Bunge na kuhakikisha mpaka anazikwa. Nilikuwa naomba tu wakati mwingine suala kama hili likitokea.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe hongera kaka yangu Ali Mchumo kwa kushinda. Ninaomba nimpe hongera dada yangu Fatma Said Ali, kwa kuambatana naye ili kumpa moyo mpaka amefanikiwa alichofanikiwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo mimi naanza kwanza na kada ya Utumishi. Hapa Bungeni niliinuka kuuliza swali la nyongeza kuzungumzia suala la kada ya wafanyakazi wa afya, Waganga, *Paramedics* pamoja na Manesi. Nikajibiwa hakuna asiyejiriwa. Ni imani yangu Utawala Bora kuliambia Bunge hili sahihi. Ukiidanganya Bunge si Utawala Bora. Mimi nilifuatilia na jana tulikuwa tunawasilisha Wizara ya Afya wataalamu wote walikuweko hapa kwa sababu nilitaka niinuke katika kupidisha kifungu, lakini wakaniambia ni kweli kabisa kwa bahati mbaya halikuzungumzwa na Waziri mhusika. Tunakubali na ni kweli na kuna baadhi ya Manesi tangu miaka ya 1980 wame-*qualify* hawajaajiriwa na wenzangu hapa wote wanakubaliana kuna *shortage* ya wafanyakazi wa afya katika vituo mbalimbali.

Wakati Naibu Waziri Pinda akijibu swali siku ya pili yake akasema amepewa kibali cha kuajiri watu sita. Mimi bahati mbaya tu kama alivyoniambia Spika ni kweli nainuka sana na mimi nakubaliana na wewe na sasa nimepunguza kuinuka kuuliza maswali ya nyongeza. Ni kwamba nilitaka kuuliza kama nafasi hizo ziko kwa nini aweke nafasi sita. Sasa mimi nilikuwa naomba tu ni kweli dada yangu ninakusihi sana wako wafanyakazi wa afya na bahati nzuri Wizara imenithibitishia hivyo. Hilo mimi nilitaka nilizungumze nalilirudia.

Mheshimiwa Spika, narudi kwenye Utawala Bora. Mimi naomba niwapongeze Ofisi ya Rais, Utawala Bora. Imeweza kufanya kazi na *African Parliamentary Network Against Corruption Tanzania Branch* karibu sana pamoja na Wabunge. Hivi sasa unaona Wabunge wanainuka wanazungumzia rushwa ni kwa sababu uliwaelimisha wajibu wao wa kusimamia na kuishauri Serikali. Hii ni kazi wanayofanya baada ya Wizara hii kuwasaidia Wabunge kuelewa majukumu yao katika suala zima la kusimamia na kupambana na rushwa. Kwa hiyo, mimi naomba nimshukuru Waziri na hasa kabisa naomba nitamke nimshukuru Mheshimiwa Hosea, Mayaya, Chitunje. Mara nyingi huwa tunakwenda kwao wanatusaidia. Mimi nasema ninawashukuru sana. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini ni utaratibu mzuri mfanyakazi anapofanya kazi na kuona mshahara wake mdogo ukimpa ruhusa baada ya saa za kazi kufanya kazi nyingine mradi tu hatumii ule muda wa Serikali. Mimi nafikiri ni utaratibu mzuri. Kwa hiyo, mimi nampongeza na natoa kauli yangu nia yangu mimi mwenyewe nampongeza Mheshimiwa Hosea kuwa na kitengo chake kile cha *Advocacy*. Kwa sababu anapofanya *advocacy* yake hatujaambiwa ametumia nafasi ya *advocacy* yake kuidhalilisha *PCB*. Kwa hiyo, mimi naomba nimpongeze. Tukianza kuwaingilia wafanyakazi katika shughuli zao tutakuwa tunawavunja nguvu na sisi tuko hapa kuwasaidia wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo *APNAC Tanzania Branch*. Imeletewa malalamiko mengi sana, imeletewa *documents* nyingi sana, lakini hamjasikia tunazzungumza Bungeni kwa sababu moja tu. Kwa sababu tulikuwa tumekosa Sekretariat ya kutosha, tumekosa *researchers* wa kutusaidia, *ku-research* haya mambo. Maana yake nikiamka hapa nikilipuka hapa sina ushahidi Spika siku moja utaniundia Tume ya Mheshimiwa Simpasa na halafu nitaanza kuingia na matatizo. Kwa hiyo, naomba nitoe taarifa Bungeni sasa hivi karibuni tutasaini *memorandum of understanding with Transparent International* itusaidie katika shughuli zetu. Ninaomba wananchi wasikate tamaa waje tu kwa Wabunge hawa wa *APNAC* na Wabunge wengine kwa kweli suala la rushwa wanalitazama kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa naomba upande wa *PCB*. Ni kweli kabisa tuna-*train s taff* wengi. Naomba tuwape moyo wafanye kazi kwa uhakika na tuwatazame wasitumie ubinafsi katika kunyanyasa watu katika kutoa ripoti zao. Itawavunja nguvu na itakuwa *PCB* itakuwa haithaminiki kwa wananchi. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba tuwatazame na hasa inapofikia wanasiisa wanawatumia wafanyakazi hawa ili waandike ripoti inayowfurahisha wao na kumkandamiza mtu. Naomba hiyo muitazame kwa sababu inataka kujitokeza. Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba wasaidieni wafanyakazi hao. Lakini wanafanya kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba na tulishatoa mapendekezo yetu na tutorudia tena sisi kama *APNAC* tunasema tutalichukua tuje kuliomba Bunge ikiwezekana basi ripoti ya *PCB* pia itolewe Bungeni ili haya malalamiko mengi sijui kuna rushwa, kuna nini yaish. Ikiletwa *PCB* ripoti Bungeni sio lazima iwe *tabled* Bunge zima. Aah!!! hapana. Kuwe na Kamati maalum kama vile Kamati ya Simpasa inatazama ripoti ya *PCB* ili tuweze kufutilia. Hii inaonekana ngumu na inapingwa vikali lakini mimi

naomba niwashauri na ndio Utawala Bora, ndio Bunge kulisimamia na kuishauri Serikali. Nilikuwa naomba hii ripoti iwe inaletwa Bungeni na inashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini bado nakubali *DPP* ushauri wake wa kwamba tukiiachia hiki chombo kiwe *independent* kinaweza kunyanyasa watu. Lakini bado kwa upande mwingine hata Idara ya *DPP* pia inaweza kutumia vibaya nafasi yake kukidhalilisha hiki chombo. Kwa hivyo mimi nasema ikifika mahali *DPP* na *PCB* mnabishana jinsi ya kupeleka kesi fulani Mahakamani basi iletwe Bungeni ili tuone nani *PCB* anataka kumnyanyasa mtu au *DPP* anataka kumlinda mtu. Lakini bila ya kufanya hivyo itakuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Spika, naomba niiambie Serikali imejitahidi sana katika suala zima la kupambana na rushwa. Imejitahidi hatutegemei rushwa kwa siku moja ikaisha. Tunasifiwa sana sasa hivi sio kama zamani mtu anadai rushwa kama haki. Sasa hivi mtu akitaka kupata rushwa anakwenda kifichoni. Zamani mtu usipotoa rushwa unasema mmh!! hii huduma niliyopewa ni sahihi hii ni ya uongo. Kwa hiyo, kutoa rushwa ulikuwa unaamini kabisa ndio unapata huduma. Lakini sasa wananchi wameelewa na wanalamika wazi wakidaiwa rushwa. Kwa hiyo, mimi naomba niipongeze.

Lakini naomba kwa upande mwingine Idara hii ikubaliane na malalamiko ya watu wengi wanaonekana wengi kwenda Mahakamani, wanaonekana wengi kukamatwa ni *petty corruption, grand corruption* bado. Mimi naomba niizungumze hii inazungumzwa hata nje kama *Tanzania Grand Corruption* bado. Inawezekana ipo lakini kwa sababu ya kuficha ficha vitu fulani *procurement*, mikataba hii ya kutumia fedha nyingi hajji Bungeni labda wananchi hawaijui ndiyo maana wanasema. Sasa mimi naomba tuweke uwazi na uwazi ni kwamba kuiomba *PCB* itakapofanya utaffiti wake na kuona kweli kuna rushwa katika sehemu fulani ilette Bungeni. Hawa ndio wasemaji wa wananchi tukikataa inasemekana *Tanzania Institutional set up* ya Tanzania inailinda *Grand Corruption*. Sasa mimi naomba tusionekane kwa dhana tu. Naomba tufanye vitu ambavyo wenzetu wanaamini na sisi tunaamini vitasaidia rushwa kuondokana na hasa *grands*.

Tumeshaletewa ripoti nyingi na bahati nzuri Waziri mimi niko pamoja na wewe kila nikipata nakuletea. Nimesema hivi sintoamua kuinuka hapa kuropoka mpaka nifanye *research* na sasa hivi tumepata Sekretariet *research* yetu tutakuwa tunakuletea. Mwisho tumeamua kabisa ikishindikana kabisa husikii Waziri wakati tumefanya *research* tutamwendea Rais, tumeamua hivyo. Kwa hiyo, nilipoinuka wengi wanasema eeh Mama Gama ameinuka aah sina kitu *specific*. Nitakitoa wakati nina ushahidi. Hilo mimi nilikuwa nataka kulizungumzia.

Mheshimiwa Spika, nawaomba *PCB* mwakani ni mwaka mzito sana wa uchaguzi na uchaguzi wa mwakani ni wa kumchagua Rais. Rais atakayeingia madarakani kwa njia ya rushwa na ninyi mtakuwa-*disappointed* hamtafanya kazi. Kaka yangu Mheshimiwa Masilingi kitengo chako kitaondolewa. Kwa hiyo, mimi ninaomba sasa hivi *PCB* ifanye kazi kutazama hawa wanaopitapita na rushwa, rushwa na kadhalika wako. Mimi ninaomba *PCB* ifanye kazi na itoe ripoti. Kama inahu Vyama, vyama basi itoe ripoti

kwenye vyama husika. Ama sivyo ninyi mtakuwa hamna kazi, Masilingi atakuwa hana kazi na Bunge litakuwa *chaos*. Mimi hilo ninaliomba sana, lakini naendelea.

Leo asubuhi wakati likijibiwa suala la Wizara ya Mambo ya Ndani lilizungumziwa suala la watu kuchukua madaraka mikononi mwao. Waziri naomba nikwambie historia huijui. Ilianzia Dar es Salaam watu kutokuridhika hawa watuhumiwa hukumu zinavyotokea Mahakamani. Matokeo yake wakirudi wanasema eeh tutawaonyesha, wanawanyanya watu na wengine walikuwa wanapigwa wanaauawa. Sasa matokeo yake wakaamua wananchi kuchukua madaraka mikononi mwao. Mwanzo ilianzia hivyo sasa hivi watu wanaona kupiga kuua ni kitu cha kawaida. Kesho vijana wetu hawa tumewafundisha tunataka wakidanganywa na vyama vya ajabu kwenye uchaguzi watashika bunduki kutuua maana yake wataona mauaji na hilo ndilo liliwu tatzizo. Kwa hiyo, sasa hivi *integrity* ya Mahakama ni *questionable*. Naomba usiikatae Mheshimiwa Waziri, naomba isikatae Serikali ifanyieni kazi. (*Makofî*)

Unaweka *advocates unless* una pesa nyingi. Kama huna fedha nyingi unaweka *advocate, advocate* atakwenda *the other side* atakwenda akachukue fedha akukandamize wewe. Mahakama mimi nimeshakwambia Waziri nina ushahidi hata kesi ambayo sikukamatwa lakini *ruling* inaonyesha kabisa hapo kulikuwa na rushwa. Haiwezekani mtu anasema *after my deuces* wewe unasema *this is a presents*. Haiwezekani halafu *una-conclude*. Sasa mimi nasema Mahakama itaifikisha wananchi waanze kufanya mambo ya ajabu.

Sasa hivi mnasikia hivyo mzee wangu amelia hapo, uchunguzi umefanyika watu wanashindwa kuogopa kwenda watamwagiwa tindikali. Mnamkumbuka Mbunge moja alimwagiwa tindikali hapo. Sasa mimi naomba kaka yangu Mheshimiwa Masilingi unafanya kazi nzuri naomba uifanye kwa haki yote. Mimi sikubaliani kwa neno linalosema hivi “Kutokujua sheria si kinga. Si kweli. Watanzania tunapitisha sheria kwa kiingereza hapo. Mtanzania kule anajua hicho kiingereza ukimpelekea hiyo sheria. Tunamaliza Watanzania wangapi wanafuata hizo sheria.

Kwa hiyo, ukimwambia si kinga unamwonea. Umem-dený kujua hiyo sheria halafu Mahakamani unamwambia si kinga kutokuja. Mimi nafikiri *it is the right time* sasa hii tuiondoe mpaka hapo Mtanzania atakapopata nafasi ya kujua sheria inayomhusu yeeye *otherwise* tunawanyanya. (*Makofî*)

Mwisho kabisa mimi naomba Serikali inapotoa ahadi ndani ya Bunge na kwa bahati mbaya. Nasema kwa bahati mbaya na sababu kuu za msingi kabisa ikakosa kutekelezeka hii ahadi naomba itoe tamko kuliko mtu anauliza swali lingine anasema mbona mwaka jana ulisema mtafanya, mwaka huu unasema hatuna fedha. Wakati ulikuwa wewe unatamka tarehe fulani nitafanya ulikuwa unajua kama fedha utazipata wapi. Sasa ni wakati muafaka Serikali inavyofikia *stage* kwamba kweli imeshindikana kwa nia nzuri wanayotaka kufanya watoe tamko na wajitahidi sana kaka zangu kule mbele hata mnapowajibu Wabunge inawezekana. Ahsante sana, naomba kuunga mkono. (*Makofî*)

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Wizara hii muhimu kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono asilimia mia kwa mia. Kwa bahati nzuri taarifa nyingi za Wizara hii huwa tunaipata kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama. Tunampongeza sana Ndugu Mheshimiwa Masilingi na Mheshimiwa Nagu nafikiri hakuna siri tunamwona anavyojibu masuala. Alivyosimamia Utumishi wa nchi hii na hata ule utaratibu wa kuzungumzia kwenye vyombo vya habari ambapo wanavyojibu masuala kwa kweli inaonyesha matumaini kwa Watanzania. Kwa hivyo, naunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia nataka nitoe pole kwa Mheshimiwa Rais kwa matatizo yake ambayo yanamkabili pamoja na operesheni ya juzi ya pili aliyoifanya na namtakia mafanikio Mwenyezi Mungu amjalie afya njema na maisha mrefu yeze na familia yake na wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nataka niipongeze Serikali na kuiambia naiunga mkono taarifa iliyotoa juu ya moto wa Ikulu. Bahati nzuri kama Kamati tulifanya ziara na tuliona kile chanzo cha moto na maeneo yaliyosambaa na ilivyokuwa. Lakini vile vile ningeiomba Serikali iangalie utaratibu wa kujenga mazingira mazuri ambayo hali kama ile kama itatokea wataweza kuikabili vizuri sana. Sisi kama Kamati tulimwuliza Waziri kumekuwa na operesheni gani kama Mheshimiwa Rais angelikuwemo mle katika kumwokoa. Kwa hivyo suala kama hili tuangalie *weakness* zile ndogo ndogo ambazo zinaweza kuleta athari kwa maeneo kama yale tuweze kuziboresha.

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchaguliwa katika ile *Commission* ya Afrika na Waziri Mkuu wa Uingereza. Mungu ambariki amfanyie maarifa mazuri katika kusimamia masuala na majukumu yale mazito. Dunia imeenea uwezo wa Tanzania. Kioo kikubwa kuwa ni Rais wetu anawarithisha na Watanzania wengine wote. Kwa hivyo ni matumaini yetu kwamba wakubwa wa dunia watamwunga mkono yeze pamoja na Taifa zima la Tanzania ili kufikia maendeleo ambayo tuliyokusudia.

Mheshimiwa Spika, mimi nikianza kuchangia hotuba hii ya Utawala Bora. Kwa kweli tunazungumzia suala ambalo ni muhimu kwa Taifa letu. Mara nyingi tunazungumza kwamba suala la Utawala Bora ni suala pana sana. Lakini vile vite kuna mambo mawili muhimu sana lazima haya Serikali iyape kipaumbele sana kwa faida ya Taifa hili. Jambo la kwanza ni Umoja wa Kitaifa. Huwezi kuzungumzia Utawala Bora kama Taifa halina umoja. Lingine la pili ni usalama wa nchi.

Kwa hivyo masuala haya mawili yawe ni vigezo kwetu sote Watanzania tukiwemo viongozi waliomo Serikalini wa vyama vinavyoendeshwa na wananchi wa kawaada ili kuleta maendeleo yaliyokusudia Taifa hili. Naiomba Wizara hii, Serikali Kuu na wananchi wote wa Tanzania tuone masuala mawili ni muhimu sana ili wananchi waweze kupatiwa haki na kufikia katika maendeleo walijotarajia.

Mheshimiwa Spika, zimeelezwa hizi kazi za Utawala Bora na wakagusia masuala ya rushwa. Hili ni suala kwa kweli limekuwa ni kero kubwa kwa wananchi. Lakini mimi halinisumbui kwa sababu Serikali imetoa maelezo mara nyingi sana katika kupambana na suala hilo. Lakini lingine nnikukuu maoni ya Kamati ya Sheria ambayo imezungumzia katika ukurasa wao wa 5 ambayo inasema “Vita dhidi ya rushwa”. Kesi nyingi za rushwa zinafungwa kutokana na kukosekana ushahidi kwa nini? Watu wetu hawana uwezo.

Kwa hiyo, hili ningeitaka Serikali ili kujenga imani kwa wananchi *statement* hii isitumike. Kwa sababu wanatuomba fedha tukiamini kwamba wanawa-*train* watu wetu kuwa na uwezo kupambana na masuala kama haya. Sasa leo kama kwenye Kamati tunapata taarifa kama hizi kwamba kuna kesi nyingi zinafutwa tutaamini nini katika karne hii ambayo imejaa uhalifu wa kila aina. Nilitaka Mheshimiwa Waziri na watendaji wote wa Serikali wakaliona hili.

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia Utawala Bora. Kuna mambo mawili au matatu nataka niiombe sana Serikali. Sina uhakika lakini naamini kutakuwa kuna wahalifu wamefungwa Magerezani kwa kushindwa kulipa kodi pengine katika miaka ya nyuma. Sasa hivi Serikali kuna kodi nyingi zimefuta. Kwa hiyo, ningeomba Serikali ifanye survey iangalie kama kweli wako watu katika Magereza yetu waweze kuwatoa mara moja. Kwa sababu Serikali kodi nyingi sana imezfuta.

Lakini la pili ni juu ya wafungwa watoto na vijana kuchanganywa na watu wazima. Kwa mujibu wa kanuni na sheria za Kimataifa ni kosa. Kwa hivyo Serikali ilifanya utaratibu wa haraka sana kuwaondoa watoto hao katika Magereza wale wanaofungwa na watu wazima. Vile vile wawekwe maeneo ambayo watapata elimu. Hawa ni wengi hatuwezi kuwaacha wakakosa elimu. Wawekwe katika maeneo ambayo watapatiwa elimu ili na wao baadaye wakitoka waje waendane pamoja na Watanzania wenzao katika kujenga uchumi na maisha ya Taifa hili.

Lingine ni juu ya athari au kasoro zilizomo kwa Mahakimu wetu. Imeonekana kuna baadhi ya Mahakimu wanahudumia karibu Wilaya nne. Watu wanakaa ndani kwa muda mrefu sana wakisubiri haki hiyo. Kwa hiyo, hili liangaliwe kwa haraka na limalizwe matatizo yake. Kwa kweli inatisha kuja kuambiwa kwamba kuna watu wengi wako ndani. Tukiangalia wanashubiri hukumu si makosa yao. Kama ikiwa Mahakimu hawapo watu wale waachiliwe waende na shughuli zao ili kuleta haki na waweze kuishi kwa usalama kabisa bila hofu yoyote.

Lingine ambalo nataka nilizungumze kwa kweli naipongeza sana Serikali katika taarifa hii kuweka huu Mfuko wa TASAF. Nataka niinukuu kwa dhati kabisa. Inasema *TASAF* ilianzishwa kama mradi shirikishi wa kujenga uwezo wa wananchi kujitegemea na kama mkakati wa kuondoa umaskini. Naipongeza sana Serikali. Kila mtu ni shahidi kwamba *TASAF* imetoa mchango huo katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya maji katika barabara, afya na elimu. Hata sisi kule Pemba tumefaidika na mfuko huu wa *TASAF*. Kwa kweli nataka niitumie nafasi hii kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Kwanza hapa imedhihirisha kwamba Pemba ni sehemu ya

Tanzania. Kwa sababu mfuko wa *TASAF* umefanya kazi katika maeneo haya na faida imeonekana.

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa kunukuu Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi katika kitabu chake cha nyongeza. Ameelezea juu ya miradi ya ujenzi ambayo imesaidiwa kule Zanzibar. Kuna dola milioni 23.376 ambazo zinajenga kule barabara na mambo mengine. Zile barabara zote ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri kwa kule Pemba nataka nilithibitishie Bungeni kwamba kweli barabara zile zipo toka Mkoani mpaka Mto wa Riwa, Mto wa Riwa mpaka Chakechake na kutoa kile kiungo cha pale mpaka *Airport*. Ni thabiti kwamba barabara zile ziko Pemba na zinafanyiwa kazi. Tunaipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, lingine sitaacha kumshukuru Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kweli Rais Karume amefanya mambo mengi na ya kiutu na ya kimaendeleo katika kisiwa cha Pemba. Nataka nikiri kwa dhati kabisa.

Pemba ambayo iko chini ya utawala wake kwa miaka mitatu na miezi tisa imebadilika sana. Kwa hiyo ni matumaini yetu kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itaweza kumpa ushirikiano na misaada mikubwa Rais Karume aweze kutekeleza yale ambayo ameyapanga kwa maendeleo ya watu wa Zanzibar na Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka nilizungumze ni juu ya hii Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ambayo iko ukurasa wa 24. Mheshimiwa Waziri amesema katika mwaka wa fedha 2004/2005 tutaendelea na utekelezaji wa awamu ya pili ya mpango wa kuboresha utekelezaji katika kazi ya Utumishi wa Umma ulioanza mwaka 2000. Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana.

Lakini pamoja na mpango huu wote tungelikuomba yale maoni yote ya Waheshimiwa Wabunge waliyyoyatoa kuhusu suala la matatizo katika Idara ya Utumishi uyashughulikie kwa nguvu zako zote. Serikali ikuunge mkono na hasa suala zima la matatizo na migogoro ya mishahara ya Walimu pamoja na posho zao. Nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa ufanuzi na maelezo sahihi. Namtakia mafanikio katika kulismamia suala hili.

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa dhati kabisa. Huwezi kuzungumzia maendeleo ya nchi kama hujagusa maeneo mawili muhimu sana Walimu na Waandishi wa Habari. Hizi ni nyenzo muhimu kwa Taifa letu duniani. Sote sisi tumepitia shule Walimu ndio waliotujenga mpaka tukafikia hapa tulipofikia.

Ninaamini kama nisingelipita shule nisingelikuwa na uwezo wa kuongea kitu hiki ambacho naongea, wala nisingekuwa na uwezo wa kupanga hivi nilivyopanga. Hata Rais kama asingelipitia shule ninaamini kwamba asingeliweza kuliongoza Taifa hili. *It means* alianzia kwa Mwalimu Kijijini huko mpaka alipofikia. Kwa hiyo, lazima Mwalimu ni mzazi na ni lazima tuthamini wazazi wetu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio makubwa ya Rais wetu mimi nakwambia hakuna siri nyingine isipokuwa nidhamu yake kubwa sana. Kitendo chake cha kumhudumia, kumtibu na kumzika kwa heshima zote Baba wa Taifa ndicho kilichomwongoza hakuna kingine. Hakuna lingine. Rais tumeona juhudhi yake alivyomuuguza Marehemu Baba wa Taifa, mpaka kumzika kwa heshima zote.

Vile vile lazima tuwaheshimu Walimu. Tutafuteni fedha popote kama hatuna kwa kweli Serikali yetu ina ushirikiano mkubwa na Mataifa yote makubwa ya nchi. Mashirika mbalimbali yatusaidie fedha tusaidie Walimu wetu hawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo ningeliomba Serikali kwa hili isilikalie kimya. Kauli ya Waziri Mkuu, kauli ya Wabunge, maelekezo ya Wabunge tulisimamie kwa nguvu zote. Tunataka kikao cha Novemba tuambiwe ni fedha ngapi Serikali ili kutatua matatizo ya Walimu. Lingine ambalo nataka nilizungumze tunafanya makosa katika nchi yetu tunapolinganisha maendeleo yetu kutaka kuyaweka kama maendeleo ya Marekani.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni walisherehekea uhuru wao kutimiza miaka 228. Na kwa mujibu wa taarifa inatuambia Marekani ilipata uhuru tarehe 4 mwaka 1776. Tuangalieni hizi *difference* kubwa iliyopo. Kwa bahati Marekani tarehe 2 Julai, walipitisha sheria ya kutetea haki za raia ikiwemo kupinga ukabila, rangi, kidini na kitaifa, mwaka 1964. Sisi mwaka 1964 tunaungana wako kwa miaka mingapi.

Kwa hiyo, inaonekana hawakuja tuko pale. Tuwatake wasomi wa nchi hii, viongozi wa Vyama vya Siasa na Watanzania wote miaka 40 tuliyofikia hapa hatukufika tu ovyo ovyo. Watu wamefanya kazi watupe tena miaka 40 waje watuambie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi huwa nashangaa sana kuona wasomi wanalinganisha Taifa letu na Taifa lingine lolote. Tuko na miaka 40 wakati Amerika iko tangu mwaka 1776. Tunaambiwa kwamba migogoro inatokea tusishangae. Kwa sababu kunako tarehe 2 Julai, Marekani ilivunja uhusiano na Uingereza.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1776 Julai, jamani Watanzania tuliangalieni hili. Twendeni na historia, jiografia na taratibu na mila zetu. Nazungumza kwa uchungu tunashangaa sisi ambao hatuna elimu tunayaona haya na kuna watu wenye elimu wanawadanganya wale. (*Makofi*)

Ndiyo!! Professa Lipumba alikuwa mshauri wa mambo ya uchumi wa Rais anawaambia nini wananchi wa Tanzania. Sisi kama Zanzibar anatuambia nini. Kama alikuwa anamshauri Rais Alli Hassan Mwinyi na Zanzibar tunasema amemsaidia nini, amekuja kumpa kazi Rais Karume leo, mtuambie na msitugombanishe. Juzi akihutubia Zanzibar, nimekuta anasema kwamba huku Zanzibar kuna mafuta mengi, ukanda huu una mafuta mengi sana, anatuambia leo. Sisi tunajua kama mafuta yapo.

Kwa mujibu wa gazeti la Uhuru la mwaka jana 2003 la mwezi kama huu kwenye Bajeti ya Zanzibar, nilikuta kwenye gazeti la uhuru ukurasa nimeusahau. Inasema kwa mujibu wa taarifa za wataalamu mbalimbali nchini tuna mafuta ambayo kama tunaweza

kuyachimba yanatosheleza kwa matumizi ya ndani ya nchi na mengine kuuza nje ya nchi. Ikaainisha kwamba kwa sehemu ya Pemba yako Vitongoji kama ni kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa Unguja yako *Ras* ya Chwaka. Tunawaomba wataalamu taarifa hizi tuziweke wazi Watanzania wajue. Watu wamekosa sera hawa. Sasa wanagusia kwamba Zanzibar kuna mafuta leo na mimi naipongeza Serikali ya Zanzibar sasa hivi kuunda Tume ambayo itashughulika masuala ya mafuta. Naipongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namalizia kumwunga mkono sana Mheshimiwa Waziri Masilingi, Waziri Nagu na Serikali kwa ujumla. Namtakia mafanikio Mheshimiwa Rais katika kusimamia Taifa hili na twende kwenye uchaguzi mwaka 2005 kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DR. ZAINAB A. GAMA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Utumishi Mheshimiwa Dr. Mary Nagu akijibu suala la nyongeza kuhusu wataalam wa Afya kwa mfano *Clinical Officers*, Manesi kutoajiriwa na hivi sasa wako wengi, alijibu si kweli, Utumishi iko tayari kama wapo waambiwe ili waombe na watapatiwa kazi. Nilipozungumza na wataalam wa Wizara ya Afya walipokuja wakati wakiwakilisha Bajeti ya Wizara ya Afya, walithibitisha kuwa ni kweli kada hizo wapo wengi wasioajiriwa.

Naomba Mheshimiwa Waziri sasa akae na Mawaziri wenzake wa Wizara ya Afya ili kutatua suala hili na kama kweli ajira kwa kada hii ipo kwa nini vibali vitolewe kwa watu wachache? Kwa nini sasa Wizara isitoe kibali bila kiwango, mradi tu ikama ya Wizara ya Afya imefikiwa kutokana na hospitali, vituo vyta afya na zahanti zilizopo za Serikali? Kama hatatoa kibali cha kuruhusu Wizara ya Afya na Halmashauri kujaza upungufu uliopo, haoni jibu lake Bungeni si sahihi?

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu Serikali inasikiliza maoni ya wadau wake kwa mfano, wananchi na mashirika ya ndani na Kimataifa. Hivi sasa kuna imani kwamba Tanzania imejitahidi sana kupambana na rushwa. Hivi sasa rushwa ndogo imeanza kutoweka, zamani rushwa ndogo watu wengi waliamini ni haki kuipata na usipoipata unaidai waziwazi na usipoiomba unayempa huduma anaamini kwamba huduma utakayompa si sahihi. Mtu kuomba rushwa hivi sasa watu wanaiomba kwa wasiwasi au kwa uwoga au kwa siri sana. Lakini rushwa kubwa bado ipo na bado haijapungua na inaaminika inazidi hasa kwenye *procurement*. Watu wanasema rushwa zinazopelekwa Mahakamani ni zile rushwa ndogo ndogo, hawaoni rushwa kubwa kupelekwa Mahakamani. Imani hii Serikali isiipinge wala isiipuuze.

Naomba Serikali iifanyie mikakati rushwa kubwa, tukiendelea kudharau muono huu wa watu, inaweza kutuletea madhara. Kwa mfano, watu walikuwa wanailalamikia Mahakama juu ya hukumu ya wahalifu. Kwa kuwa Serikali haikuchukulia suala hili *seriously*, hivi sasa watu wanachukua sheria mikononi mwao. Kwa hiyo, malalamiko ya watu juu ya rushwa kubwa ikidharauliwa na kuachwa, watu watachukuwa sheria mkononi. Naomba Ofisi ya Rais, Utawala Bora ilichukulie suala hili *seriously*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Spika, nami naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu kwa njia ya maandishi. Kwanza nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Mheshimiwa Wilson Masilingi (Utawala Bora) kwa jitihada zao za utekelezaji wa shughuli za Serikali za kila siku.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni upande wa utawala bora hususan rushwa. Katika kipindi cha fedha kinachomalizika hivi sasa 2003/2004, nilitoa taarifa katika Taasisi ya Kuzuia Rushwa Mkoa wa Mara kuhusu fedha za *fumigation* katika Shule za Sekondari Tarime, Musoma Ufundu na Mara, kiasi cha shilingi milioni 54. Nina hakika hatua mbalimbali zitakuwa zimechukuliwa kufuatilia tatizo hili kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni.

Mheshimiwa Spika, nikiwa mwakilishi ambaye nililetewa malalamiko hayo na wananchi, nimekosa taarifa toka Mkoani. Suala hili nilimdokezea Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Utawala Bora na akachukua hatua, hata hivyo sijapewa taarifa ya nini kinachoendelea. Ningependa kupata maelezo ili nifahamu hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nipewe maelezo wakati Waziri akifanya majumuisho ya hoja yake.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, nampongeza mtoa hoja Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, ametumia ufundu na uzoefu katika kuwasilisha Bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, ninayo yafuatayo katika hoja husika kama ifuatavyo:-

Kwanza, napongeza kwa kazi nzuri inayofanywa na *TASAF*, imetoa mchango mzuri katika Jimbo la Muleba Kaskazini. Mchango mkubwa wa *TASAF* umewezesha Jimbo kuongeza idadi ya shule za sekondari, barabara, shule za msingi na zahanati. Nashauri katika awamu ijayo kuondoa matatizo yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya watu wenye tabia ya kulaghai wananchi kwamba *TASAF* inagharimia kila kitu, kwa hiyo, wananchi hawapaswi kuchangia. Ulaghai huu unachelewesha maendeleo na mafanikio ya *TASAF*.

Pili, naipongeza Serikali kwa kuwarudisha wastaafu katika malipo ila wale waliokua chini ya *PPF* hawajafikiriwa. Menejimenti ya Utumishi wa Umma iliangalie hilo.

Mheshimiwa Spika, aidha, nashauri kima cha chini cha pensheni kwa wastaafu kifikiriwe kiwe kima cha chini cha wakati wote kwa sababu kustaifu kazi si kuacha kuishi. Mstaifu awezeshe kumudu maisha ya kawaifa. Mstaifu kwa kima cha chini cha mshahara atapata huduma za kiwango cha chini naye ataendelea kuishi kuliko kiasi cha shilingi 20,000/= ambacho hutegemea kubadilika pale kinapolalamikiwa.

Mheshimiwa Spika, nashauri ramani ya *gate* kubwa pale Ikulu iangaliwe upya. Ukaguzi wa pale uongezeke kwa kuwekewa mitambo maalum badala ya ukaguzi wa sasa. Ulinzi uimarishwe na uanzie pale pale mlangoni. Ingefaa pia ukawepo ukaguzi mwingine kabla ya kuingia katika Ofisi husika. Hali ilivyo sasa siku moja inaweza kuzua tafrani, Mungu apishie mbali. Hata hivyo kinga ni bora kuliko tiba.

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kuhusu juhudzi za kuziba mianya ya rushwa. Pamoja na juhudzi kubwa zinazofanywa, rushwa ya uchaguzi inaota mizizi na huku inapigwa kisogo na masikio yenye pamba. Kwa kuwa uchaguzi wa viongozi ni mwanzo wa maandalizi ya viongozi wa nchi kupitia chama chochote, ni vema rushwa katika uchaguzi ikadhibitiwa mapema, vinginevyo tutaongozwa na viongozi watoa rushwa. Viongozi wakipatikana kwa rushwa, hatari yake itakuwa kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, liko jambo moja ambalo linaokena ni ukarimu, lakini ukweli wenyewe ni mkakati mbovu wa kujijengea umaarufu na kujipatia haki asiyostahili mhusika. Ukarimu huu ni maarufu kwa jina la takrima. Ukweli wenyewe kwa imani yangu, takrima wakati wa kampeni au karibu na kampeni za uchaguzi ni rushwa iliyopewa jina zuri. Nashauri suala hili liangaliwe upya na wataalam wa masuala haya watoe maoni yao wakitazama hatma ya uaminifu, uadilifu, haki na wajibu kwa Taifa letu. Takrima wakati wa uchaguzi iachwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. SALIM OMAR ALI: Mheshimiwa Spika, mimi nachukua fursa hii kusema kwamba sina pingamizi na hotuba hii hata kidogo ila kuna mambo ambayo yanahitaji kuboreshwa. Kwa mfano, kuungua kwa nyumba ya Rais ni udhaifu mkubwa ambaeo umetoa historia ya kukumbukwa kwa Taifa letu. Tunaelewa waziwazi kuwa moto ni rafiki wa mwanadamu ikiwa utautumia ipasavyo ila pia moto ni adui wa mwanadamu unapotumika isivyopaswa. Kama ilivyokuwa Rais ni Mkuu wa nchi. Kwa hiyo, tuheshimu jambo hilo kuwa Rais alipo pawe na usalama wa kutosha.

Kwa hiyo basi, ni kwa nini jengo la Rais (Makazi ya Rais) yaweze kuteketeta kwa shoti ya umeme na kuteketeza vyote ambavyo vilikuwemo katika nyumba ya Rais wetu? Jambo hili ni aibu kutokea tena na tunaomba lisitokee tena. Je, ni namna gani tumejizatiti na jambo hilo?

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya ukarabati ambayo inahusu ujenzi wa nyumba ya mapokezi pamoja na kuweka vifaa na zana za kisasa jengo la Polisi na sehemu za kuegeshea magari inategemewa kukamilika mwezi Desemba, 2004. Sehemu hii ni muhimu sana kufanyiwa ukarabati kwa umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema ukarabati huo unategemewa kukamilika Desemba, 2005. Kusema hivyo haitii moyo sana na sasa napendekeza iwe Desemba, 2004 ukarabati huo uwe umekamilika.

Mheshimiwa Spika, rushwa ni adui wa haki, rushwa ni sawa au zaidi ya ugonjwa wa *Ebola*, kwa hiyo, ni jukumu la kila mtu kusimamia kupiga vita rushwa. Leo haieleweki haki ni ipi na batili ni ipi. Kwa njia hiyo, hatutafika au tutafika lakini siyo salama kama tunavyotarajia kufika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri wangu dhidi ya wala rushwa ambao wanaweza kuiondoa nchi katika ramani ya uaminifu. Ushauri wangu tuwe na mpango maalum wa kuwataja wala rushwa kwa kupiga simu na mpiga simu hiyo alipwe gharama ya matumizi hayo na mpiga simu asitajwe na pili, ufuatiliaji uwepo kikamilifu ili ukweli wenyewe uonekane.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili la Bajeti la 2003/2004, tulisikia Mheshimiwa Mbunge akichangia akisema amewataja wala rushwa na bado hakuna ufuatiliaji wowote.

Mheshimiwa Spika, kanuni zetu za Bunge zinataka Mbunge akiongea Bungeni aseme lile ambalo ana uhakika nalo na Mheshimiwa Mbunge ameshataja na kulitangazia Bunge. Je, ushahidi huo hautoshelezi au ni ushahidi gani na wa nani gani unaweza kuwa ushahidi wa kutosheleza?

Mheshimiwa Spika, bado tunayo kazi kubwa kuweza kuzuia rushwa hasa wala rushwa wakubwa. Wala rushwa wapo nchini na tunakula nao chakula na tunatembea nao lakini kuwashika ni shida, sijui ni kwa nini, ni cheo, kabilia, dini au rangi? Sijui ni lipi kati ya hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ahsante sana Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Zanzibar, Wabariki Wazanzibari, Mungu ibariki Afrika na wabariki Waafrika.

MHE. FRANK M. MUSSATI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja moja kwa moja. Aidha, nawapongeza Mawaziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Mheshimiwa Wilson Masilingi, Makatibu Wakuu na watumishi wote wa Wizara hizi mbili kwa kufanya kazi nzuri katika mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *PCB* kwa kuweza kufungua ofisi katika Makao Makuu ya Wilaya nyingi nchini kote na hasa Mjini Kasulu pamoja na kwamba ofisi hizi zina watumishi wachache, naomba wasikae tu maofisini kusubiri malalamiko na kwenda

kufungua na kuendesha kesi Mahakamani, wazunguke Vijijini kuwaelimisha wananchi vita dhidi ya rushwa. Elimu inayotolewa sasa hivi haitoshi na inatakiwa ipewe msukumo mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TASAF* kwa kazi nzuri waliyofanya katika Jimbo langu la Kasulu Mashariki tangu ilipoanza kazi. Nawatakia kila la kheri ili wafanye vizuri zaidi awamu ya pili itakapoanza Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na timu yake kwa hotuba nzuri ya Bajeti yake. Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi ameitoa hotuba hiyo kwa umahiri wa hali ya juu sana kama kawaida yake. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwenye suala la taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU). Hamasa ya kuchangia hili suala imetokana na hotuba ya Bajeti katika ukurasa wa tisa, *bullet* ya kwanza, ya pili na ya nne, *dash* zote hususan zinazozungumzia taasisi za elimu (Mzumbe).

Mheshimiwa Spika, kwenye *bullet* ya kwanza, ukurasa wa tisa kuna taarifa kwamba TAKURU iliokoa shilingi milioni 557. Hii inaonyesha kazi nzuri. Lakini takwimu hii peke yake haitoshi kuonyesha faida za TAKURU japo si zote zinaweza kupimika kwa vigezo vya kifedha. Lakini pia, ingefaa kufahamu ni kiasi gani cha gharama ya matumizi ya fedha kilitumika kwa muda unaolingana na muda uliotumika kuokoa hiyo shilingi milioni 557. Je, dhana ya gharama za matumizi zipo kwenye TAKURU na kama ndivyo, takwimu na mfumo wa kuweka hizo takwimu upo na unawezesha mlingano wa yanayookolewa na TAKURU?

Mheshimiwa Spika, *bullet* ya pili, ukurasa wa tisa na ya nne ukurasa wa kumi, zinazungumzia upanuzi wa TAKURU kwenye Wilaya zote na sehemu teule (Chuo Kikuu cha Mzumbe, Leseni za Biashara Dar es Salaam). Huu upanuzi wa TAKURU unaogopesha na sijui unalenga nini? Kilicho na uhakika ni kwamba tutaishia kuwa na *system* ya u-TAKURU ambayo ni *expensive* kuliko rushwa yenyewe. Hili lazima lifikiriwe kwa uangalifu mkubwa. Tusingependa ku-create mazingira ambayo ni vigumu watu kutoaminiana na ambayo tunachungana. Tujiepushe na kuingilia mazingira ya taaluma ya vyuo vyetu. Menejimenti za vyuo hivyo wawajibishwe kutenda kazi zao na kusimamia mazingira ya taaluma. TAKURU itayaharibu na kuvuruga dhana na mazingira ya taaluma kwenye vyuo vyetu kama mtindo wa kuwapeleka huko kunusa utaendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mawaziri katika Ofisi ya Rais, Waheshimiwa Dr. Mary Nagu na

Mheshimiwa Wilson Masilingi, pamoja na watendaji wote wa Ofisi hii kwa kazi kubwa ya kutayarisha na mwisho kuwasilisha bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi kuhusu malipo ya wastaa fu waliochukua mafao yao kwa mkupuo lakini walikuwa hawajafikisha umri wa kustaafu yaani miaka 60. Je, nao watarudishwa kwenye *pay-roll*?

Je, wale ambao hawakuchukua kwa mkupuo na mafao yao yakasimamishwa baada ya kulipwa kwa kipindi fulani wataingizwa kwenye *pay-roll* au watasubiri wafikishe umri wa miaka 60?

Naomba maagizo ya viongozi yanayotolewa humu Bungeni au kwa njia ya vyombo vyta habari yaye yanafuatiwa na barua ya ufanuzi kwa viongozi wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni pale Waziri Mkuu alipotoa tamko kwamba ushuru unaoleta kero kama vile wanaotozwa akinamama wanaouza nyanya na mboga mboga sokoni usitishwe. Kwetu Kigoma haukusitishwa kwa kisingizio cha kukosa barua ya maelezo. Mpaka sasa akinamama wanapigwa, kumwagiwa nyanya zao na wengine wako Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, nachukua fursa hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuunga mkono kwa asilimia mia moja. Hata hivyo kwa kuboresha na hasa ikizingatiwa kuwa kila mara kuna namna bora zaidi ya kuendesha mambo.

Mheshimiwa Spika, nitachangia katika eneo la Utawala Bora. Hali ya rushwa ndogo ndogo imeanza kupungua katika ngazi za chini hususan kwenye shule, hospitali, vyombo vyta usafiri, vyombo vyta fedha na hivyo kuanza kuleta matumaini katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, rushwa kubwa bado ni tatizo hasa katika eneo la mikataba na manunuzi. Upo uwezekano kwamba rushwa ya mikataba inatokana na kukosekana kwa wanasheria waliobobe katika taaluma ya biashara ya soko na mikataba ya Kimataifa. Hali hii isipuuzwe hasa ikizingatiwa kuwa nchi yetu imekuwa na mfumo wa uchumi hodhi kwa muda mrefu na ni dhahiri kuwa wenzetu wa nchi nyingine wametuzidi ujanja kutoptana na uzoefu wa muda mrefu katika biashara ya soko.

Mheshimiwa Spika, zipo taarifa kuwa baadhi ya wawekezaji huja na mikataba yao ilioandaliwa na upande mmoja na sisi kuingia katika mikataba tusiyojua nini kitatokea baadaye. Hata hivyo wanasheria wasio na uzalendo wanaweza kuchukulia udhaifu huo na kupitisha mikataba yenyen walakini. Nashauri, Serikali kuanzisha kitengo chenyen taaluma, uadilifu na uzalendo kwa nchi yetu pamoja na mbinu, mikakati na ujanja wa kuchumia juani na kulia kivilini.

MHE. BEATUS R. MAGAYANE: Mheshimiwa Spika, ningependa kupata ufanuzi kuhusu *SASE Scheme* ambayo kwa kiwango kikubwa ni *discriminatory* hata mionganini mwa wafanyakazi wa ofisi moja. Hivi kuna vigezo mahsusini vilivyowekwa kuondoa uwezekano wa upendeleo na hivi kuwa *counter productive?* Hivi *sustainability* ya mpango huu ikoje hasa?

Mheshimiwa Spika, taarifa ya chanzo cha moto Ikulu imeacha maswali mengi kuliko majibu. Hivi kweli moto unaweza kufukuta kwa siku tatu hata watusika wasione moshi na hivi kuchukua tahadhari? Je, vifaa vya kugundua moto *fire detectors* vilikuwa havifanyi kazi?

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo kubwa la watumishi kupandishwa vyeo hata mara tatu bila kurekebishiwa mishahara kwa kila ngazi. Hii imesababisha madeni makubwa kwa Serikali hasa kwa walimu na wafanyakazi wa Maliasili. Nijuavyo hakuna anayepandishwa cheo bila fedha ya mshahara wake kuwa imepangwa, hivi fedha hizo huwa zinakwenda wapi? Kama Serikali Kuu hutenga fedha hizo na mishahara ya waliopandishwa vyeo, je, wanaotakiwa kulipa wamewajibishwa vipi kwa kuipaka tope Serikali?

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kupambana na rushwa, bado rushwa ni tatizo katika jamii yetu. Ni vema Serikali ikubali ili hatua za pamoja zichukuliwe ili kukomesha tatizo hili. Vigezo kwamba imepungua huenda visisaidie sana kwani watoa uchambuzi huo huenda wasijue hali halisi.

Mheshimiwa Spika, tatizo liko kubwa la watumishi wa Serikali kuwa ndio wakandarasi watoa huduma mbalimbali kwa Serikali, hivi rushwa kubwa ipo katika eneo la ununuzi na bei ya huduma ni ghali mno.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania hatuna tabia ya kujiuzulu pindi kunapotoka tuhuma za rushwa au kutowajibika ili kutoa fursa ya uchunguzi wa kina, ni vema watusika wenyewe wawe wanatoa majibu kupitia *media* ile ile iliyotumiwa na watuhumu ili kutopaka matope Serikali nzima.

Aidha, watoa tuhuma za uongo hadharani washtakiwe ama na Serikali au watuhumiwa wenyewe kwani kunyamaza tu kunaweza kuleta hisia za kukubaliana na tuhuma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwapongeza wote ninyi wawili katika kuandaa Bajeti hii nzuri ya kuboresha huduma kwa watumishi nchini. Nasema, hongera, hongera sana.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu kwanza, sera ya utumishi Serikalini wa mikataba ya miaka miwili miwili na kuwapunguza watumishi wasiokuwa na kosa katika utumishi wao, sio sera nzuri katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, wapo watumishi wazuri waliosomeshwa na Serikali hii kwa gharama kubwa na kupata elimu ya juu, lakini baada ya utumishi wao wa muda mfupi wakaonewa vivu na watumishi wasiokuwa na elimu na kutolewa taarifa chafu au mbaya na kuondolewa katika utumishi wao. Naishauri Serikali watumishi wa mikataba ya miaka miwili miwili katika utumishi wa Taifa letu sasa basi.

Mheshimiwa Spika, pandisheni mishahara ya watumishi Serikalini kwa kiwango kikubwa cha kutosha. Asilimia inayoongezwa kwa watumishi Serikalini ni ndogo mno. Serikali imejibanza kwenye kichaka cha uwezo mdogo, umaskini uliokithiri na kadhalika. Wakati huo huo Serikali inatamka kuwa Pato la Serikali limeongezeka. Kama Pato la Taifa limeongezeka si basi hata watumishi nao wapate mishahara mizuri na hasa ukizingatia sera ya kupunguza watumishi na kubaka na wachache ili maslahi yao yaongezwe na kuwa bora.

Mheshimiwa Spika, rushwa nchini bado ni tatizo la Taifa. Ongezeni juhudzi za kupambana na rushwa na utafiti unatakiwa bado na kuangalia nini chimbuko lake. Baada ya kugundua kiini cha rushwa mikakati iandaliwe ya kuzuia tatizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, napenda kuanza na kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (UTUMISHI) na kuipongeza Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Wizara hii haina miradi ya kutelekeza, lakini ni kiungo muhimu sana kwa kuimarisha utendaji na kufanikisha maendeleo kwenye Wizara nyingine nchini.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni jambo la kuzingatiwa sana, kwani amani haiwezi kupatikana bila Utarawala Bora, haki haiwezi kupatikana bila Utawala Bora na Serikali imara na uongozi imara lazima Utawala Bora uwe madhubuti. Sasa basi kama suala hili linatakiwa kuwa imara, ni lazima adui mkubwa rushwa apigwe vita. Rushwa ni adui wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mimi sielewi Serikali wanaposema rushwa imepungua. Kama rushwa imepungua kwenye Wizara, bado rushwa ni kubwa sana kwenye Halmashauri zote. Wananchi wanakosa imani na Halmashauri hizo pamoja na

Mahakama, bado rushwa inaendelea kuwanyima wananchi wanyonge haki. Mnyonge akinyimwa haki, ni sawa na utumwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri kueleza matatizo yaliyoko kwenye maeneo ya Majimbo ya Vijiini. Kuhusu upungufu wa walimu, shule nyingi zina upungufu wa walimu. Wanapopangwa, wanakwenda kuripoti na kutoweka kwenda maeneo mengine na shule hiyo kubaki bila walimu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TASAF*. Naomba mipango ya Maendeleo ya *TASAF* wapange kwenye maeneo yaliyo nyuma kwani kuna maeneo ambayo wameachwa kabisa. Kuhusu maendeleo ya mipango ya miradi ya maendeleo, hupangwa kwa upendeleo mkubwa na kuyaacha maeneo mengine bila mradi, jambo ambalo halileti haki.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye Bajeti kuna miradi mingi kwenye baadhi Mikoa na Wilaya. Hata mipango ya miradi ya fedha za wafadhili, kuna maeneo mengine hayana hao wafadhili kana kwamba wao hawana matatizo. Naomba usawa wa miradi uzingatiwe kuanzia Serikali Kuu hata Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hotuba hii.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA: Mheshimiwa Spika na mimi napenda kuchangia katika hotuba kidogo tu, ingawa mchango wangu mkubwa umo katika hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa hotuba yake alivyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa sana na mwisho naye Waziri wangu Mheshimiwa Wilson Masilingi, naye nampongeza angalau kwa kusalimiana vizuri kila tunapoonana na hata ninapokwenda na kazi zangu huwa tunazungumza vizuri, ingawa sipati majibu yoyote baada ya hapo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mwanzoni, nilikuwa sina haja ya kuchangia, isipokuwa kuna jambo dogo ambalo nilitaka niliseme kama Msemaji wa Upinzaji wa Wizara hii. Jambo lenyewe ni kuhusu Waziri wa Afya, jana alipokuwa akijumuisha Wizara yake kwa kejeli, alisema kuwa Wasemaji wa Upinzani mwisho wao ni humu ndani tu, lakini ukitoka tu humu ndani hawahuksiki na chochote. Hivi ni kweli hii? Ikiwa mwisho wao ni humu ndani tu, basi kuna haja gani ya kuwepo hii Kambi ya Upinzani? Hivi hii Kambi ya Upinzani si ipo kisheria?

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Upinzani kwa Wizara ya Afya Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, hakutaka kushirikishwa kwenye Wizara, kwenye kazi za Wizara, ila alitaka kushirikishwa kwa mambo madogo madogo tu kama semina na mambo mengine madogo madogo tu ili aielewe vizuri Wizara. Hakuna na maana nyininge.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, atufafanulie hivi Waziri huyu majibu yake yalikuwa mazuri au vipi? Kama Waziri wa Utawala Bora, unasema nini?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa napenda kumwarifu Mheshimiwa Waziri kuwa kwa sababu nchi hii imeamua kufuata mfumo wa vyama vingi, basi Upinzani ni sehemu ya Bunge letu kwa sehemu zote za nchi yetu hii. Nchi ni yetu wote, siyo ya watu maalum na wengine kuwa mwisho ni humu ndani tu. Sitaki nizungumze kitu chochote zaidi ha hiki. Ahsante sana.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote, nawapongeza sana kwa kazi nzuri wanayoifanya na naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, ninachomshauri Mheshimiwa Waziri ni kwamba ili uendeshaji wa Menejimenti ya Utumishi uende vizuri, naomba alete *amendment* ya sheria ile iliyozinyang'anya Halmashauri haki za madaraka ya juu ya watumishi wao mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, natumaini Mheshimiwa Waziri anafahamu kabisa ya kwamba Halmashauri zipo kufuatana na Katiba ya Tanzania. Kwa hiyo, hazipaswi kuonewa bila kubadilisha Katiba.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu nafahamu Mheshimiwa Waziri anailinda Katiba, natumaini tatizo hili mwisho wake utafika sasa.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba ufanuzi, nakumbuka mwaka 2002 tulizindua mradi wa huduma za wateja utakaoteklezwa na Idara za Serikali, je, ni mafanikio na matatizo gani tangu mradi huu uzinduliwe? Je, ni Idara ngapi zilizoingia katika mradi huu?

Mheshimiwa Spika, Serikali imanzisha vitengo vya *PCB* hadi ngazi ya Wilaya kwa ajili ya utendaji bora wa kazi. Naomba vikosi hivi viimarishwe kwa usafiri kwa mfano, magari pikipiki, majengo ya ofisi na kaadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kiambatanisho Na. 6 kinachoelezea mwenendo wa mapato ya Serikali, kasi ya upandaji bei kuanzia mwaka 1992 hadi 2003 na wastani wa mishahara kwa mwaka 1996 hadi 2003, kwa nini haukuweka *exchange rate* iliyopo sasa na iliyokuwepo mwaka 1992?

Mheshimiwa Spika, kwa nini tusilinganishe kwa kuangalia uwezo wa kununua (*Purchasing Power*) kwa wananchi wa kawaida?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa malalamiko ya rushwa yapo katika maeneo ya Hospitali, Mahakama, Halmashauri na Polisi na kwa kuwa Kikosi cha *PCB* kipo Wilayani na mtumishi ni mmoja ama wawili tu.

Mheshimiwa Spika, je, kuna mpango gani wa baadaye kupeleka huduma hadi ngazi ya Tarafa na Kata? Je, Serikali ipo tayari kuhusisha jeshi la sungusungu ambalo lipo katika vijiji na wao hawatotama kupokea rushwa?

Mheshimiwa Spika, ninawatachia kheri na baraka.

MHE. JANET B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu katika kutoa pole kwa familia ya Mrehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa katika nafasi mbalimbali, ikiwemo Bunge la Afrika (*AU*) na hasa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika, pamoja na wengine Mheshimiwa Arcado Ntagazwa na Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuupongeza uongozi mzima wa Ofisi ya Rais, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dr. Mary Nagu katika jitihada za kuleta mabadiliko makubwa katika Idara hii.

Mheshimiwa Spika, suala la Utumishi ni gumu na linahusisha sana suala zima la hatua za binadamu hasa pale mtumishi wa umma anapohitaji haki zake. Madai ya haki za mafao yake hasa pale anapohamishwa au kupunguzwa kazi, ni jambo ambalo bado linaleta usumbufu sana. Hawapati haki za malipo yao wakati unaotakiwa, kwani malipo hucheleweshwa sana na kuleta usumbufu mwangi kwa wafanyakazi. Bado Wizara hii husika ina kazi kubwa ya kufuatilia jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo na miradi inayoendelea kwa kupitia mpango wa makundi maalum, kama vile yatima, wazee, wajane, walemvu na waathirika wa UKIMWI. Sehemu hii bado inahitaji sana ufuutiliaji wa makini na wa kutosha. Aidha, inabainika kwamba bado misaada haiwafikii walengwa kama inavyotakiwa. Waathirika wa UKIMWI hasa bado wanunung'unika kwamba misaada haiwafikii wengine kabisa. Inabidi basi Wizara hii itilie mkazo katika suala la kuhusu huduma kwa walemvu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haijatilia nguvu za kuwasaidia wazee katika Taifa letu. Nchi yetu haijatoa mafunzo ya kutosha kwa wazee ili wajue haki zao. Pia Taifa halijaweza kujali sana kutenga maeneo ya ardhi ili wazee waweze kujifanyia shughuli zao kama vile kilimo cha bustani na kadhalika. Taifa pia halijaweza kujenga nyumba za kutosha katika mikoa mbalimbali za kuwahifadhi na kuwatunza wazee. Ingekuwa bora kuwe na ufuutiliaji wa makini kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la muhimu ni lile la kuwaenzi viongozi waasisi a Taifa la Tanzania. Pamoja na kuwaenzi waasisi hawa, nia iendane pamoja na kutoa uelewa kwa vijana hasa mashulen, ili hao waweze kuelewa historia nzima ya huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, pendekazo lingine liwe ni pamoja na kuwaenzi wananchi mbalimbali waliotumikia nchi hii wakiwa wameshafariki au iwe wangali hai. Kusiwepo upendeleo hata kidogo katika kutoa nishani, kufuatana na upendeleo. Wizara husika ni lazima iwe na kumbukumbu ya wale tangu uanzilishi wa Taifa hili, wamekuwa wakitumikia nchi hii kwa kujitolea na kwa nguvu zao zote. Tuwe na orodha sahihi ya watu hao.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kama itaendelea kuboresha masjala na kukarabati nyaraka kongwe za Kijeruman. Ningombi Serikali iyaangalie sana maeneo yote mbalimbali na hasa yale yaliyokuwepo mikoa mbalimbali. Pamoja na hayo, Wizara ijitahidi sana pia katika kuangalia uwezekano wa kufuutilia maeneo kongwe ya vizazi vyetu vya Tanzania, kama vile ngome za zamani zilizojengwa ili kulinda maeneo ya wananchi chini ya Machifu wa zamani katika kujikinga na maadui mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huu, naomba kuunga mkono hoja mia kwa mia.

MHE. AZIZA SLEYUM ALLY: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nawapongeza sana watendaji wote na Mawaziri, kwa kazi nzuri zaidi wanaoifanya.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika suala la Utawala Bora. Utawala ni uongozi, una sheria ambayo inawaongoza ambao hawana elimu na hawajui sheria yao. Inawapasa kuifahamu, ni sawa na kuongoza mnyama.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sana sheria hizi zirekebishwe ili wananchi waweze kujua sheria za nchi yake ili asivunje sheria. Ni wajibu kujua sheria yenye.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ESTER K. NYAWAZWA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kazi nzuri katika kusimamia Wizara hii vizuri na kuhakikisha watumishi wamepunguza malalamiko.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kuwa uboreshaji wa utendaji katika Maofisi, ni baadhi ya watumishi wachache ndio wakorofi. Naomba nitoe maoni kuhusu Watumishi wa Hospitali, Mahakama na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika Hospitali za Serikali hasa Hospitali ya *General* hapa Dodoma, inasikitisha. Unakuta usafi unanza saa 2.00 asubuhi, watu wanaambiwa wawahii saa 1.30. Kama usafi ni saa 2.00, Daktari aanze kazi saa ngapi?

Mheshimiwa Spika, mgonjwa akifika pale saa 1.30, wafanya usafi hadi saa 3.00, Daktari atafika saa 5.00 asubuhi, anadai alikuwa wodini. Ukimfuutilia wodini hayupo, yuko katika shughuli zake mitaani ama katika *Private Hospital* au anaanzia katika duka lake la Dawa kwanza, ndipo aje kazini. Kama mgonjwa anaumwa sana, anaweza kufa kabla hajapata huduma. Mbaya zaidi ni kwamba akija saa 5.00 asubuhi, anaona

wagonjwa wawili au watatu, anatoka hadi kesho. Huu ni utumishi kweli? Nashauri Serikali iunde Tume ya Utumishi wa Umma, ilifuatilie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ukienda Mahakamani, mtu mwenye kesi, shahidi na mshitakiwa, lazima waende Mahakamani washinde pale wamekaa kumsubiri Hakimu, haonekani au haji kabisa. Huo ndiyo Utawala Bora? Tutapunguza umaskini kweli, mtu kumsubiri mtu ambaye yeche analipwa mshahara, lakini huyu anayesubiri huduma anapoteza muda mwangi bila kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka kuwasaidia wananchi wetu kwa maeneo niliyotoa mfano, Tume ya Utumishi wa Umma ihakikishe inasimamia maadili ya watendaji. Kila mtu awajibike katika eneo lake la kazi aliyopewa na Serikali .

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Waziri wa Utawala Bora, kwa kusimamia suala la uboreshaji wa maslahi ya walimu. Mtu atafanya kazi kwa moyo hata kama mshahara wake utalingana na kazi anazofanya. Kuongeza mishahara ya walimu ni uamuzi mzuri, ni kundi kubwa ambalo tunalitegemea sana katika kusimamia elimu katika kuondoa ujinga. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, nitaomba sana ajira ya walimu wa Sekondari mwaka 2004/2005 iongezwe, kwa sababu wananchi wameamua kujenga Sekondari za kila Kata ili wananchi tuisiwakatishe tamaa kwa nguvu zao walizochangia katika ujenzi huo. Mkoa wa Mwanza tunatarajia mwanzoni mwa mwaka 2005 tutafungua Sekondari 174. Tutashukuru kama zoezi hili litaenda sambamba na ajira za walimu wa shule za sekondari.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mawaziri wote wawili kwa kumsaidia sana Mheshimiwa Rais wetu. Amani na utulivu, wamesimamia na tunazidi kumwombea Rais wetu apone haraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba hii mia kwa mia na fedha zote wapewe.

MHE. AGGREY D. J. MWANRI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), kwa hotuba yake nzuri na yenye uchambuzi wa kina. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Serikali kwa kusikia kilio cha walimu na hivyo kukubali madai yao. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilionyesha *how serious the government is* katika kuwajali watumishi wa umma. Hata hivyo naomba niishauri Serikali kuwa kutamka walimu watalipwa ni kitu kimoja na kupatikana kwa fedha za madai hayo ni kitu kingine. Kuna haja ya kusimamia malipo yanayotokana na madai ya walimu kwa karibu na kuondoa kila aina ya urasimu ambao utazuia haki kutendeka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie miradi ya *TASAF* katika Jimbo langu la Nanyumbu. Miradi mingi imekwama licha ya wananchi kushiriki kikamilifu baada ya kuhamasishwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Ndirika - Mangaka, ni mmojawapo wa miradi ambayo imekwama. Wananchi walianza kuchimba mtaro wa kuitishia bomba kutoka chanzo cha maji kilichopo Ndwiwa kupeleka Mji Mdogo wa Mangaka. Mabomba hayakutosheleza sehemu yote ya mradi huo kutokana na makisio mabaya ya mabomba kwa mradi wote. Sasa mradi huo umekwama na wananchi wa Mangaka wanaendelea kupata shida ya maji. Naomba Serikali kuhakikisha kuwa mradi huo wa maji wa Ndwiwa - Mangaka, unamalizika ili kuondoa tatizo la maji katika maeneo ya Mji Mdogo wa Mangaka, na ili nguvu za wananchi zisipotee bure.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya *TASAF* ambayo imekwama ni ya uchimbaji wa mabwawa katika maeneo kadhaa ambayo wananchi wake wana shida sana ya maji. Miradi hiyo ipo katika Vijiji vya Namasongo na Mp Wahia ndani ya Kata ya Chipuputa, kijiji cha Maneme katika Kata ya Nanyumbu, Kijiji cha Maratani katika Kata ya Maratani na Kijiji cha Mpombe katika Kata ya Napacho. Maeneo yote hayo, wataalam walikwenda wakafanya *survey* na wananchi walishiriki kikamilifu. Tangu wataalam hao waondoke, hatujapata taarifa yoyote juu ya maendeleo ya miradi hiyo ya mabwawa. Wananchi wanaona kama yote hiyo ilikuwa kama danganya toto. Naomba Serikali imalizie miradi hiyo ili kuwaondolea wananchi wa maeneo husika adha ya kukosa maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TASAF* kuhamia kwenye Wilaya zingine katika awamu yake ya pili na kutishia shughuli zake kwenye zile Wilaya za awamu ya kwanza, kwanza nimefurahi kusikia kuwa bado *TASAF* itashirikiana na wananchi kumalizia ile miradi ambayo haijamalizika. Lakini ningependekeza vile vile kuwa *TASAF* iendelee kuwa na miradi mipyä kwenye Wilaya ambazo zilikuwemo kwenye awamu ya kwanza, sambamba na zile za awamu ya pili kwani bado wananchi wanazo shida nyingi ambazo hazikwisha kwenye awamu hiyo moja. Tatizo ni kuwa wananchi walikuwa na shida nyingi sana kuliko uwezo wa *TASAF* kusaidia zote hizo. Haukuwepo au urasimu katika kupata ufadhili, ulikuwa mkubwa. Wananchi waliomba kusaidiwa ufadhili katika miradi mingi sana, lakini ni michache tu ndiyo iliyofanikiwa kupata ufadhili. Kwa vile bado wananchi katika Wilaya ambazo zilikuwemo kwenye awamu ya kwanza, wanazo kero nyingi ambazo wangependa kusaidiwa, basi naomba *TASAF* iendelee kufadhili miradi mipyä katika Wilaya hizo.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

SPIKA: Katika waliojiorodhesha kuchangia hoja hii amebaki mmoja tu Mheshimiwa Benedict Losurutia, lakini hayupo Bungeni. Asiyekuwepo na lake halipo. Kwa hiyo, mjadala huu umefikia mwisho. Tutakaporejea saa 11.00 jioni Mawaziri wawili

wenye hoja hii wataanza kujibu halafu tutaendelea na hatua nyingine kama tunavyofahamu.

Kwa hiyo, baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.32 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kabla sijatoa maelezo juu ya hoja ambazo zimewasilishwa kuhusiana na masuala ya hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri mwenzangu, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salaam za rambirambi kufuatia msiba uliotufika hapa Bungeni wa kuondokewa na marehemu Mheshimiwa Yetet Sintemule Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini.

Aidha, natoa salaam za pole na za rambirambi kwa Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini na familia yake kufuatia kifo cha mtoto wake mpendwa. Naomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili, napenda kutoa shukrani na pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa jinsi alivyowasilisha hoja ya Ofisi hii ya Rais na pia nitoe shukrani na pongezi kwa Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu, Ikulu na Watumishi wote katika Ofisi ya Rais, Ikulu na Utumishi kwa ushirikiano na kazi nzuri ambayo wameifanya kufanikisha kazi ambazo tumezitolea taarifa na kuwasilishwa kwa niaba yetu na Waziri Mheshimiwa Dr. Mary Nagu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, natoa shukrani na pongezi kwa Mwenyezeki wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wao wa hali ya juu sana na maneno ya ushauri ambayo wametoa kwetu wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, nampongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, ambaye amewasilisha Taarifa ya Kamati kwa niaba ya Mwenyezeki wa Kamati na Wajumbe kwa kazi nzuri anayoifanya. Pia, natoa shukrani za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wa hali ya juu waliochangia na ambao hawakuchangia. Wale ambao wamepata fursa ya kuchangia kwa kauli na maandishi, michango yao tunaiheshimu na tunaichukua kwenda kuifanyia kazi. *(Makofî)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka Mheshimiwa Rais katika hotuba yake ya mwisho wa mwezi Juni ametamka kwamba Serikali inaheshimu na itazingatia na kufanya kazi ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ambao wanautoa katika Mkutano huu wa Bajeti. Kwa hiyo, yale ambayo tutashindwa kuyazungumza au kuyatolea ufanuzi katika dakika 30, haina maana kwamba hayana uzito. Kama Waheshimiwa Mawaziri waliotutangulia walivyokuwa wanaahidi mbele ya Bunge hili, tutaendelea kuwasiliana na Bunge kutoa ufanuzi tukiwajibika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kueleza kwa shukrani kabisa kwamba ushauri uliotolewa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala wakitoa wito kwa jamii kwa ujumla kushirikiana katika mapambano ya rushwa, tunaupokea kwa heshima na tutaendelea kuboresha mikakati yetu tukizingatia mbinu za kisayansi ili kukabiliana na tatizo hili gumu la rushwa.

Mheshimiwa Grace Kiwelu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amechangia akizungumzia maeneo mengi ya Utawala Bora. Ningependa kumshukuru kwa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani na ningependa kumhakikishia kwamba sisi tutaendelea kushirikiana na Kambi ya Upinzani kufanya yale ambayo wameshauri na tunaona yanaweza yakawa na manufaa kwa umma. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Grace Kiwelu, amezungumzia demokrasia, mikutano ya hadhara na *FFU*, kuweka bendera nyekundu katika mikutano hiyo na akanitaka nitoe miongozo juu ya suala hili.

Napenda tu kumhakikishia kwamba kama Waziri nikumbushe tu miongozo ipo na sheria zipo. Ninaloweza kusisitiza ni kwamba, kwa sababu mikutano ni halali na ina vibali, tushirikiane wanasiasa na viongozi wa siasa kuwashimiza wasikilizaji wetu katika mikutano ya hadhara kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa ili kuepusha *FFU* kutumia virungu.

Pili, ameshauri kwamba Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (*PCB*) wawajibike kwa Bunge na siyo kwa Rais. Haya ni mapendekezo ambayo yanaweza yakajadilika. Binafsi naamini kwamba Bunge ndiyo mamlaka ya hali ya juu na Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge. Bado nitaendelea kuamini kwamba Bunge lina uwezo wa kusimamia Serikali na Taasisi zake kwa mujibu wa Katiba. Lakini iwapo yatakuwepo mapendekezo na jamii ikaafiki, marekebisho yanaweza yakafanyika kwa mujibu wa taratibu na Katiba ya nchi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, amezungumzia masuala ya Mheshimiwa Mchungaji Christopher Mtikila kwamba kama alisema uongo achukuliwe hatua. Binafsi napenda kushauri tu kwamba, masuala ya Mhehsimiwa Mchungaji Christopher Mtikila nimeyazungumzia mara nyingi na huwa napenda kumheshimu sana Mheshimiwa Mchungaji Christopher Mtikila kama raia na kiongozi wa chama cha siasa, si vizuri kuendelea kumjadili ndani ya Bunge. Ningeshauri Kambi ya Upinzani wamshauri Mchungaji Christopher Mtikila ili aweze kuendesha mambo yake kwa mujibu wa sheria

na wanaweza wakamsaidia kuyafikisha kunakohusika kama wanaona hayashughulikiwi sawa sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba Polisi wasiendeshe mashtaka bali wafanye kazi ya upelelezi tu, huo ni ushauri amba ni mzuri na tayari Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba ameshaanza mashauriano na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuangalia namna ya kuboresha eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba *PCB Director General* ateuliwe na Rais na kuthibitishwa na Bunge, hayo ni mapendekezo kama mengine niliyozungumzia yanayohusiana na uboreshaji wa Mamlaka ya Bunge na Katiba yetu. Kwa hiyo, nisingependa kutoa maoni yangu kwa sababu ni mjadala na mapendekezo yanaweza yakaendelea kujadilika katika nyanja za mashauriano katika pande zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuimarisha ukaguzi wa ndani wa sekta zote ni sawa, hakuna asiyependa kufanya hivyo na Waziri wa Fedha ametoa taarifa mara nyingi, jitihada zinazofanyika kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa hesabu za Serikali kwa mujibu wa sheria za hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kuweszsha Bunge na Kamati zake kufanya uchunguzi, hili tayari linafanyika kwa mashirikiano mazuri kati ya Serikali na Bunge na Kamati za Bunge zinaendesa chunguzi kadhaa ambazo kila Mbunge anafahamu na sina sababu yoyote ya kuingia undani wa uchunguzi huo kwa sababu sitawajibika kutoa taarifa mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kwamba hatua zichukuliwe haraka, ni ushauri amba ni tunauchukua, lakini ni lazima nitahadharishe kwamba ni lazima tunapochukua hatua dhidi ya watumishi tuzingatие haki za binadamu na sheria. Haraka haraka haina baraka, lakini kuongeza haraka kwa maslahi ya umma ni jambo ambalo litatiliwa mkazo na litaendelea kutiliwa mkazo ili kuondoa kuwakatisha watu tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kwamba wanaofanya vizuri watambuliwe, ni jambo zuri tutawatambua. Pia kuhusu kwamba mamlaka huru ziundwe za kusimamia Taasisi za Umma, haya ni mapendekezo ambayo yanajadilika, mimi bado naamini Bunge ni mamlaka ya juu na huru ya kuweza kusimamia Taasisi zote za Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Msemaji wa Kambi ya Upinzani amesema Sekretarieti ya Maadili ifutwe kwa sababu kwa mujibu wa Msemaji wa Kambi ya Upinzani anaona haifanyi kazi na pesa zinaharibika.

Napenda kuchukua nafasi hii kupongeza Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kazi nzuri wanayoifanya. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ikiiongozwa na Mheshimiwa Jaji William Maina, inafanya kazi nzuri na kazi hii wameianza tangu mwaka 1995 na dunia inatuheshimu kwa hilo kwa sababu Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Nchi hii na

inaendeshwa kwa mujibu wa sheria zilizotengenezwa na Bunge hili Tukufu na wao hawawezi kufanya mambo kinyume cha sheria kwa sababu ni waadilifu. Hatuwezi kuwatia kashkash ili wavuruge mambo kufurahisha watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la viongozi kuandikisha magari na majumba ya thamani kubwa kwa majina ya watoto walio chini ya umri wa miaka 15 hatua gani zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Grace Kiwelu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, kwa mujibu wa kifungu cha 9 kifungu kidogo cha kwanza cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995, kiongozi anatakiwa kutaja mali zake, mali za mke au mume na watoto walio chini ya umri wa miaka 18. Hivyo, siyo kosa kwa kiongozi kuandikisha mali kwa majina ya watoto walio chini ya umri wa miaka 15 mradi kiongozi huyo anataja mali hizo katika tamko lake analotakiwa kutoa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kwamba, mwananchi anapotaka kujua kiongozi anamiliki nini anaambishi ajaze fomu za maombi na kutakiwa kulipa fedha na taarifa anazozipata haruhusiwi kuzitoa popote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi anayetaka kujua kiongozi anamiliki mali gani hatakiwi kujaza fomu yoyote ila anatakiwa kuwasilisha maombi katika Ofisi ya Kamishna wa Maadili ya Viongozi wa Umma kwa maandishi au kwa kufika mwenyewe tu akazungumza na Watumishi wa Sekretarieti ya Maadili. Masharti ya kuona mali hizo yamewekwa kisheria kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 108 la mwaka 1996.

Masharti hayo ni mwenye kutaka kuona mali hizo kuwa na malalamiko dhidi ya kiongozi anayehusika na kulipa ada ya shilingi 1,000/=. Taarifa za mali hizo mwananchi anaweza kuzitoa popote isipokuwa haruhusiwi kuzichapisha kwenye magazeti. Kwa mfano, kama mwananchi huyu anamtuhumu kiongozi kwa rushwa au wizi, basi anaweza kupeleka taarifa hizo Taasisi ya Kuzuia Rushwa au kituo chochote cha Polisi.

Hata hivyo kiongozi yejote anaweza kutangaza mali zake kwenye magazeti kama anataka kufanya hivyo yeye mwenyewe na tunakaribisha viongozi wa upande wa Upinzani wafuate mfano wa viongozi wa CCM kutangaza mali hizo kwenye magazeti na redio, lakini tuna wajibu wa Kikatiba kulinda usiri wa mali za viongozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kwamba majukumu ya sekretarieti yanaweza kufanywa na vyombo vingine kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Usalama wa Taifa na vingine vingi ambavyo Serikali inavijua. Maeleo tunayoweza kutoa ni kwamba, sekretarieti inafanya kazi yake kwa karibu na ushirikiano na vyombo vyote hivyo ambavyo tumevitaja yaani Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Taasisi ya Kuzuia Rushwa, Polisi na Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma. Sekretarieti inashughulikia maadili ya viongozi maalum walijotajwa katika sheria wakati vyombo vingine vilivyotajwa vinashughulikia maeneo maalum ya Utawala Bora kama rushwa,

haki za binadamu na jinai za kawaida, wizi, ubadhilifu na mengineyo. Kwa hiyo, mgawanyo kwa kuzingatia taaluma na uzoefu ni jambo ambalo tunapaswa kulipatia kipaumbele.

Napenda sasa nielezee maneno ambayo yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge katika michango yao na nitachanganya, walioandika kwa maandishi na waliozungumza. Nianze na Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, anasema rushwa kubwa hasa inayohusu mikataba ni budi tuitilie mkazo pia kama tunavyofanya kwa rushwa ndogo ndogo na akashauri kianzishwe Kitengo cha Wataalam Maalum Waadilifu watakaochambua Mikataba ya Kimataifa ili kuepusha ubadhilifu. Ni wazo zuri, lakini napenda kumhakikishia kwamba Serikali ina mikakati ya kuimarisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuboresha Kitengo cha Sheria za Mikataba ili tuweze kuondoa mapungufu yaliyopo.

Mheshimiwa Beatus Magayane, anazungumza kwamba, vigezo vinavyotumiwa kueleza kwamba rushwa imepungua huenda wasijue hali halisi ya nchi yetu, kwa hiyo si vizuri kuwafuata. Binafsi nakubaliana naye. Mtakumbuka nimesema mara nyingi kwamba tunavyopata taarifa kutoka nje ya nchi kupitia vyombo kama *Transparency International* sisi huwa tunavichukua kwa sababu dunia nzima inavichukua, lakini tunakuwa na wasiwasi na vigezo wanavyovitumia kwa sababu wameniambia mara kadhaa kwamba wao wanategemea taarifa za magazeti na Wananchi wa kawaida mitaani. Sasa sisi hiyo tunaona ni *very subjective* kwa sababu mtu kama anachukia Serikali mtaani yuko *jobless pale Samora Avenue*, ukimuliza rushwa anasema: “Inaongezeka karibu tunakufa,” kama hajala chakula.

Sasa hayo siyo mambo ya kuamini kwa kweli na magazeti yakiamua *ku-gang-up* dhidi ya Serikali iliyoko madarakani watakuwa kila gazeti wanaeleza rushwa inapaa, rushwa inapaa na hizo *cuttings* ndizo wanazozitumia wanaofanya tafiti za ongezeko la rushwa kutukandamiza kama Tanzania.

Sasa mimi huwa nasema hawatutendei haki, lakini hatusemi rushwa hapa hakuna. Tumekubaliana Jumuiya ya Kimataifa kwamba hakuna nchi yenye uwezo wa kumfundisha mwenzie juu ya mapambano dhidi ya rushwa. Kwa hiyo, tushirikiane kwa heshima na kila nchi ina wajibu wa kupambana na rushwa. (*Makofii*)

Kuhusu suala la kwamba wanaotoa tuhuma hadharani washtakiwe ikibainika wanasema uongo, ni ushauri mzuri wa Mheshimiwa Beatus Magayane. Sisi tumejaribu kuachia watu wakomae, kuburuzana Mahakamani ni taabu sana. Kadri tunavyosonga mbele watu wakichokana hasa tunapoelekea Uchaguzi Mkuu wataanza kuburuzana Mahakamani asubuhi na jioni, lakini tuvumiliane, watu wasiseme uongo. Tukosoane kwa nia ya kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, amesema kwamba rushwa ndogo inapungua, lakini bado ipo kubwa na ile kubwa ni hasa kwenye manunuzi, kwa hiyo, tulipe mkazo. Kwa kweli tunalipa mkazo, kutekeleza Sheria ya Manunuzi ya

Serikali ya mwaka 2001 na kuboresha miundombinu ili kuwadhibiti hawa wanaopenda kula rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Salim Omar Ali anazungumzia ukarabati wa Ikulu ni muhimu na hasa mapokezi na jengo la polisi na la walini za Ikulu. Tunaupokea ushauri wake kwamba ujenzi uharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa kupiga simu kutoa taarifa za rushwa, upo unaendelea na haulazimiki kutaja jina lako, wewe ukishasema tu, *PCB* wanakupokea na kushughulikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lekule Laizer, anasema rushwa hasa kwenye Halmashauri za Wilaya ni kero. Tunapeleka Ofisi za Taasisi ya Kuzuia Rushwa mpaka Wilayani kwa kuzingatia umuhimu wa kukabiliana na rushwa katika Halmashauri za Wilaya. Kwa hiyo, ushirikiano wa Bunge ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TASAF* kwamba maeneo yaliyoko nyuma yazingatiwe, yafikiriwe katika kutoa miradi, ni ushauri mzuri na awamu ya pili itagusa Wilaya zote na zile ambazo tayari zinahusika na *TASAF* miradi haitasitishwa, lakini watahakikisha miradi inakamilishwa kabla ya mwisho wa mwaka huu. Kwa hiyo, Wilaya ya Monduli hasa Jimbo la Longido bila shaka litaguswa ipasavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, amesema Hakimu anachelewa kuingia Mahakamani hivyo anachelewesha watu kwenda kulima. Nakubaliana naye, kwa kweli si Utawala Bora. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Sheria na Mambo ya Katiba bila shaka kwenye hotuba yake atawezeku kilitokea kauli. Ninachowezwa kusema sasa hivi ni kwamba, toeni taarifa za Mahakimu wenyewe tabia za namna hiyo ya ulevi au jeuri tu. Hakimu asiyefika saa tatu kazini wewe Mbunge mjulishe Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya akikataa kuchukua hatua kutumia Bodi za Mahakama za Wilaya tujulisheni ili tuweze kumshughulikia yule Hakimu kwa sababu anavunja heshima ya Mahakama.

Mheshimiwa Ruth Msafiri, anapongeza *TASAF* na anashauri Ikulu ulinzi getini uimarishwe. Pia anashauri takrima wakati wa uchaguzi isiruhusiwe. Hili limeanza kuzua mjadala. Wale ambao hawakuwa Bungeni wakati sheria hii inapita linawapa utata. Lakini mara nyingi ninapajaribu kueleza historia yake nachukuliwa kama natetea rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika takrima tuliiweka katika sheria ili kuendana na mazingira ya kitamaduni ya Kitanzania kwamba huwezi ukawa uko kwenye kampeni na kundi la watu 20 ikafika saa ya chakula ukawaambia: “Nipisheni kwa sababu mimi ni mgombea, halafu tukutane kesho asubuhi wakati wa mzunguko.” (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mazingira yetu hairuhusiwi, lakini tukasema hivi, kama kuna mtu na hili ndiyo nataka kusositiza, kama kuna mtu ana mashaka kwamba takrima imekuwa juu ya kiwango kuelekea rushwa anapelekwa Mahakama Kuu na

Mahakama itaangalia ushahidi, hivi hii pilau ilikuwa gunia ngapi au sahani ngapi au bia kiasi gani, maana ni kazi ya Mahakama. Lakini tukisema Watanzania tudanganye dunia kwamba mgombea anawenza akazunguka anakula mwenyewe, anakunyuwa mwenyewe eti anapambana na rushwa sio sahihi! (*Kicheko/Makofi*)

Mmemsikia Mheshimiwa Rais kwenye hotuba yake ya mwisho wa mwezi anaeleza habari za Marekani. Sisi hatuwezi kujilinganisha na Marekani, lakini ni vizuri tukaulizana na wale, mtu anachangiwa zaidi ya shilingi milioni 340...

WABUNGE FULANI: Dola.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Dola za Kimarekeni, ni mabilioni ya shilingi na wanaendelea kuchanga kwa ajili ya uchaguzi. Sasa sisi huku wanasema: “Mtanzania aende na suruali yake na *briefcase* achukue fomu, apambane mpaka awe Mbunge. Hakuna mtu kunywa soda wala pilau.” Hiyo siyo *realistic* kwa kweli. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mjadala unawenza ukaendelea, lakini mimi sitetei rushwa, tunasema takrima ni *realistic*. Mimi nimegombea mara tatu, lakini huwezi ukasema nimwambie mtu: “Toka nje nile kwa sababu mimi ni mgombea unajua.” Lakini yeze akikupa bia unakunyuwa kwa sababu yeze si mgombea! Sasa huo tunaita unafiki. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, ameeleza kwa machungu sana na akanitaka nitoe majibu kilichotokea Tabora ni Utawala Bora? Kwa kweli siyo Utawala Bora. Natamka waziwazi bila kusita na ninaungana naye kwa majonzi kabisa, tunaomba roho ya Marehemu Diwani, Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema na sisi Serikali nimeshawapatia taarifa alizoniletea Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo vyombo vyetu wafuatilie kwa haraka ili haki itendeke na yeze atashirikishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, yeze ametoa ushauri mzuri kuhusu kuboresha mishahara, mikataba, madeni kupitiwa na *performance audit*. Ni mambo mazuri ameshauri, lakini isipokuwa amekerwa sana na kauli ya Serikali ambayo ilitolewa, anadhani ililetwa kama mkakati wa kuzuia Wabunge wasiseme. Kwa kweli nilizungumza wazi kwa niaba ya Serikali kwamba hatuna nia ya kufunga mjadala ndani ya Bunge au nje ya Bunge. Lakini kauli ya Serikali ilitolewa kwa kuzingatia haki ya Serikali pia kujieleza mbele ya Bunge na mbele ya Wananchi kama ambavyo Mbunge ana haki ya kusema na sisi hatuwezi kuzuia Mbunge kusema.

Kwanza Serikali haina uwezo wa kufunga midomo ya Wabunge, hatuna. Hata tungkuwa na nia hiyo, lakini Serikali tukisemwa ni lazima tuseme maana tunawajibika kwa Bunge. Sasa hiyo siyo *pre-emptive action*. Kwani tunategeshana hapa, tunategana! Hapa ni kusema uwazi na ukweli ili tuboreshane katika mjadala dhidi ya rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halimensi Mayonga anasema rushwa ndogo zidhibitiwe, lakini anaridhika mambo ni mazuri, yale madogo madogo tuyakabili. Tunakubaliana na ushauri wake.

Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, anaomba Utawala Bora kusaidia Wabunge kupambana na rushwa. Tunawashukuru *APNAC* na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, kwa ushirikiano tunaoupata katika kupambana na rushwa ni mambo ambayo tutaendelea kushirikiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, anataka nitoe kauli, hivi vivuli wanaishia ndani ya Bunge?

MBUNGE FULANI: Ndiyo.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Wanasema kwa sauti kwamba ni ndiyo. Sasa mimi sijui mwanga unatoka ndani ya Bunge tu, ukitoka nje unazimika! Nitaendelea kushauriana na Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, kwenye hili ili tuliboreshe kwa kushirikiana na Wabunge wenzetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, amezungumzia moto wa Ikulu. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imetoa taarifa na tumeipokea kwa masikitiko. Tunaomba tuendelee kushirikiana kuzuia haya yasitokee kama walivyotushauri wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Frank Mussati, ametoa pongezi kwa *PCB* kwenda hadi vijiji. Kasulu wameshafika na pongezi kwa *TASAF*. Wataalam wanazisikia, tunazipokea kwa heshima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, kweli mwaka 2003 alileta taarifa ya tuhuma za rushwa. Alileta kwa maandishi na wataalam wameniletea taarifa kwamba uchunguzi unaendelea na kazi hiyo amepewa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali ili kusudi akishirikiana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Polisi wachunguze tuhuma za rushwa katika Sekondari za Tarime, Musoma Ufundu na Mara na kadri watakavyokuwa wanakwenda katika uchunguzi huo ni lazima Mheshimiwa Mbunge ajulishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kumwomba tu awe na subira kwa sababu kama kweli walifanya vituko, tunaamini hiyo timu kwa sababu ni ya watu wengi, Polisi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Kuzuia Rushwa na Usalama wa Taifa. Tutaweza kumletea majibu ambayo yanaridhisha na jinai haozi, tusiwe na haraka, tutawadhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, amesema sheria zisambazwe kwa watumishi wa umma, tutafanya hivyo. Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, ameshauri kuchunguza chanzo cha rushwa, tutaendelea kufanya hivyo na kuboresha mikakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niseme siyo rahisi kujibu kila hoja ambayo imetolewa, lakini napenda kusema kwamba Waheshimiwa Wabunge wametupatia ushauri mzuri sana. Ambao nilikuwa sijawafikia ni pamoja na Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, anayesema kwamba sio vizuri hizi Ofisi za Wakuu wa Taasisi kuzipeleka kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya labda zitaingiliana na uhuru wao. Hawajapata maeneo huru, kwa hiyo, tukipata uwezo watajengewa ofisi huru.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia tu kwa kumshukuru tena na kumpongeza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Dr. Mary Nagu, kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kuwasilisha hoja kwa niaba yetu na akafanya kazi hiyo vizuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, mtuvumilie kwani hoja zinazohusu Utawala Bora ni nyingi. Tutatayarisha na sisi kitabu ili kusudi tujibu kwa ufasaha zaidi, kutoa maelezo ya nyongeza ili tuweze kushirikiana. Tunaomba mtuidhinishie fedha ili tutekeleze majukumu haya tusonge mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati nakushukuru wewe na Mheshimiwa Spika, kwa uongozi wenu mahiri kwa jinsi mlivyoongoza majadiliano ya leo ya Bajeti ya Ofisi ya Rais na Asasi zake. Aidha, kwa moyo huo huo nampongeza Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge wa Mwanga, kwa kuwasilisha kwa ufasaha Maoni na Ushauri wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Kamati anayoongoza Mheshimiwa Athuman Janguo, Makamu wake, Mheshimiwa George Lubeleje.

Ningependa kuihakikishia Kamati yetu kuwa, maoni na ushauri wao wote utazingatiwa kwa kutambua kuwa ushauri wao utasaidia katika kuboresha utendaji ndani ya Serikali. Napenda kukiri kuwa maoni na ushauri wao umetokana na ushiriki wao wa makini na wa busara katika kufuutilia utendaji wa Ofisi ya Rais. Napenda vile vile kuishukuru Kambi ya Upinzani na hasa Mheshimiwa Grace Kiwel, aliyewasilisha maoni yao. Yale yote ambayo yanachangia katika kuboresha utendaji wa Serikali tutayazingatia ipasavyo na kwa makini sana. Yale ambayo yana nia ya kudhoofisha tutajaribu kuyakwepa ili Serikali ya CCM iendelee kuongoza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuendelea kuwapongeza na kuwashukuru Wabunge wenzangu waliochangia kwa maandishi au kwa kusema katika hoja yangu na hoja ya Waziri wa Utawala Bora na Mawaziri wengine walionitangulia wakiwasilisha hoja zao. Wingi wa michango yenu ambayo ni zaidi ya 30 inaonyesha shauku yenu katika kufuutilia utendaji katika Ofisi ya Rais na Asasi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kwa heshima na taadhima niwatambue wote waliota michango yao kwa kuanza na wale waliochangia kwa kusema hao ni pamoja na Mheshimiwa Wilson Masilingi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati na Mbunge wa Mwanga, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Bernard Membe, Mheshimiwa Halimensi Mayonga, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafuatao ni wale waliochangia kwa maandishi katika hotuba ya leo ambao vile vile nawapongeza na kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wa kwanza ni Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Salim Omar Ali, Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Janet Kahama, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Lekule Laizer, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Gwassa Sebabi, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Joel Bendera na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandomsy, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. (*Makofî*)

Kama mlivyoshuhudia, michango ni mingi na ni mizuri yenyewe busara na hivyo itatusaidia katika kuboresha shughuli zetu. Namshukuru Mheshimiwa Wilson Masilingi, kwa kunisaidia kujibu hoja zenu ipasavyo. Maelezo yangu yataelekezwa zaidi maeneo ambayo hajayagusa na hususan yale yanayohusu Utumishi wa Umma. Muda ukiruhusu nitasisitiza mengine ambayo yanahitaji msisitizo. Nitaanza na hoja ya kwanza ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maslahi ya watumishi yamekuwa yakiboreshwa kama nilivyozungumzia katika hotuba yangu kwa mfano mishahara imikuwa ikiboreshwa, malipo ya mishahara huzingatia vigezo maalum kwa mfano elimu, ujuzi, uzoefu na mtiririko wa mamlaka na madaraka. Uoanishaji wa malipo ya mshahara kati ya taasisi na Serikali ni moja ya mambo yanayoendelea kushughulikiwa katika utaratibu wa uboreshaji wa mfumo wa mishahara katika utumishi wa umma. Wote mnajua kwamba kwa kweli kazi ya uboreshaji utumishi wa umma ni kubwa na inahitaji umakini sana. Ni kweli kuna taasisi ndani ya Serikali watumishi wanalipwa zaidi kuliko wengine hata pale ambapo utaalam unafanana. Lakini ni kutokana na mahitaji maalum ili kuongeza ufanisi na tija ndani ya Serikali na hiyo ni kwa kuibua tu, lakini kwa siku za usoni tutajitahidi sana kuhuisha na kuona kwamba wale wenye utalaam unaofanana, uzoefu unaofanana na mengine yote yanayofanana wanapata ujira unaofanana vile vile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu malipo ya malimbikizo ya maslahi ya walimu na watumishi wengine Serikalini, Serikali imeshatoa tamko rasmi wakati wa hitimisho la hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba malipo haya yataendelea kulipwa katika

mwaka huu wa fedha 2004/2005. Ningependa kusema vile vile kwamba Tume ya Utumishi ya Umma, ilianza na kazi hiyo, kwa kuzingatia kwamba walimu ni muhimu sana katika uondoaji wa umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza kiwango cha chini cha pensheni, Serikali ingependa kufanya hivyo, lakini tatizo ni uwezo hasa ikizingatiwa kuwa tunawarejesha wale ambao walilipwa pensheni yao kwa mkupuo. Bajeti ya Serikali inahitajika kwenye maeneo mengi sana. Kwa hiyo, tukifanya kila kitu kwa mara moja itakuwa kila kitu tutakifanya kwa ufanisi ambao hautamsaidia mtu yejote. Kwa hiyo, kwa siku za usoni tunaangalia kima cha chini cha wastaafu, lakini kwa mwaka huu tunaona kwamba kwanza tuwahudumie wale ambao hawana chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewa kuanza kuwalipa waliolipwa kwa mkupuo, tatizo ni kukamilika kwa taratibu za kuwahakiki na kuwaorodhesha wastaafu wahusika. Wastaafu wametawanyika nchi nzima na kupata taarifa zao kwa kweli inachukua muda kwa sababu nchi hii ni kubwa. Lakini tutalipa pale ambapo tutamaliza kazi hiyo na mimi nawahakikisha Waheshimiwa Wabunge na wastaafu wenyewe kwamba tunajitahidi ili wastaafu hawa wasiendelee kukaa na adha. Kulingana na taratibu hawa pamoja na wengine watalipwa pensheni zao kulingana na sheria zilizopo. Mambo ya Serikali yanafanya kiutaratibu na kanuni na kisheria na kwa hiyo, malipo ya wastaafu hawa ambao tumewarudisha kwenye malipo ya kila mwezi yatafanywa kwa mujibu wa sheria ambazo zipo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kugusia vigezo vilivyotumika kuongeza mshahara kwa kati ya asilimia 9 hadi asilimia 12.5 hili liliulizwa na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mbunge wa Moshi Vijiji. Bajeti ya mishahara (*Wage Bill*) imeongezeka kwa asilimia 18, sehemu ya Bajeti hiyo itatumika kwa gharama za ajira mpya. Ukiongeza mishahara kupita kiasi maana yake unapunguza ajira mpya kwa sababu na ajira mpya nayo inalipiwa kutokana na wage bill hiyo hiyo. Sehemu nyingine inalipa gharama za upandishwaji vyeo watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, umesikia watumishi wa umma wanavyolalamika kwamba wanakaa muda mrefu kwenye cheo kimoja bila kupandishwa, yote haya yanaangalia *wage bill* ambayo leo asubuhi niliitolea hoja. Salio ndiyo linatumika kuongeza viwango vya mishahara ambapo tunaangalia uchumi na mapato ya Serikali. Hatuwezi kulipa mishahara kupita uwezo wa mapato ya Serikali au mapato ya nchi. Vile vile tunaangalia mfumko wa bei ambao kwa kiasi kikubwa ndiyo unakula fedha za mishahara au ujira wa watumishi. Lakini ukiangalia kwenye picha ambayo iko kwenye kitabu cha hotuba, utaona kwamba mishahara ya watumishi wa umma, daima imekuwa juu ya mapato hata ya nchi na mapato ya Serikali na utaangalia kwa kadri mfumko wa bei ulivyokuwa unashuka, mishahara ilikuwa inapanda, maana yake ni kwamba real wage ilikuwa inaongezeka na kwa hiyo kwa kweli ndiyo maana hata sikikii sana manung'uniko ya watumishi wa umma kwa sababu kutokana na utaalamu wao na uelewa wao wanajua kwamba Serikali imejitahidi sana kuboresha maslahi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo ningependa kuongelea ni uhamisho wa watumishi wa umma na hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Grace Kiwelu na

Mheshimiwa Bernard Membe. Sera ya Serikali kuhusu kuhamisha ni kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa kazi wa watumishi. Hata hivyo chini ya utaratibu mpya wa ajira na usimamizi wa watumishi wa umma, uhamisho utakuwa unafanyika pale tu ambapo waajiri wamekubaliana au Serikali itaona ni lazima sana kufanya hivyo kwa manufaa ya umma na kazi hiyo itakuwa inafanywa na Ofisi ya Rais, Utumishi.

Hoja nyingine ni ajira za watumishi wa afya kujaza nafasi zilizo wazi. Hoja hii ilitolewa na Mheshimiwa Halimensi Mayonga na Mheshimiwa Dr. Zainab Gama. Uamuzi wa kuajiri moja kwa moja watalaam wa kada nyeti umekwischachukuliwa na Serikali kwa mfano nafasi zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha kwa sekta ya elimu ni nafasi 12,799. Kwa sekta ya Afya ni nafasi 2,372. Kwa Sekta ya Polisi ni nafasi 175, kilimo ni nafasi 723 na watumishi wengine ni nafasi 9,443. Kama kuna wengine ambao bado wako hawajapata kazi inawabidi na wao waende watoe taarifa kwa sababu taasisi zinazowafunza watumishi wa sekta ya afya siku hizi ni nyingi.

Kwa hiyo, Serikali haitaelewa kwa urahisi hasa pale ambapo tulikuwa tumesimamisha ajira kujua ni nani ambaye hajaajiriwa wakati kuna zahanati ambazo zinakaa bila madaktari au watumishi wanaohudumia sekta ya afya. Lakini ikumbukwe vile vile kwamba ajira vile vile inategemea uwezo wa Serikali kuajiri katika mwaka ule. Kila tunapopata uwezo tutakuwa tunawaajiri watalaam wanaotakiwa hasa kwenye sekta ya afya na sekta ya elimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kuongelea hoja ya viongozi kuandikisha magari na majumba ya thamani kubwa kwa majina ya watoto walio chini ya umri wa miaka 15 hatua gani zimechukuliwa. Hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Grace Kiwelu na kwa kiasi kikubwa Mheshimiwa Wilson Masilingi, ameiongelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu namba 9 (1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 kiongozi anatakiwa kutaja mali zake, mali za mke au mume na mali za watoto walio chini ya miaka 18. Hivyo siyo kosa kwa kiongozi kuandikisha mali kwa majina ya watoto walio chini ya miaka 15, mradi kiongozi huyo anataja mali hizo katika tamko lake analotakiwa kutoa kwa mujibu wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma. Kwa hiyo, siyo kosa kuandikisha mali yako kwa jina la mtoto wako ilimradi unaitaja kwenye tamko lako la mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni wananchi wanapotaka kujua kiongozi anamiliki nini anaambiwa ajaze fomu za maombi na kutakiwa kulipa fedha na taarifa anazipata harusiwi kuzitoa popote. Hoja hii vile vile imetolewa na Mheshimiwa Grace Kiwelu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwananchi anayetaka kujua kiongozi anamiliki nini hatakiwi kujaza fomu yoyote, ila anatakiwa kuwasilisha maombi katika ofisi ya kamishna wa maadili kwa maandishi au kwa kufika mwenyewe. Masharti ya kuona mali hizo yamewekwa kisheria kwa mujibu wa Tangazo la Serikali namba 108 la mwaka 1999. Masharti hayo ni mwenye kutaka kuona mali hizo kuwa na malalamiko dhidi ya kiongozi anayehusika na kulipa ada ya shilingi 1,000/=. Taarifa za mali hizo mwananchi anaweza kuzitoa popote isipokuwa harusiwi kuzichapisha kwenye magazeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama mwananchi huyo anamtuhumu kiongozi kwa rushwa au wizi basi anaweza kupeleka taarifa hizo *PCB* au polisi. Hata hivyo kiongozi yejote anaweza kutangaza mali zake kwenye magazeti kama atataka kufanya hivyo yeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile kuongelea majukumu ya sekretarieti yanayoweza kufanywa na vyombo vingine kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, *PCB*, Usalama wa Taifa na vingine vingi ambavyo Serikali imejirudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekretarieti inafanya kazi zake kwa karibu na kwa ushirikiano na vyombo vingine kama Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, *PCB*, Polisi na Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Sekretarieti inashughulikia maadili ya viongozi maalum walijotajwa katika sheria, wakati vyombo vingine viliviyotajwa vina shughulikia maeneo maalum ya utawala bora kama rushwa na haki za binadamu. Nia ya kutenganisha vyombo hivi ni kujenga utaalam (*specialty* au *professionalism*) ya kushughulikia masuala haya. Hata kabla ya *PCB* kuundwa, rushwa ilikuwa inashughulikiwa na polisi. Lakini ikaonekana kuna haja ya kuwa na chombo maalum cha kushughulikia rushwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea juu ya walimu pamoja na watumishi wengine kutopewa likizo, hoja hii imetolewa na Mheshimiwa Halimenshi Mayonga. Tatizo hili lilitokana na mfumo wa menejimenti tuliokuwa nao na itapungua baada ya kupeleka mamlaka ya usimamizi kwa kila mwajiri na kuundwa kwa Tume ya Utumishi ya Umma, ambayo itasimamia utekelezaji wa masuala ya maslahi ya watumishi kwa kila mwajiri. Kila mwajiri sasa anatakiwa kuweka kwenye Bajeti gharama za likizo kwa kila mtumishi. Kila mwajiri anapomhamisha mtumishi lazima ahakikishe kwamba yale yote yanayokwenda na uhamisho yamekuwa tayari kabla hajamchukulia hatua. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni Makatibu Wakuu kutokuwa Wenyeviti wa Bodi za Ushauri wa Wakala za Serikali. Hoja hii imetolea na Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe. Wakala za Serikali zimeundwa kuboresha huduma ili kuhakikisha wakala zinabaki zaidi na Serikali. Lakini wakati huo huo zinatakiwa kufanya shughuli zake kibashara au kwa ufanisi. Bodi ya Ushauri imeundwa chini ya Katibu Mkuu. Sasa hivi ndiyo tathmini kuhusu utendaji wa taasisi hizi unafanyika. Matokeo ya tathmini hiyo ndiyo yatakayowezesha kubuni utaratibu bora zaidi wa usimamizi wa wakala hizo.

Hoja nyingine ni utekelezaji wa mikataba ya huduma kwa wateja na kama imeshaleta mafanikio. Hii ni sehemu ya utekelezaji wa programu ya uboreshaji utumishi wa umma. Sasa hivi tunafanya tathmini ya kuona kama ile mikataba ya huduma kwa wateja, imefanikiwa kuboresha utumishi.

Ningependa kutoa wito kwa wananchi wa Tanzania, kwamba mikataba ile imetolewa ili tusaidiane na Serikali katika kuona kwamba watendaji wanatimiza wajibu wao. Pale ambapo hawatimizi wajibu wao kila ofisi ina *mechanism* ya kupokea

malalamiko na ikiwezekana andikeni kwenye ofisi ya utumishi tutayapeleka kunakohitajika na utumishi yenyewe itachukua hatua zinazotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Janet Kahama ya kuwaenzi Viongozi Waasisi wa Taifa la Tanzania. Serikali imeandaa Muswada wa Sheria ya kuwaenzi Waasisi wetu na itawasilishwa Bungeni hivi karibuni, ni mategemeo yangu tutaona umuhimu wa kupitisha sheria hiyo na tutashukuru sana kama itapitishwa ili tuwe na mfumo rasmi wa kuwaenzi waasisi na viongozi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Mgana Msindai, alitaka kujua marekebisheso ya Sheria ya Utumishi wa Umma kama yatafanywa lini. Nazidi kumwahidi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine kuwa marekebisheso ya Sheria ya Utumishi wa Umma namba 6 (6) yako kwenye *process* ya kufanyiwa marekebisheso na pindi tutakopokuwa tayari tutaleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda vile vile kuongelea utaratibu wa malipo ya *SASE*. *SASE* ni utaratibu wa malipo ya kumotisha utendaji kazi wenye matokeo na ambao ni sehemu ya utekelezaji na sera ya malipo ya mshahara na ni utaratibu wa muda tu. Utaratibu huu kwa sasa unatumika katika Wizara mne. Vigezo vya kulipa *SASE* ni pamoja na kuwa mpango wa kimkakati, kuwa na mpango wa mwaka wa kazi wa kila mtumishi, kila mtumishi anayehusika kuwa na mkataba wa kazi uliotiwa saini kati yake na msimamizi wake wa kazi, kuwepo kwa mkataba wa huduma kwa mteja *sustainability* ya mpango huu ni kuwa kadri Serikali inavyokuwa na uwezo basi na sisi tunaendelea kuondokana na *SASE* na kutekeleza ile sera yetu ya ajira na ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningombaa kwa Idara ya Afya wangeweza kutumia *SASE* kuwalipa watumishi wa afya ambao wako sehemu za pembezoni na kwenye mazingira magumu. Kwa namna hiyo, tutakuwa tumetumia *SASE* vizuri katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu kudhibiti rushwa katika utumishi wa umma. Katika kupiga vita rushwa katika utumishi wa umma Ofisi ya Rais, Utumishi, imejitahidi kuchukua hatua zifuatazo:-

Kuanzisha utaratibu wa kubainisha mianya zaidi ya rushwa na kuziba kwa kubadili mifumo ya uendeshaji kwa mfano mikataba ya huduma kwa mteja, utendaji wa kazi wenye kuzingatia malengo, ajira zenye kuzingatia sifa na vigezo vinavyopimika na ushindani wakati wa kuajiri watumishi wapya. Kila Wizara kuwa na mkakati wa kupambana na rushwa na kutoa taarifa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kuwaelimisha watumishi wa umma juu ya maadili ya watumishi wa umma. Lakini vile vile ningependa kuongelea jambo moja dogo kwamba kwenye utumishi wa umma napo uzushi siyo utawala bora, kumzulia mwenzako kwamba anakula rushwa wakati hali rushwa siyo utawala bora. Tabia ya kuwazulia watu kwa sababu yoyote ile si nzuri na kama tutaendekeza kwamba tunakula kwa uzushi tutakuwa hatujengi utawala bora. Kwa wale ambao wana ushahidi na ninajua kwamba

kupata ushahidi wa rushwa ni vigumu kwa sababu rushwa ni sawa sijui niseme na kufanya mapenzi au ngono. Huwa watu hawatoi rushwa kwenye sehemu ya wazi wanatoa rushwa mahali ambako hawaonekani. Kwa hiyo, ni rahisi sana kumzulia mtu anachukua rushwa ambapo hachukui rushwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mimi nitatoa mfano, kwa mfano, tunapomaliza shule huwa tunapoanza kazi mara ya kwanza huwa tunakopeshana, unaendelea unakopeshana, mwenzako mara haji kukopa wewe unaendelea kumkopa yeye. Halafu inatokea yule ambaye ameacha kukopa kwa sababu amepata fedha mahali anamzulia yule anayeendelea kukopa hayo kwa kweli siyo mambo ya kuendekeza kwa sababu inawezekana na wale wala rushwa wanawenza kujificha kwa kuwasingizia wenzao ambao hawali rushwa ili wasionekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linawezekana kabisa kwa hivyo kama alivyoeleza Mheshimiwa Wilson Masilingi, ni kwamba lazima taratibu na sheria zilizowekwa zifuatwe kama sehemu ya utawala bora kufichua wala rushwa na siyo uzushi kuhusu rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia ningependa kusema kuwa utumishi wa umma ni kiungo muhimu katika shughuli zote za maendeleo hapa nchini. Aidha, utumishi wa umma umefanya mengi na mafanikio makubwa yanapatikana kwenye uchumi, siasa na kwenye huduma za kijamii. Pia utumishi wa umma, umechangia sana kuondoa tofauti mbalimbali nchini na hivyo kuleta umoja wa Kitaifa. Ni katika msingi huu ambapo utumishi wa umma umekuwa muhimili wa amani, usalama na utulivu pamoja na nyenzo muhimu ya kuleta umoja wa Kitaifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imelenga kuwa na utumishi wa umma wa kuaminika wenyе ufanisi unaofanya kazi kwa tija, unaoonyesha matokeo haraka ya kazi yake na usiogubikwa na rushwa na maadili yasiyo ya kiutumishi. Huu ndiyo msingi wa Utawala Bora, ambao ni muhimu katika kujenga Taifa imara, linaloendeshwa kwa misingi ya sheria, ukweli, uwazi na haki kwa wote. Serikali imara itatokana na watumishi imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja na ninawashukuru sana. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

FUNGU 20 - OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu 1001 - *Administration and General* 4,163,392,200/=

MWENYEKITI: Hebu watalaan pale mrekebishe hizi taa zimewaka hapa. Hebu endelea tuone kama inasikika. Mnasikia? Washa sasa.

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu 1001 Utawala na mshahara wa Mheshimiwa Waziri, wakati nikichangia kwa maandishi nilizungumzia kuhusu tatizo la rushwa kwenye fedha za *fumigation* ambazo zilipelekwa Mkoa wa Mara kwenye shule tatu. Fedha hizi zilipelekwa takribani mwaka mmoja na nusu uliopita. Mimi nilivyochangia nilitaka nielezwe tu nini kimefanyika, maana kuna kauli za kubezwabezwa wakati tunazungumzia habari za rushwa, tunaambiwa tuchangie, tuonyeshe ushahidi. (*Makofî*)

Sasa nikidhani kwamba ningepewa maelezo ya nini kimefanyika. Waziri wa Utawala Bora, alivyokuwa anazungumza sasa hivi anazungumka kwamba imeundwa Tume. Lakini nataka kusema si maelezo niliyokuwa nayategemea leo kwa sababu Serikali inataka Wabunge tusaidie Serikali kutoa ushahidi kuhusu tuhuma za rushwa na tunavyofanya hivyo tunaonekana kama vile tunakuwa watu ambao tumeharibikiwa, tumechanganyikiwa kidogo na akili.

Sasa mimi nilitaka Waziri anieleze ni ushahidi gani unatakiwa kwa sababu suala hili fedha zilikwenda kwenye Mkoa wa Mara, fedha hizi za kupeleka kufanya *fumigation* pale Shule ya Sekondari Tarime, Shule ya Ufundı Musoma Sekondari, Shule ya Sekondari Mara, kukatokea matatizo nikaviarifu vyombo vya dola. Nilivyotoa taarifa hizi nikamwalifu Waziri wa Elimu na Utamaduni yuko hapa, nikamwalifu Waziri wa Ujenzi, bahati mbaya hayupo, Serikali ipo. Mimi nashangaa ninavyoambiwa tena inaundwa Tume, Tume ya kitu gani? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kitu hiki kilifanyika mapema, iliundwa kampuni hapa ya kufanya kazi ya *fumigation* kwa muda wa wiki mbili, ilivyoundwa kampuni hiyo ya kufanya *fumigation* viongozi wa Wizara ya Elimu na Utamaduni, chini ya Waziri Mheshimiwa Joseph Mungai, wakapeleka fedha, nikamwalifu Waziri, wakaambiwa wale wakuu wa shule zile kwamba wanahitaji *Navy* apewe ile kazi, walivyokuwa wamemwambia fedha zile zikapelekwa zaidi ya milioni 54, *procurement procedure* haikufuatwa kabisa. Nikamwambia Waziri wa Elimu na Utamaduni hapa nikamfuata nikaonekana kama najikomba kwake, hii siyo nchi ya kujikomba kwa Mbunge mwenzangu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikamfuata Waziri wa Ujenzi, nikamweleza kuhusu tatizo hili ahaa! Hivi tunafikishwa mahali hapa tena naambiwa tena Tume inaundwa, Tume ya kufanya nini? Maana kitu hiki kilikuwa wazi pale pale, kampuni imeundwa siyo zaidi ya mwezi mmoja ipewe kazi na kazi ya *fumigation* ushahidi unapotea mapema, kwa hiyo, nikadhani wakati huo huo ndiyo kazi ingefanyika pale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *tender* haikufanyika, mtu amepewa kazi ya shilingi milioni 54 kwenye ku-*fumigate* hizi shule, leo tunaambiwa tulete ushahidi inaundwa Tume kwa matumizi gani ya fedha za walipa kodi wa nchi hii? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu bado tukizungumza kuhusu rushwa tunaambwa kwamba ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, dakika tano zako zimekwisha na nadhani hoja imeeleweka.

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Naomba maelezo ya Waziri, siungi mkono hoja naondoaa bado shilingi kwenye mshahara huu. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni kweli Mheshimiwa Ibrahim Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini alileta taarifa juu ya tuhuma ambazo amezitolea ufanuzi wa nyongeza sasa hivi.

Mimi nilichofanya nilimkabidhi *Major General*, Mstaafu Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa bila kucheleta na nikamtaarifu Mheshimiwa Ibrahim Marwa na amekuwa anafuatalia kweli tangu alipoleta malalamiko yake kwetu. Mimi nilikuwa namweleza jinsi ambavyo Mkurugenzi Mkuu anaendelea kulifuatalia. Ufanuzi nilioutoa sasa hivi wakati wa majumuisho kufuatia mchango wake wa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilikuwa ni kuweka bayana kwamba sasa hivi kinachofanyika kwa sababu zinatafutwa tuhuma za rushwa siyo wizi wa shilingi milioni 54 ambayo ingekuwa *straight forward case* ambayo isingeletwa kwa Waziri wa Elimu na Utamaduni wala Waziri wa Ujenzi, ingekwenda Polisi huko huko bila kuja hata huku Bungeni. Lakini kwa sababu matatizo ya rushwa ni magumu, tukapeleka kwenye Taasisi ya Kuzuia Rushwa na wao kwa sababu tunasema wafanye kazi pamoja na wenzao, wamenipa taarifa leo, sio Tume ile, Mkurugenzi wa Taasisi ya Kuzuia Rushwa akishirikiana na Polisi, akishirikiana na Usalama wa Taifa wanajaribu kutafuta ukweli.

Mhehsimiwa Mwenyekiti, hiyo sio Tume, huo ni uchunguzi wa kitaalam na sisi tunaaminii katika *prosecution* yaani uendeshaji wa mashtaka, sio *persecution*, sio kwamba ukishamtuhumu mtu, uhakikishe anafungwa ndio haki inatendeka. Tunataka haki itendeke hata katika kumfikisha kwenye utaratibu wa kumweka hatiani. Kwa hiyo, mimi naamini katika mwaka mmoja anaozungumza, tungeshindwa kabisa, tingesema hakuna kinachofanyika au tumekuta ni uwongo wa Mbunge amedanganya. Sasa ningemshauri Mbunge aturudishie shilingi, awe na subira kwa sababu alicholeta *actually* sio ushahidi wa rushwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, hajatoa shilingi bado.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Basi atuunge mkono tupewe hela tuendelee kupeleleza hii kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize jambo moja, sisi hatubezi michango ya Waheshimiwa Wabunge, tunaposema kuleta ushahidi. Huu aliouleta ni tuhuma na inachunguzwa ili tupate ushahidi, waende kortini na ikibainika kweli kama ni wizi

atafungwa kwa wizi, kama amehonga ili asijulikane kwamba hela imekwenda, hata kama ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Utamaduni, atashughulikiwa. Tunakwenda kwa uwazi ili kusudi na yeze ajue.

Sasa hakuna cha kubezana hapa, namsihi Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, hii sio *clear case* ya kuonesha tunabeza ushahidi wa Wabunge. Kwa sababu kama ushahidi ni wenyewe si unakwenda kortini? Sisi tunatafuta ushahidi ili twende na kwa kweli tumeheshimu na nimelifanyia kazi hatua kwa hatua. Kwa hiyo, ningepuuza ningesema usije na hujikombi kuja kwetu kwa sababu na sisi tukija Mara, Musoma Mjini hatujikombi, tunakwenda kwa Mbunge mwenzetu. Karibu sana Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, utukubalie, utuunge mkono tupewe hela twende kufanyakazi. (*Makofii*)

HOJA YA KUONDOA SHILINGI

MHE. IBRAHIMU W. MARWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kitu kimoja kwamba umesimamia vizuri majadiliano haya, maana nadhani tulichotaka kukiweka wazi ni kwamba wananchi na sisi wawakilishi tunapozungumza kwamba kuna rushwa na bado tunaambiwa kuleta ushahidi na ushahidi huu tunaambiwa tupeleke Mahakamani, basi ndio tunakatishwa tamaa kushughulikia tatizo hili. Maana kama tukipeleka hata hizo tuhuma tunaambiwa tupeleke Mahakamani ndiko kwenye kuweza kuthibitisha hilo, nadhani ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema bado siungi mkono hii hoja, naondoaa shilingi mpaka nihakikishiwe kwamba ni nini kinafanya kuhusu hili tatizo la hili suala ambalo ni la muda mrefu sasa. Naomba labda kwa mwongozo wako unieleze nini cha kuendelea kufanya hapa. (*Kicheko/Makofii*)

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, pengine hili la kuondoa shilingi limekuwa kwa wakati huu sio la kawaida, lakini maelezo na kanuni iko wazi ambayo ningependa kuwasomea. Kanuni ya 81(2)(c) inasema hivi: "Halikadhalika Mbunge ye yote aweza kutoa hoja isiyokuwa na mjadala ya kupunguza shilingi moja katika kifungu chochote cha fungu hilo. Madhumuni halisi ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyetoa aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsusni ambalo dhahiri linahusika na kifungu hicho. Hoja hiyo itaamuliwa bila mjadala wowote. Lakini Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu yake kwa hoja hiyo na endapo hoja itakubaliwa, basi kifungu kinachohusika kitakuwa kimepitishwa kikiwa na upungufu huo wa shilingi moja." Sasa Mheshimiwa Ibrahimu Marwa ametoea hoja yake na sijui pengine Waziri angependa kutoa maelezo kabla sijawahoji juu ya kutoa shilingi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Namshukuru sana Mheshimiwa Ibrahim Marwa, yeye ameweka sharti kwamba hatatoa shilingi iwapo maelezo ya kutosheleza yatatolewa kuhusu ni kipi kinafanyika sasa hivi. Nayatoa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachofanyika sasa hivi ndugu yangu Ibrahim Marwa, ni kuchunguza kuhakikisha kwamba tunajiridhisha na haya ambayo umetusaidia kuyapata kuwa chanzo cha uchunguzi wa kina kuweza kupata uhakika wa kumweka jela huyo kama ni mwizi ili itosheleze. Kwa hiyo nakushukuru, ndio maana hatukupuuza ushauri ulioutoa tukasema sasa tuijandae, maana yake tukienda kwa Jaji au kwa Hakimu yeye anachotaka ni lazima tumridhishe amshughulikie mtu, ni kosa la jinai. Kwa hiyo, ndugu yangu Ibrahim Marwa ninachojaribu kukuhakikishia sasa hivi, hatujapuuza hicho kitu, lazima kifanyike na lazima nikuletee taarifa kama ulivyoniletea mimi. Nakuomba uniachie hiyo shilingi tupite bila matatizo ndugu yangu Ibrahim Marwa. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Hoja hii tena sio ya Mheshimiwa Ibrahim Marwa, ameileta Bungeni, Bunge liamue kuondoa shilingi ama kutoondoa shilingi.

(*Hoja iliamuliwa na Kukataliwa*)

MWENYEKITI: Baada ya Bunge kukataa kuondoa shilingi, sasa namwita Mheshimiwa Thomas Ngawaiya.

MHE. THOMAS NGAWAIYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nami nataka ufanuzi kidogo. Kabla ya hapo, niseme tu kwamba kwa mara ya kwanza majibu ya Mawaziri yalikuwa ni mazuri sana kuliko siku zote, nawapongeza. Lakini kuna mambo ambayo yanataka ufanuzi na mengine yanaweza yakawa juu ya Waziri kwa mfano mishahara asilimia 12 iliyopandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka ufanuzi ni kwamba sasa hivi vitu vimepanda mara mbili, umeme mara mbili, usafiri mara mbili, mafuta ya Petroli yamepanda, sasa huyu mtu wa kima cha chini tunayemzungumzia, kuna ufanuzi gani wa kumpa *only ten percent* kwa nini asipewe mara mbili ili aweze kumudu maisha yake? Ndiyo hicho nilikuwa nataka kuuliza.

Pili, nilitaka hii takrima vile vile iwekewe mipaka. Kama takrima, tumezungumza sawa, ni vyema, lakini sasa magunia mangapi ya ulezi? Mbege kiasi gani? Kwa hiyo, kuwe na mipaka. Kama hakuna mipaka, nataka maelezo hayo. Ahsante sana. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kwa swali alilohitaji ufanuzi Mheshimiwa Thomas Ngawaiya. Wakati nikifanya majumuisho ya hoja yangu na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, nilieleza kwa kirefu vigezo vinavyotumika kuongeza mishahara kila mwaka. Nimeeleza kwamba Bajeti ya mishahara ya Serikali au watumishi wa umma inatumika kwa mishahara kwa kupandisha vyeo na kwa ajira mpya. Kama fedha zote zitawekwa kwenye nyongeza ya mishahara maana yake ni kwamba

walimu wasiajiriwe wakati madarasa mengi yamejengwa, Watumishi wa Afya ambapo Zahanati zimejengwa nyingi wasiajiriwe na kusipandishwe cheo hata kimoja Serikalini. Ndio maana kwa kutumia utaalamu wa Utumishi tukaona kiasi tunachowenza kukiongeza mwaka huu ni kati ya asilimia tisa na asilimia 12.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwamba bei ya mafuta na bidhaa nyingine zinapanda, lakini ni kweli vile vile ukiangalia hii *drawing* tuliyotoa kwenye kitabu cha hotuba, utaona kila wakati mishahara imekuwa juu ya kadri mfumko wa bei unavyokuwa. Kwa hiyo, ukiona kuna tofauti kubwa kati ya mfumko wa bei na nyongeza ya mishahara utakuta kwamba huu mfumko wa bei hautakuta nyongeza ya mshahara iliyotolewa. Namwomba Mheshimiwa Thomas Ngawaiya pamoja na Watumishi wa Umma wakubali kwamba Serikali imejitahidi kutoa nyongeza hii pamoja na kugharamia yale masuala mengine ndani ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu takrima, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Utawala Bora, anisaidie kujibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, anashauri kwamba tuweke mipaka juu ya takrima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uchaguzi kadri kifungu ambacho sinacho sasa hivi kinavyozungumza, kwa kuzingatia kwamba sio rahisi kupima mipaka ya takrima, imeeleza kwamba ni kwa mujibu wa mila na desturi zetu ambazo tunazichukulia kwamba hiki kilichotolewa wakati wa uchaguzi hakivuki mipaka kuweza kufikiriwa kwamba ni rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna utata, basi mlalamikaji anaiweka kama hoja ya kulalamika kupinga uchaguzi kwamba hii haikuwa takrima ilikuwa rushwa na ushahidi utatolewa mbele ya Mahakama na Mahakama Kuu itaamua kwamba kweli hapa ulivuka mpaka na kwa hiyo, uchaguzi wako unatenguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatahadharisha Wabunge, kama una mashaka na mipaka ya takrima, usitoe kabisa ili unusurike, usije ukatenguliwa uchaguzi wako. Nashukuru sana. (*Kicheko/Makofi*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 30 - OFISI YA RAIS, BARAZA LA MAWAZIRI

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	56,939,078,800/=
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	544,424,700/=
Kifungu 2001 - <i>Cabinet Secretariat</i>	914,946,300/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 32 - OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA

Kifungu 1001 - *Administration and General 2,908,065,900/=*

MHE. BERNARD K. MEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nachangia hoja yangu mchana, nilieleza kero mbili ambazo ningependa ufanuzi na ningependa nirudie kwa sentensi moja moja kwamba wananchi wa Mkoa wa Lindi, wanashtuka na kasi ya uhamaji wa viongozi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitamka kwamba katika kipindi cha miaka mitatu na nusu ukiachilia mbali Wilaya nyine za Lindi, lakini Wilaya mbili pamoja na Mkoa tayari viongozi wasiopungua 24 wamekwishahama. Wengine walikaa miezi tisa, wengine wamekaa mwaka mmoja kwa majina tunawajua na Mheshimiwa Waziri amesema, kuhamza huku kunategemea maelewano kati ya mwajiri na yule anayehamishwa.

Ningependa kujua tu, wale watu walikuwa imara, afya zao zilikuwa nzuri, hawakuwa wanaumwa ngirimaji kwamba walikuwa wanahitaji kuja kukaa Dar es Salaam, ni maelewano gani haya yanayowafanya waajiri wakubali kuwahamisha viongozi wao kutoka Mkoa wa Lindi katika kipindi cha mwaka mmoja tu kupeleka sehemu nyine? (*Kicheko*)

La pili, nilieleza kwamba changamoto moja ya Idara ya Utumishi iwe ni kujaribu kuviangalia upya vipengele vya *by-laws* hasa vya uhamiaji ili Utumishi ijiridhishe kwamba haiwaumizi watumishi wake bora na waaminifu na wachapakazi katika nchi hii. Nikatoa mfano kwamba wapo watumishi na nina hakika sio mtu mmoja tu, nikatoa mfano wa mtumishi wa Mtwara, Mkurugenzi wa Mji ambaye ameachishwa kazi bila kupata chochote kile kwa sababu wazazi wake hawakuzaliwa Tanzania japokuwa yeye mwenyewe kuna ushahidi kwamba kazaliwa Tanzania na nimesoma naye, amesoma mpaka amepata stashahada na amekuwa Mkurugenzi wa Mji. Sasa hivi hana kazi na anasota na familia yake. Huyu ni mtumishi wa Serikali aliyeefanya kazi zaidi ya miaka 20, anakaa nyumbani bila kazi yoyote.

Niliomba Utumishi wanihakikishie saa hizi kwamba moja, suala hili litafikishwa mahali pake, lakini pili, kwamba vipengele vya sheria vinavyowaumiza wafanyakazi wetu hasa hiki cha *immigration* kilichopitwa na wakati, kinachunguzwa upya ili Muswada uletwe kwenye Bunge hili tufanye mabadiliko. Hatuwezi kuwaumiza Watanzania waliozaliwa katika nchi hii na tunawaadhibu eti tu kwa sababu wazazi wao wamezaliwa nje ya nchi wakati nchi za wenzetu zimeanza kurekebisha kasoro hizi. Naomba maelezo. (*Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ufanuzi kwa suala la Mheshimiwa Bernard Membe ambalo kweli ndio alilozungumzia kama mchango wake wakati wa majadiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhamisho wa mara kwa mara, iliwezekana pale kabla ya Sheria ya Utumishi wa Umma hajapitishwa hapa Bungeni. Lakini nilieleza katika maelezo yangu wakati najumuisha hoja yangu kwamba baada ya sheria hii kupita, sasa si rahisi kwa Watumishi wa Umma kuhamishwa holela holela bila kufuata utaratibu ambao upo. Ni kweli vile vile kwa mujibu wa sheria hii mpya, sasa tuna Tume ya Utumishi wa Umma ambapo Mtumishi akiona kwamba anafanyiwa isivyo haki, basi anaweza kulalamika na malalamiko yake yakafikishwa kwenye Utumishi wa Umma. Lakini napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ili tuweze kuboresha siku za usoni, nitaliangalia hivi ni kwa nini hawa watumishi wamekuwa wakihamishwa mara kwa mara. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Bernard Membe, avute subira ili tuangalie na ninahakikishia kwamba kwa kweli kwa sheria hii mpya tutakuwa tunafuata utaratibu, lakini ningeomba vile vile Mkao wa Lindi kama alivyokuwa amechangia Mheshimiwa Bernard Membe kwamba wakati miundombinu inaboreshwile vilenamslahi mengine ya watumishi yaboreshwe kama nyumba na mambo mengine ambayo yanaweza yakavutia watumishi kubaki Mkao wa Lindi. Lakini namhakikishia kwamba nitalifanyia kazi. (*Makofî*)

Kuhusu suala la pili la kuondolewa kazi Mkurugenzi wa Mji wa Mtwara, kwanza kuna suala la uraia ambalo linahusu Sheria ya Uraia. Ni kweli kwa mujibu wa sheria ya nchi yetu, kama mzazi wako si mzaliwa wa Tanzania, wewe sio raia. Ila unaweza ukawa raia kwa kufuata zile taratibu ambazo zimebekwa. Kwa hiyo, nawaomba Watanzania wote, wakati sheria hii bado hajaangaliwa upya, wahakikishe kwamba wanahalalisha uraia wao na hakuna mtu atakayewanyima kama kwa kweli wanastahili. Lakini kuhusu hili la mtumishi ambaye ametumikia miaka 20, wakati akiuhalalisha uraia wake sidhani kama kutakuwa na tatizo la yeYe kubaki kwenye utumishi wa umma na kwa wakati huu kama ilikuwa kutokujua sheria ambapo kwa kweli kutokufahamu sheria si *excuse*, ningesema kwamba pengine hata basi abakie kama mtumishi wa muda lakini hilo nalo ni la utumishi, naomba vile vile tulifanyie kazi kwa sababu kalileta humu Bungeni na si rahisi kutoa majibu ya uhakika lakini nina hakika tutaliangalia ipasavyo na tutampa taarifa Mheshimiwa Mbunge. (*Makofî*)

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba tu maelezo ya kina kwa swali la (a) na (b).

(a) Mwaka 2003 katika Bajeti kama hii nilizungumzia juu ya mradi mkubwa wa Rais (Mfuko wa Rais *TASAF*), nikapata majibu kuhusu Sekondari ya Ndido kwamba wananchi wameibua mradi wa kujenga Sekondari pale na wamechangia matofali 5000, mchanga lori 85, mawe lori 86, ng'ombe (makami) 200, ng'ombe (kishibor) 60 na michango wa *TASAF* ambayo imeandikwa baada ya kuiibua, milioni 97. *DC* aliyejukua Kiteto Ndugu Ole-Molloimet, alipofika akasitisha kabisa mradi huo kwa nguvu zake.

Nilizungumza mwaka 2003 na ushahidi kwamba hata hiyo Sekondari Waziri Mkuu naye alichangia shilingi 500,000/=. Mheshimiwa Joseph Mungai amekwenda akathibitisha hiyo michango ya wananchi, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mwenyekiti wa *LAAC* na Kamati yake wamekwenda wamethibitisha na ule mradi sasa hivi umefutwa na yule *DC* amesimamisha michango yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujua tunapozungumza hivi na kuthibitisha na naongea sasa hivi na Watanzania wote, hivi Serikali inaonaje? Inaendelea kumlinda mtu wa namna hiyo ambaye anawaabisha Watanzania na nguvu zao na bila kufuata kanuni na taratibu za Mfuko wa Rais, huu ndio utawala bora? (*Kicheko/Makofi*)

Naomba majibu kwa hilo na nina hakika mimi ni Mbunge mzoefu nikisema nitoe shilingi tutapata taabu hapa. (*Kicheko/Makofi*)

(b) Katika majibu ambayo nimeyapata, nilichangia hoja ya Waziri Mkuu nikachangia vizuri katika Utawala Bora. Majibu ya Serikali ambayo niliyapata katika jengo hili yalinisumbua sana. Niliambiwa *DC* huyo tumekuletea kwa sababu wewe ni Mmasai mwenzake. Sijaelewa kabisa Mbunge akilalamika kuhusu mtumishi anatafutiwa kabilalake. Kama sasa utawala bora ndio umebadilika, tuelezwwe kabisa kwamba kama Mbunge ni mkorofsi, basi anatafutwa kabilalake ili aende akamkulize, ndio utawala bora sasa ambao tunaafuata. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata jibu lingine ambalo limenishangaza sana. Nikaambiwa kwamba wananchi wangu wa Kiteto wanansikiliza...

MWENYEKITI: Muda umekwisha, dakika tano, kengele imegongwa.

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza maelezo kwa hayo halafu nitaendelea. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Benedict Losurutia. Aliyosema ni kweli kabisa, alieleza kushangazwa kwake na alichoeleza ni kwamba Mkuu wa Wilaya ya Kiteto aliingilia kati kupinga maamuzi ya wananchi waliyokuwa wameamua ya kujenga Sekondari. Nilipofutilia na viongozi Watendaji wa Mfuko wa *TASAF* wakanieleza kwamba Mbunge alikuwa sahihi kama nilivyokuwa nimemweleza ndani ya Bunge hili kwamba Mkuu wa Wilaya hana uwezo katika utaratibu wa *TASAF* kupinga maamuzi ya wananchi kwa sababu misingi ya *TASAF* ni Mfuko ule wa kuwezesha wananchi kutekeleza au kutimiza azma yao ya kujiletea maendeleo na Mkuu wa Wilaya anapashwa kuelekeza sio ku-*dictate* juu ya maamuzi haya. (*Makofi*)

Napenda kuchukua nafasi hii kumsihi Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Waziri Mkuu anasikiliza yuko kwenye Ukumbi huu, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI yuko humu, Serikali nzima tupo na wananchi wanatusikia. Awamu ya pili ya *TASAF* ikianza, pesa zikiwepo, sasa sio suala la Mkuu wa Wilaya ni suala la wananchi wanataka nini na Sekondari lazima ijengwe. (*Makofi*)

MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA: Mimi ni muungwana na sitaki kujisifu. Lakini wananchi wanaelewa hili tatizo sasa. Naomba Serikali, sitaki kuipeleka Serikali initamkie sasa hivi, lakini naomba Serikali ichukue hatua ambayo inaona kwamba ni bora kwa ajili ya kunusuru watu wa Kiteto kwa jambo hili. (*Makofi*)

La pili, nilikuwa sikumalizia, majibu ya Mmasai kupelekwa kwa Mmasai au Mngoni kupelekwa kwa Mngoni au Mbunge kuweza kupewa fursa ya kumchagua *DC* wake, ndiyo majibu niliyopata, ili kama sasa ndio taratibu tuweze kuelewa. Hii iko kwenye *Hansard*, sio kwamba nazua.

Sasa ili Serikali iweze kufuta kwenye hii *Hansard* kwa sababu Watanzania wamesikia hiyo kwamba Mbunge akilalamika anapelekewa kabilia lake, tunaomba kama ndio uongozi bora ambao tunaufuata tuambiwe. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule *DC* sikulalamika, aliondolewa, akaingia badala ya Ole-Molloimet. Nataka nifanye *clarification*, amechukuliwa Pasto Bimbule amepelekwa Ukerewe ambako ni kwao, yeze tayari ameshahamishwa Ukerewe ambako ni kwao amekwenda Tabora, Benedict Losurutia hayuko kule. Aliyofanya nayo kule kumhamisha mimi sijui kwamba huyu Mbunge analalamika. Hivi Mbunge ndiye analalamika, ma-*DC* wote wanazunguka nchi!! (*Kicheko*)

Mimi naomba tu kitu kimoja kwamba katika majibu ndani ya Ukumbi huu, Wabunge wajibiwe kama inavyostahili. Mbunge ajibiwe vizuri kabisa. Mimi sikuwepo, kumbe mnatuangalia hapa kama huyu Mbunge yupo au hayupo, kama hayupo unamkandamiza tu, maana akiwepo angeshika shilingi, ungemjibu pale pale. Basi, Mbunge ajibiwe inavyostahili awepo, asiwepo, ajibiwe kwa ustaarabu. Naomba sasa nijibiwe Mmasai kwa Mmasai ndio nitaridhika. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kusema kwa niaba ya Serikali kwa sababu mimi sikumbuki haya majibu, lakini Mheshimiwa Mbunge hawesi kusema uongo. Kama ilitokea kauli ya namna hiyo kwamba ukorofi wake kwa sababu ni Mmasai sasa anapelekewa na Mmasai mwenzie wadhibitiane, haikuwa kauli sahihi. Ilikuwa labda utani na tunamwomba radhi kwa maudhi hayo. Sio msimamo wa Serikali Mnyamwezi kumpelekeea Mnyamwezi mwenzie kama ni mkorofi au Mmasai kumpelekeea Mmasai mwenzie.

MBUNGE FULANI: Wahaya!

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, UTAWALA BORA: Wahaya huwa sio wakorofi. (*Kicheko*)

Ninachotaka kusema hapa ni kwamba napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge, wananchi wamesikia na viongozi wetu wakuu wamo ndani ya Ukumbi huu wamesikia, ukorofi wa huyo *DC* wameusikia.ya ukumbi huu amesikia kwamba ukorofi wa huyo *DC* wameusikia. Hoja zake anatoa mifano, tutafuatilia ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka na watu wanahamishiwa kwenye kwenye vituo siyo kwa ukabila bali kwa utendaji wao na kama hakidhi mahitaji atadhibitiwa na mamlaka zinazohusika zitamshughulikia. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitisha na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	85,337,600/=
Kifungu 2001 - <i>Policy Development</i>	265,993, 800/=
Kifungu 2002 - <i>Management Services</i>	134,714,800/=
Kifungu 2003 - <i>Establishment</i>	304,103,600/=
Kifungu 2004 - <i>Ethics Division</i>	90,254,700/=
Kifungu 3001 - <i>Human Resource Development</i>	603,825,400/=
Kifungu 3002 - <i>Civil Service Training Centre</i>	68,220,200/=
Kifungu 3003 - <i>Tabora Secretarial College</i>	54,393,000/=
Kifungu 3004 - <i>Gender</i>	20,000,000/=
Kifungu 4002 - <i>Management Information System</i>	120,662,400/=
Kifungu 4003 - <i>National Archives</i>	346,919,800/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 33 - ETHICS SECRETARIAT

Kifungu 1001 - *Administration and General* 690,735,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila mabadiliko yoyote)*

FUNGU 94 - PUBLIC SERVICE COMMISSION

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	1,290,840,300/=
Kifungu 2001 - <i>Civil Service</i>	669,582,600/=
Kifungu 2002 - <i>Local Government Service</i>	753,275,100/=
Kifungu 2003 - <i>Teachers' Service</i>	2,434,847,100/=

Kifungu 2004 - *Fire and Immigration Service* 597,377,000/=

Kifungu 2005 - 647,945,600/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila ya mabadiliko yoyote)*

FUNGU 30 - PRESIDENT'S OFFICE AND CABINET SECRETARIAT

Kifungu 1001 - *Administration and General* 34,331,254,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila ya mabadiliko yoyote)*

**FUNGU 32 - PRESIDENT'S OFFICE - PUBLIC SERVICE
MANAGEMENT**

Kifungu 2001 - *Policy Development* 7,972,910,500/=
Kifungu 2002 - *Management Services* 12,845,342,000/=
Kifungu 2003 - *Establishment* 967,215,000/=
Kifungu 2004 - *Ethics Division* 298,700,000/=
Kifungu 3001 - *Human Resources Development* 2,251,223,000/=
Kifungu 3002 - *Civil Service Training Centre* 707,754,000/=
Kifungu 3004 - *Gender* 1,120,327,500/=
Kifungu 4002 - *Management Information System* 3,799,028.000/=
Kifungu 4003 - *National Archives* 6,029,100,000=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi
bila ya mabadiliko yoyote)*

(Bunge lilirudia)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge Tukufu likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi limepitia Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba kutoa hoja kwamba taarifa ya Kamati sasa ipokelewe na makisio haya yapitishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi
wa Umma ya mwaka 2004/2005 yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Baada ya kufika hapo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 8 Julai, 2004 saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.38 jioni Bunge lilahiriwa mpaka siku ya Alhamisi
tarehe 8 Julai, 2004 saa tatu asubuhi)*

